Kikao cha Tisa - Tarehe 28 Mei, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2014/15.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha mezani Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Katiba na Sheria kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka 2014/15.

Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 8
Kutokamilika Ujenzi wa Maegesho ya *'Land Craft'*

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe sana Mhe. Naibu Waziri, tunafanya hapa kwa niaba ya wananchi wakati ninapouliza swali aliangalie kima na mantiki yake na ukweli wa swali hili lilivyo. Kwa heshima ya hali ya juu serikali itoe majibu ya suala hili.

Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya 1984 inampa mtu haki ya kufanya biashara iliyokuwa halali na kwa kuwa kuna eneo lililotengwa kwa ajili ya meli za *'Land Craft'* ambalo halijakamilika ujenzi wake na vyombo vyengine kushindwa kutumia eneo hilo kinyume na ilivyoahidiwa na wafadhili wa ujenzi huo Kampuni ya *Azam Marine.*

(a) Kwa kuwa vyombo vya *'Land Craft'* vinafanyakazi kwa kubahatisha hadi maji yanapojaa kutokana na mradi huo kutokamilika serikali ina mpango gani kuwanusuru wafanyabiashara wanaoendelea kupata hasara.

(b) Kwa kuwa lengo la matumizi ya eneo hilo limekwama na badala yake kunufaisha Kampuni ya *Azam Marine* pekee, kwa nini bandari ya Forodha Mchanga isiendelee kutumika ili uwanja wa biashara uwe sawa.

(c) Kwa kuwa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 inapiga vita ubaguzi, je, haki na usawa uko wapi kama mfanyabiashara mmoja anawekewa mazingira mazuri ya kufanya biashara na wengine kuachwa kukumbana na vikwazo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suala lake Nam. 8 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi, naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, sura ya 3, Ibara ya 11, 12(1), (2), (3), (4), (5) imeeleza kwa kina nini haki za binaadamu likiwemo suala la usawa mbele ya sheria, pamoja na kupatiwa haki na fursa nyengine nchini. Aidha, Katiba hiyo hiyo imetoa fursa ya kuanzisha sheria kadhaa kwa lengo la kuendesha shughuli za serikali vizuri zaidi kwa maslahi ya wananchi. Miongoni mwa sheria hizo ni sheria nambari 1 ya mwaka 1996 iliyoanzisha Shirika la Bandari la Zanzibar kwa lengo la kuimarisha huduma bora zaidi kwa watumiaji wake.

Mhe. Mwenyekiti, kwa madhumuni hayo hayo ndipo Shirika la Bandari lilipopata mshirika wa maendeleo Kampuni ya *Azam Marine*,wamekubaliana naye kwa kushirikiana na kuendeleza ujenzi wa jengo la abiria pamoja na chelezo kwa ajili ya huduma kwa meli za *LCT,* yaani *Land Craft.* Aidha, Shirika la Bandari pamoja na serikali tunashukuru sana Kampuni ya *Azam Marine* kwa uzalendo na mapenzi yake kwa nchi yetu. Tunatambua gharama zilizotumika kwa ajili wa ujenzi wa chelezo pamoja na jengo ni kiasi kisichopungua shilingi bilioni mbili. Aidha, kama vilivyo kwa jengo la abiria, chelezo kile ni mali ya Shirika la Bandari na watumiaji wake ni wananchi wote zikiwemo meli za watu kadhaa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kulitanabaisha Baraza lako tukufu kwamba ujenzi wa chelezo hicho unaendelea na kwa hatua zinazoendelea hivi sasa ni uchimbaji ambapo kwa hivi sasa Kampuni ya *Coastal Drainage* ambayo ni Kampuni tanzu ya *Azam Marine* wanakamilisha unununzi wa mashine kubwa na ya kisasa kwa ajili ya uchimbaji huo na kuajiri mtaalam bingwa kutoka Nigeria kwa ajili ya ushauri na usimamizi mzuri zaidi.

(a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu kupitia Shirika la Bandari limezipangia meli za aina ya *"Land Craft"* kufunga Gati na kushusha au kupakia mizigo katika sehemu mbili (2). Sehemu ya kwanza, inategemea na wingi wa maji ni Gati Kuu *(Berth Nam. 3),* pamoja na kwenye *"Slipway"* mpya, yaani hicho chelezo kwenye Gati ya abiria. Kwa ufumbuzi wa muda wa kati, nadhani zoezi la uchimbaji likikamilika tatizo la kushindwa kufunga meli kwenye chelezo kilichopo hivi sasa litakuwa limepatiwa ufumbuzi.

Aidha, kwa mpango wa muda mrefu na wa kudumu, tuombe mradi wa bandari ukamilike, lakini kwa muda wa dharura kuwanusuru kwao ni kufuata maelekezo ya vikao husika ili kuzingatia muda pamoja na upungufu wa vifaa husika. Tukizingatia maelekezo ya utaratibu, tunaamini kadhia hii itakuwa imepatiwa ufumbuzi kwa muda wa dharura.

(b) Mhe. Mwenyekiti, matumizi ya *Slipway* yanawanufaisha Kampuni zote na wala Kampuni ya *Azam Marine* peke yake, kwani baadhi ya wakati hata vyombo vya Kampuni hiyo hushindwa kutumia sehemu hiyo na kutumia Gati kuu *Berth* Nambari 3, kama zinavyofanya Kampuni nyengine. Msingi mkubwa ni kina cha maji ambacho hakitegemei aina ya meli, ndio kijae au kupungua kwake.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali imeamua eneo la Forodha Mchanga lisitumike kwa kushusha au kupakia mizigo kwa sababu za kiusalama wa nchi pamoja na uhifadhi wa Mji Mkongwe. Hata hivyo, inapotokea dharura maalum ambapo dharura hiyo lazima ithibitishwe na vyombo husika vya Serikali, ndipo ruhusa maalum itatolewa.

Mhe. Spika, naomba nimjulishe Mhe. Mjumbe kwamba tangu kusimamishwa matumizi ya eneo hili kwa ajili ya upakizi na ushushaji wa mizigo wananchi wanaotumia maeneo hayo wakiwemo na wageni wameonesha kufurahi na kuridhika na utulivu uliyokuwepo hivi sasa.

(c) Mhe. Spika, Wizara yangu haioni kama kuna mazingira mazuri iliyowekewa Kampuni moja kwani Wizara yangu inatoa fursa na mazingira sawa kwa wote kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Tunaamini hali iliyopo hivi sasa ni ushindani wa kibiashara, yaani *Fair trade competition*. Hivyo, kila mmoja ana nafasi ya kutengeneza wigo wa ushindani huo dhidi ya mwengine. Ni msingi huo huo wa Katiba unaoruhusu wafanyabiashara na wananchi wengine kuanzisha ushindani wa kutoa huduma bora na nzuri kwa wananchi wake huku serikali ikisimamia sheria na taratibu husika.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri, sijui niseme yana afya au hayana afya, lakini tuendelee, ni sababu gani zilizosababisha kukaa kikao tukakubaliana baina ya mimi na wewe saa tisa kabla chombo kufunga, ukafika baadae saa 10 ukaja kunigeuzia kibao kwa nyuma, ukanambia utaratibu huu haukubaliki, mpishe mwenzio ambaye ndie aliyejenga gati. Je, malalamiko haya baina mimi na wewe nishakueleza kama mara mbili tatu kuna wananchi wanaumia na mali zao. Ninafikiri utakuwa tayari kuwajibika pindipo...

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, anavyosema simsikii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, Mhe. Naibu Waziri, hasikii huku sasa, hebu isogelee hiyo *microphone* ili uweze kuongea vizuri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba bora nisiendelee tena kuuliza swali la nyongeza nikae kitako, naona tutafika pahali, hatofika pahali. Naomba kukaa kitako.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu kwamba huna swali jengine au vipi?

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Sina swali jengine Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya majibu ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyaeleza, naomba nimuulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Waziri, amekiri kwamba Kampuni ya *Azam Marine* imeekeza kwenye ujenzi wa chelezo na *Passengers terminal building* ambalo ni zaidi ya bilioni mbili, lakini muekezaji huyu huyu anaomba wizara hii kupitia bandari kupatiwa chumba cha ofisi pale bandarini kwa ajili ya Kampuni yake. Je, ikiwa yeye ameekeza zaidi ya bilioni mbili na wakati huo huo wanamnyima chumba ambacho baadae kitakuwa ni mali ya bandari. Haoni kwamba ni kuwadanganya wawekezaji. lakini hawana nia nao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini (b) miundombinu ile ni miundombinu ya mali ya serikali kwa maana chini ya bandari, kwa nini baadhi ya vyombo wanapofunga kwenye hiyo chelezo ambayo muekezaji ameekeza, inaonekana kama kwamba wao hawana haki wakati ni mali ya Shirika la Bandari.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Mwenyekiti, swali la kwanza, ameuliza kwamba, kwa nini bandari tunamnyima nafasi Kampuni ya *Azam Marine* pamoja na mema ambayo anayatendea nchi? Kwa nini tunamnyima nafasi ya kupata chumba kwa ajili ya kufanya ofisi?

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Kampuni ya *Azam Marine* imeonesha nia ya kutaka kujenga jengo kwa ajili ya kupata huduma za ofisi kwa ajili ya kuuzia tiketi na ni kweli wamewasiliana na Shirika la Bandari, Shirika la Bandari wamewasiliana na serikali, serikali haijaonesha kipingamizi chochote. Hatua ziliopo ni kwamba Shirika la Bandari wameitaka Kampuni ya *Azam Marine* kuwasilisha michoro, michoro ipelekwe katika taratibu husika kuona kwamba wenzetu wa Mji Mkongwe na aina ya mchoro wanaotaka kujenga.

Mhe. Mwenyekiti, mazungumzo yaliyopo kwamba *Azam Marine* anataka kujenga *ground floor,* mapendekezo ya Shirika la Bandari kwamba Ofisi hiyo ni vyema ikijengwa *ground floor* iwe na uwezo wa kubeba ghorofa moja. Kwa maana kwamba msingi wake uwe wa kuweza kubeba ghorofa moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, madhumuni na mategemeo ya Shirika la Bandari kwamba ujenzi huu utafanyika. Serikali haina pingamizi tunakamilisha taratibu, mjenzi huyu yupo, fedha zipo na sisi kama Shirika na Serikali hatuna pingamizi nae, tumeshazungumza maelezo yaliyopo ni kukamilisha taratibu. Kwa hivyo, si kweli kwamba mshirika huyu serikali imemzuilia nafasi ya kutaka kujenga.

(b) Mhe. Mwenyekiti, nadhani aliyeuliza hili swali pengine hafaham vizuri hiki chelezo kilipo. Chelezo hiki maji yakijaa kinakuwa kina-*tide* isiyozidi mita nane mpaka mita 9. Meli ya *Azam Link* ambayo ndio meli pekee ina uwezo wa kufunga kwa mfumo wa *Land craft* kwa maana kwamba *row-row,* lakini ni meli ambayo ina mkuku na ina propela, inatofautiana na meli nyengine. Kwa hivyo, kama tatizo la maji meli, hii ndio inayoathirika zaidi na upungufu wa maji kuliko meli nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, na ukiangalia katika ratiba zao za wiki, meli ya *Azam Marine* inafunga siku ya Jumatano, siku ya Alhamisi na siku ya Jumamosi, zinapokuwa zimerudi safari ya Dar-es-salaam na katika muda wote wa siku si zaidi ya masaa 2 anayoyatimia, muda wote uliobakia kwa siku pamoja na kiwango kidogo cha maji, meli zinazotumia, Aziza, Buraq na meli nyengine ikiwemo ya *MV* Khadija.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, sio kweli kwamba chelezo hiki Makampuni mengine yakitumia yananyanyasika au kana kwamba sio chelezo chao. Chelezo hiki wanaonufaika zaidi ni Makampuni

mengine kuliko Kampuni ya *Azam Link*, kwa sababu meli yake yeye inahitaji kina kikubwa zaidi cha maji kuliko hizi meli nyengine.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliono: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza napenda kumshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kutoa majibu mazuri ya swali isipokuwa mimi nina nyongeza ndogo tu. Katika meli ambazo zinatumia chelezo ile meli zote hizi za *LCT* zilizopo haziruhusiwi kuchukua abiria. Kwa hivyo, ni meli za mizigo. Sasa kama ni meli za mizigo meli ile ina *schedule* yake ya kutoka Pemba na Zanzibar, kila siku ya Alhamisi kutoka Pemba, Jumatano inakwenda na siku ya Jumapili inarudi kutoka Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa siku hizi za Alhamisi na Jumapili kwa jioni ndio huwa kuna tatizo hilo linalozungumzwa kwa sababu ile lazima ishushe abiria pale, lakini mimi binafsi yangu nimepita mara 4 au 5, nimeikuta Buraq 3 inapakia gari au mizigo mengine. Kwa hivyo, ni sahihi kwamba chelezo kile hakitumiki kwa *Azam Marine* tu, lakini kinatumika na Kampuni nyengine, isipokuwa kutokana na hizo siku mbili za Alhamisi na Jumapili, hizo inawezekana kukawa na tatizo kwa sababu lazima iwepo na *Schedule* ya kutoka Pemba, halafu ndio inakwenda Dar-es-salaam. Ahsante sana.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikamuuliza Mhe. Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza ninamshuru Mhe. Waziri alivyokuwa akijibu swali lake la msingi, kwanza alianza kutaja vifungu vya Katiba ya Zanzibar, sasa nilikuwa naomba hii Katiba ya Zanzibar kwa kweli kama tunavyoitaja, basi tujitahidi kuisimamia na kuitekeleza kama ilivyo, isiwe tunataja vifungu kwa kuonesha tu kwamba Katiba ya Zanzibar inasema hivi, naomba tuitekeleze kwa vitendo.

Mhe. Mwenyekiti, sasa swali langu liko hapa, tunamshukuru sana muekezaji wetu huyu Ndugu Bakhresa kwa uekezaji anaoufanya, lakini sasa swali langu zaidi liko hapa. Uekezaji anaoufanya Ndugu Said Salim Bakhresa ukiacha uekezaji wa kuleta meli za kusafiri na mambo mengine, lakini ameingia uekezaji wa kuweka miundombinu ya ujenzi ndani ya bandari yetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa, je, Shirika la Bandari lenyewe au serikali wanayo *master plan* ya ujenzi wa bandari ya Zanzibar? Na kama *master plan* hiyo wanayo, je, ndio hiyo ambayo huyu Ndugu Salim Bakhresa anaifata? Na kama hakuna *master plan* Zanzibar kwa kuwa tunategemea baada ya Katiba mpya kupita tunategemea Zanzibar tutafunguka katika uchumi mkubwa sana wa gesi na mafuta. Kwa hivyo, Zanzibar tunategemea itakuja taka kuweka uekezaji mkubwa sana kwenye bandari yake hii ya Zanzibar.

Je, baada ya hizi harakati za ujenzi wa ndugu Bakhresa na hiyo *master plan* ya Zanzibar katika kuimarisha bandari ikija ikiwa tayari, je, itaoana na huu ujenzi ambao anaoufanya yeye sasa hivi?

(b) Je, hizi gharama anazofanya ndugu Bakhresa sasa hivi kuna makubaliano gani na serikali katika suala zima aidha anaisaidia tu serikali au kuna makubaliano baadae kurejesha hizo gharama zake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, maswali yako ni mangapi, mawili au ni matatu?

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, swali langu moja lilikuwa kumtaka tu Mhe. Waziri anapotaja vifungu vya Katiba, basi tuhakikishe tunavitekeleza, huo ulikuwa ni ushauri. Halafu kuna maswali yangu mawili ya nyongeza kwamba kuna *master plan* kwa yale ambayo anayoyafanya au anafanya kwa anavyoona yeye na kama hakuna *master plan* kwa kuwa tutakuwa na uekezaji mkubwa Zanzibar baada ya hii rasilimali kuambiwa, sasa shughulikieni nyinyi wenyewe. Bandari ya Zanzibar tunategemea itakuwa na *master plan* yake ya kuimarisha bandari zake, je, haitokuja kuathiri na huu ujenzi unaofanywa sasa hivi na Ndugu Salim Said Bakhresa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri jibu maswali mawili kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe.Mwenyekiti, nakushukuru, naomba nimjibu Mwakilishi wa Jimbo la Kwamtipura kama ifuatavyo:-

Mhe.Mwenyekiti, kwanza napenda nimueleze kwamba tukizungumza bandari hadi tuitaje jina ili iweze kufahamika. Bandari ya Malindi ni bandari ambayo ndiyo tunayotumia sasa hivi na ina *master plan* kwa sababu tayari serikali imeshaamua kujenga bandari nyengine mpya Kwampigaduri na hiyo iko mbioni na maelezo yake yatakuja kutolewa wakati tutakapowasilisha bajeti yetu. Kwa hivyo, bandari ile inaelekea kuwa ni ya abiria zaidi kuliko ya mizigo katika *master plan* inayokuja, hii ya Malindi.

Mhe.Mwenyekiti, kwa hivyo, *master plan* ipo na anachokifanya muwekezaji anapata maelekezo kamili kutosha Shirika la Bandari, hapa unaruhusiwa kufanya hivi na kufanya hivi na kufanya vile. Kwa hivyo, hata hiyo ofisi anavyoitaka, basi ameshapata maelekezo rasmi ni nji gani ataweza kutumia jengo lake kwa ajili ya ofisi na jengo litakalojengwa kwa niaba yake litatumika kwa kiasi kitu gani.

Mhe.Mwenyekiti, la pili, ni kwamba uwekezaji wote unaowekwa hapo, bado milki ni ya Shirika la Bandari na Shirika la Bandari ndiyo lenye milki ya sehemu yote inayoekezwa. Kwa hivyo, yapo mambo mengine anapewa mwenyewe kwa *grant* yake na yako mambo ambayo yanafidiwa wakati utakapofika, kwa mfano hii sehemu ya pili ya ujenzi atakayoifanya inabidi alipiwe kutokana na kodi atakayolikodi hilo jengo atakalolitumia. Kwa hivyo, ziko aina mbili, iko ile ambayo alijitolea yeye mwenyewe na iko ambayo anafidiwa, lakini *master plan* ya bandari, sasa hivi ipo kwa sababu inaelekea katika bandari ya abiria zaidi kuliko ya mizigo wakati tunajitayarisha na ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri. Ahsante sana.

Nam. 53

Hatua za Kutunzwa Wasanii Wakongwe

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Mhe.Mwenyekiti, kazi ya sanaa ya aina yoyote, kazi kubwa ni kuelimisha, kuburudisha pamoja na kukonga nyoyo aidha za wale wanaoona, wanaosikia au wanaoshiriki moja kwa moja katika mtiririko wa utoaji wa sanaa hiyo.

Kwa kuwa sanaa ni sawa na kioo ambacho jamii hujitazama na kurekebisha na kwa kuwa mazingira ya wasanii wetu, pamoja na hatma zao zimekuwa ngumu pale wanapofika katika umri wa uzee na hatimae kumalizia vibaya sana.

Je, serikali imechukua hatua gani katika kuona wasanii walioifanyia kazi kubwa nchi hii hawaaziriki pale wanapomalizikiwa na nguvu.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Jimbo la Wawi swali lake Nam. 53 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, naomba nikubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kazi ya sanaa ya aina yoyote ni kuelimisha, kuburudisha pamoja na kukonga nyoyo za wale wanaona, kusikia au wanaoshiriki katika uwasilishaji wa sanaa hiyo. Nakubali pia kwamba sanaa ni sawa na kioo ambacho jamii hujitazama na kurekebisha jamii husika.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba wasanii wetu wanapoishiwa na nguvu kwa kuwa wazee wanakuwa hawako katika hali nzuri kiuchumi, lakini wasanii kama wafanyakazi katika jamii yetu, hali hiyo haiwapati peke yao hata wakulima, wavuvi na wafugaji nao wanapokuwa wazee hali zao kiuchumi huwa siyo nzuri. Kwa upande wa wasanii serikali inajitahidi kuwaelimisha kupitia Baraza la Sanaa kwamba wajisajili kwenye Hakimiliki ili haki zao ziweze kulindwa na ziwanufaishe katika kujikwamua na umasikini na hali ngumu na hasa wanapokuwa katika umri wa uzee.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa yeye mwenyewe amekiri kwamba sanaa ni kioo ambacho mtu

hukitizama na baadae hujirekebisha, kwa kuwa baadhi ya wasanii katika kuwasilisha sanaa zao mara nyingi huenda kinyume na mila na silka za Kizanzibari kwa kuweza kuonesha sanaa zao au kuwasilisha sanaa zao. Aidha, wakiwa nusu uchi au katika mazingira mabaya sana.

a) Je, kama sanaa ni kioo hatuoni wasanii hawa badala ya kuirekebisha jamii katika maadili mazuri kuingiza katika maadili ambayo siyo, je, serikali imechukua hatua gani kwa wale wasanii wanaokaa katika medani ya majukwaa na kuanza kuneng'ua pamoja na kucheza huku wakiwa uchi au nusu uchi.

b) Kwa kuwa hii hatimiliki imekuja juzi wanatakiwa sasa wajiingize katika mambo ya usajili hatimiliki ili haki zao zitunzwe pale ambapo wamestaafu na kuwa hawawezi kufanya tena hizi kazi, lakini kwa kuwa kuna wasanii ambao sasa hivi takribani wametuburidisha sana katika miaka ya nyuma, kwa mfano wasanii kama vile Halikuniki ametuburudisha sana siku za nyuma katika sanaa ya maonesho...

Mhe. Mwenyekiti: Naomba twende kwenye swali moja kwa moja.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa sasa hayumo tena katika sanaa na ametuburidisha sana kina Marehemu Dkt. Ayoub hapa na wengine na kadhalika. Je, serikali kwa sababu hawa wameshastaafu hata kina Bi Tele, tayari wameshastaafu, ni vipi haki zao zitalindwa hawa?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na wasanii ambao wanaonesha sanaa zao wakikiuka maadili ya Kizanzibari, wizara inajitahidi kupitia Bodi ya Sensa kuona kwamba sanaa zote zinazochenzwa au kuoneshwa ni zile ambazo zinafuata maadili nchini.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, naomba tumsikilize Waziri wakati anajibu ili yule mwenye kuuliza swali aweze kufahamu majibu ya swali lake. Ahsante Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, jitihada ambayo tunaifanya ni kuhakikisha kwamba Bodi ya Sensa inajitahidi kuhakikisha kwamba inazikagua sanaa zote kabla ya kuoneshwa ili kuepuka wasanii kwenda kuteleza katika kuteleza wakati wa kuonesha sanaa zao ili zisiharibu maadili ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu wasanii wazee na wao bado wanao nafasi kwamba sanaa zao ambazo walicheza zamani, ziweze pia kufanyiwa usajili katika Hakimiliki, na kwa sababu bado kuna watu ambao wanapenda michezo yao ya zamani, basi wakati wowote itakapokuwa inachezwa watapata haki yao ambayo sanaa zao zilikuwa zimeshughulikiwa na ndiyo utaratibu pekee ambao unaweza kutumika kupata chochote ambacho kitawafanya angalau wajisaidie katika maisha yao.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kwa sababu Waziri wa Michezo. Hivyo, nichukue fursa hii kuipongeza timu ya Shaba ya kisiwani Kojani ambayo ni timu ya kijijini, lakini imefanya kazi kubwa ya kupanda daraja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tumezungumzia watu wa sanaa, lakini Mhe. Waziri naye nimpongeze sana katika kushirikiana na wananchi katika mambo hayo ya utamaduni na michezo pamoja na sanaa hizi tunazozitaja, yeye ni shahidi tarehe 23/05/2014 kulikuwa na tamasha kubwa sana la kufanya sherehe ya timu ya Shaba, na aliona vikundi mbali mbali vya sanaa hizo, yeye mwenyewe alifurahi sana.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo, nataka nimuulize Mhe. Waziri katika kuendelezwa utamaduni wetu huu na kuzienzi sanaa hizi na vikundi hivi kama ulivyoshuhudia; msewe, kibati, mambo ya ugole na mambo ya karati utavisaidia vipi ili kuweza kuviwezesha vikundi hivi na utamaduni wetu ukue zaidi na kuendeleza kuitangaza nchi yetu ya Zanzibar?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, na mimi pia naomba nichukue nafasi hii kuipongeza timu ya Shaba ya Kojani kwa kupanda daraja na kuwa katika timu ambazo zitacheza katika *league* kuu ya Zanzibar mwaka huu. Nimuombe tu Mwakilishi na wapenzi wote wa Kojani hasa wa Kojani wenyewe kuhakikisha kwamba walii-*suport* timu yao kihali na mali ili iweze kufikia lengo ambalo wamekusidia.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tuna vikundi vingi vya sanaa nchini na moja katika azma ya Serikali ya kuiunda Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kuja na dhana ya utalii kwa wote ni kuona kwamba tunasisitiza utalii wa utamaduni ambapo vikundi hivi vya sanaa vitapata nafasi kushiriki katika shughuli za utalii na hivyo kupata kipato kikubwa katika shughuli zao za kiutalii na kujiongezea pato katika maisha yao.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mwenyekiti, ahsante na mimi kunipa nafasi hii kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijauliza swali langu na mimi nichukue fursa hii kuipongeza klabu ya Shaba kwa kuweza kupanda daraja na kucheza *premier league* ya Zanzibar. Aidha, niipongeze timu kongwe ya Zanzibar Klabu ya Ujamaa ya Jimbo la Rahaleo kwa kuweza kuwa bingwa kwa Wilaya ya Mjini kwa mwaka huu 2014/2015.

Mhe. Mwenyekiti, mchezo wa sanaa umekuwa ikiitangaza sana Zanzibar katika nchi mbali mbali za nje, hususan sanaa ya taarab zikiwemo nyimbo za Bi Kidude, lakini hivi sasa kumeibuka na kuendeleza sanaa ya vikundi vya tamthilia, kama vile kikundi cha Bi Tele na vikundi vyengine mbali mbali na hivi sasa kuna mchezo wa tamthilia unaoitwa Taharuki ambao umekuwa kivutio kikubwa cha wapenzi wa sanaa ya tamthilia hapa Zanzibar.

Je, wizara ina mpango gani wa kuwasaidia vikundi hivi vya sanaa kujiendeleza na kujitangaza zaidi Zanzibar ili kuiga mfano wa vikundi vya tamthilia kama Nigeria na Ghana.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, pia, naomba niipongeze timu yake Mhe. Mwakilishi ya Ujamaa kwa kuwa katika timu ambayo itacheza *league* kuu ya Zanzibar na nadhani kwamba mchango wa Mhe. Nassor Jazira katika hili umekuwa mkubwa hadi Jamaa ikafika hapo ilipo.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya tamthilia ni kweli kwamba ina mchango mkubwa katika utamaduni wa nchi yetu, lakini pia, katika uchumi wananchi wetu katika hali hiyo ndipo Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alipoahidi kwamba atajenga jengo maalum kwa ajili ya wasanii mbali mbali hasa michezo ya kuigiza na katika kufanya hilo, ndiyo maana wizara ikalifanyia marekebisho makubwa jengo liliopo Rahaleo kwa ajili ya kazi hiyo na tunategemea katika bajeti hii tutamalizia shughuli ya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kurikodia ili vijana wetu wawe na pahali pazuri na pa kisasa na jengo maalum na kumbi mbali mbali ambazo zitawasaidia katika kurikodi michezo yao na kuwafikia wananchi wetu.

Nam. 78

Sheria ya Alama za Biashara Kuruhusu Mawakala Kutoka Bara

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:-

Sheria ya alama za biashara *'Trade mark*' ya Zanzibar inaruhusu mawakala kutoka Tanzania Bara kufanya kazi za usajili hapa Zanzibar wakati Afisi zao zipo Bara. Hali hii inapelekea kupotea kwa ajira pamoja na kodi ya serikali.

(a) Je, kwa nini sheria hii haifanyiwi marekebisho.

(b) Kuendelea kuruhusu mawakala kutoka Tanzania Bara kusajili hapa Zanzibar, si kupoteza mapato ya serikali.

(c) Kuna faida yoyote inayopatikana kwa mawakala hao kutoka Bara kufanya usajili Zanzibar.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria) – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 78 lenye kifungu (a), (b) na (c), lakini kwanza naomba kutoa maelezo kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Usajili wa Alama za Biashara (*Trade marks*) Zanzibar unasimamiwa na Sheria ya Kulinda Haki za Tasnia ya Mali za Ubunifu (*The Zanzibar Industrial Property Act*) Nam. 4 ya mwaka 2008. Pamoja na kusimamia usajili wa alama za biashara, sheria hii vile vile, inasimamia usajili wa Hataza (*Patents*), Tasnia za Maumbo (*Industrial Designs*), Alama za huduma (*Service Marks*) na Viashiria vya eneo (*Geographical Indications*). Sheria hii pia, imezungumzia namna ya wakala (*Agents*) wanavyotakiwa kufanya kazi zao za usajili hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba, sheria inayosimamia Usajili wa Alama za Biashara hapa Zanzibar inaruhusu mawakala kutoka Tanzania Bara kufanya kazi za usajili hapa Zanzibar wakati Ofisi zao zipo Bara. Jambo la msingi ni kuwa Mawakala hao wanaotokea Tanzania Bara wawe wamethibitishwa kufanya kazi Zanzibar na kwa kuwa mawakala wanaofanya kazi hizi za usajili wa alama za biashara ni wanasheria. Hivyo, kupata ridhaa ya Mahakama kuthibitishwa kufanya kazi zao za kisheria hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 114 cha Sheria ya Kulinda Haki za Tasnia ya Mali za Ubunifu Zanzibar, iwapo makaazi ya kawaida ya muombaji au Makao Makuu yake ya Biashara yako nje ya Zanzibar, muombaji atawakilishwa na Mwanasheria anayefanya kazi hiyo anaeishi Zanzibar au aliyethibitishwa kufanya kazi hizo Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, kwa mujibu wa Sheria ya "*Legal Practitioners*" sura ya 28, kifungu cha 3 na 4 cha Kanuni ya Sheria, hiyo inatoa fursa kwa Mawakili kutoka nje ya Zanzibar kufanya shughuli za uwakili nchini kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu ya Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo, sasa namjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, sheria inayolinda Haki za Tasnia ya Mali za Ubunifu iliyopo hivi sasa ni ya karibuni na inakidhi haja kwa kiasi kikubwa na inaenda sambamba na sheria mbali mbali za Kimataifa zinazolinda haki za Tasnia za Mali za Ubunifu. Kuhusu wakala kutoka Tanzania Bara kufanya kazi zao Zanzibar, fursa au haki hiyo wanayo kutokana na sheria za nchi. Hata na sisi kwa mujibu wa sheria yao kama hii tunaweza kufanya kazi Bara kama tutafuata utaratibu uliowekwa. Jambo la msingi ni kufuata taratibu zilizowekwa na nchi kwa mujibu wa sheria. Hivyo basi, kwa hivi sasa hakuna umuhimu wa kuifanyia marekebisho Sheria hiyo, iwapo patatokea umuhimu wa kuifanyia marekebisho sheria hiyo, wizara haitosita kufanya hivyo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sheria imeelekeza kuwa iwapo makaazi ya muombaji au Makao Makuu yake ya biashara yako nje ya Zanzibar, muombaji huyo anatakiwa awakilishwe na Mwanasheria anayefanya kazi hiyo Zanzibar au kutoka nje ya Zanzibar ambaye amethibitishwa na Mahakama Kuu kufanya kazi hizo hapa nchini. Hivyo, Mawakala kutoka Tanzania Bara wanafuata utaratibu sawa na wale Mawakala kutoka Zanzibar. Kuendelea kwao kuleta kazi zao hizo kwa usajili wa alama za biashara hapa Zanzibar, hakupotezi mapato ya serikali kwani kazi za wateja wao wanazozisajili zinalipiwa kikamilifu kwa mujibu wa sheria za nchi. Sambamba na hilo, Mawakala hao huwa wanalipia ada ya kufanya kazi zao za Kisheria kupitia Mahakama Kuu ya Zanzibar.

(c) Mhe. Mwenyekiti, zipo faida zinazopatikana kwa mawakala hao kutoka Bara kufanya Usajili wa Alama za Biashara hapa Zanzibar. Kwa kiwango kikubwa cha kazi za usajili wa Alama za Biashara zinazosajiliwa Zanzibar huwa zinatoka nje ya nchi kupitia Mawakala walioko Tanzania Bara. Hivyo, serikali inafaidika kimapato kwa kiasi kikubwa kutokana na kusajili kazi zao hizo kwa hapa Zanzibar.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Kaimu Waziri, tabia za kazi za wasanii kugemwa na kunufaisha watu bila ya kuwepo makubaliano ya biashara inaendela kufanyika kwa vituo vya redio, televisheni na uuzaji wa *CD* bila ya kuwanufaisha wenyewe. Je, kuna kesi ngapi mpaka sasa hivi wizara yake imeikwisha kuzishughulikia?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba yako malalamiko kuwa matatizo kama aliyotaja Mhe. Mwakilishi yanafanyika nchini na tumewakilisha hayo ni masuala ya uhalifu ambayo yakiripotiwa kwetu na kupitia Afisi ya Muendesha Mashtaka,

basi taratibu za kisheria zinachukuliwa. Kwa hiyo, siwezi kumwambia hivi sasa kwamba ni kesi ngapi tayari zimeshatolewa hukumu, naomba anipe nafasi jibu hilo nitamjibu kwa maandishi.

Mhe. Farida Amour Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri na marefu sana ya Mhe. Waziri, naomba nimuulize kwamba, kwa mwaka jana na mwaka huu wizara yake imepata mapato yake kiasi gani na inasajili alama ngapi za biashara.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014 alama zilizosajiliwa ni 619 na hadi mwaka huu alama zilizosajiliwa ni 430. Mapato yaliyopatikana naomba nilichukue hili kwa sababu nahitaji jibu sahihi sana ambalo fedha fedheha, naomba nimjibu kwa maandishi.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana na mimi naomba nimuulize swali dogo tu Mhe. Waziri kama jibu lake la mwisho alivyojibu. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kutokujua hesabu ya mapato yanayokusanywa na wizara yake, ni kuonesha udhaifu ambao watendaji wake wa kazi kuwa hizo pesa zinaliwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo (Kny: Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria): Mhe. Mwenyekiti, ninachozungumza ni kwamba jumla ya alama za biashara zilizosajiliwa nimezitaja, kwa mwaka jana na mwaka huu kabla haujamaliza. Sasa ni vizuri nitoe jibu la uhakika la fedha kiasi gani zimekusanywa, huo sio udhaifu. Nataka kuhakikisha kwamba Baraza lako tukufu linapata majibu ambayo yanatakiwa kwa mujibu wa Kanuni na taratibu zetu, hakuna fedha iliyoliwa hata moja kwa sababu fedha zote zinazokusanywa zinaandikiwa risiti na zipo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyojibu tutamjibu kwa taratibu zetu za Baraza ili tuhakikishe kwamba tunatoa jibu ambalo ni sahihi.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, kabla swali langu namba 10 halijajibiwa naomba nichukue fursa hii kumpongeza *Left Name Canal*, JK Mbwelo wa Kambi ya *Alhamisi Camp* pamoja na wapiganaji wote wa *TPDF* waliopo katika kambi ile kwa kuweza kutoa mashirikiano mazuri kwa wapigakura wa Jimbo la Wawi pamoja na wananchi wa Wilaya nzima ya Chake Chake, kwa kuweza kuwapatia matibabu katika Hospitali ya Jeshi pamoja na elimu katika skuli yao ya Jeshi. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya mama yake Cholo na wapiga kura wote wa Jimbo la Wawi tunachukua fursa hii kuwapongeza wapiganaji wetu.

Baada ya maelezo hayo, naomba swali langu namba 10 lipate majibu hivi sasa.

Nam. 10

Msaada wa Serikali kwa Hospitali ya Jeshi – Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kambi ya Jeshi la Wananchi *TPDF (14KJ*) iliyopo Vitongoji wameanzisha skuli ya msingi pamoja na Hospitali, sio tu kwa ajili ya kuwatibu wapiganaji wetu, lakini asilimia 90% ya wanafunzi wagonjwa wanaosoma na kutibiwa katika taasisi hizo ni raia ambao ndio walipa kodi wakuu wa nchi hii. Kwa kuwa kuna kila dalili zinazoonesha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijatoa uungaji mkono wa juhudi za wapiganaji wetu hao.

Je, ni lini serikali yetu itawaunga mkono wapiganaji wetu hao angalau kwa kuwapatia banda moja la shule pamoja na kuingiza Hospitali yao katika mgao wa madawa kwa Hospitali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 10 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, napenda nikubaliane na Mhe. Mwakilishi kwamba, Hospitali ya Jeshi iliyopo Vitongoji inahudumia asilimia kubwa ya raia wanaoizunguka kambi hiyo na ndio walipa kodi wakuu wa nchi hii, lakini

ninachokataa, siamini na si kweli hata kidogo kwamba kuna angalau chembe za dalili zinazoonesha kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haiungi mkono juhudi za wapiganaji wetu hao.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya inatoa mashirikiano makubwa kwa Hospitali zote za wapiganaji ikiwemo hiyo ya Vitongoji na Uongozi wa Afya wa Wilaya huwa inazijumuisha katika mipango yake ya Wilaya.

Mhe. Mwenyekiti, sababu ya msingi ni kwamba wapiganaji nao ni wananchi wa Tanzania kama raia wengine na hakuna sababu ya kutokuwaunga mkono watoto wetu tuliowazaa, raia wa Taifa letu wenyewe wanaotulinda na maadui, kwa sababu tu eti wao ni wapiganaji.

Mhe. Mwenyekiti, hii haingii akilini.

Mhe. Mwenyekiti, napenda Mhe. Mwakilishi afahamu kwamba wafadhili wakubwa wanaoshirikiana na Wizara ya Afya ya Zanzibar katika masuala ya dawa ni Danida, ambao wanaleta dawa kwa mujibu wa mapendekezo na mahitaji ya vituo vya afya kwa Hospitali zilizo chini ya wizara hiyo tu (Wizara ya Afya).

Mhe. Mwenyekiti, Hospitali ya Vitongoji ni Hospitali ambayo iko chini ya Wizara ya Ulinzi ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, mgao wa *DANIDA* haihusiki nayo. Ukiacha dawa zinazotolewa na *DANIDA*, Hospitali ya Vitongoji haijanyimwa dawa zile ambazo zinanunuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kutoka kwa wafadhili wengine wasiokuwa *DANIDA*.

Mhe. Mwenyekiti, si dawa tu ambazo Wizara ya Afya inawapa Hospitali ya Vitongoji, bali wizara inawapa mahitaji yao kama kituo chengine cha afya cha serikali ambacho kinatoa huduma kwa wananchi bila ya kujali ni kituo cha aina gani ilimradi tu kinahudumia Watanzania. Mfano hai Wizara ya Afya imeipa Hospitali ya Vitongoji katika mgao wake wa vifaa seti ya compyuta, mashine za kupimia *pressure*, friji la kuhifadhia dawa za chanjo, dawa aina zote za chanjo, kibeba dawa wanapokwenda kutoa huduma za chanjo nje ya kituo, *(Outreach Services*), mezani za kupimia uzito watoto na watu wazima, dawa na vifaa vya huduma za uzazi wa mpango. Pia, wizara inatoa madaftari ya kutunzia kumbukumbu, fomu tofauti za kukusanyia taarifa na vifaa vya usafi kwa kila robo mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe, chini ya Uongozi wa Afya wa Wilaya, Hospitali ya Vitongoji inashirikishwa katika mambo yote ya vituo vya afya. Wafanyakazi wake wanashiriki katika mikutano ya kila robo mwaka ili kutathmini mafanikio na mapungufu ya Hospitali hiyo, kushiriki katika mafunzo mbali mbali yanayofanywa na Wizara ya Afya na pia uongozi huo unawafuatilia na kuwasaidia katika utendaji wao wa kazi bila ya kubaguliwa.

Mhe. Mwenyekiti, hiyo kama haitoshi, asilimia zaidi 90 ya wafanyakazi wa Hospitali ya Vitongoji ni waajiriwa wa Wizara ya Afya. Jumla ya wafanyakazi 7 wa kada mbali mbali wamepangiwa kufanya kazi katika Hospitali hiyo. Kuna nesi, fundi sanifu maabara, wakunga wasaidizi (*PHNB*), mkunga anaehudumia kina mama na watoto (*MCH AID*) na maodali.

Mhe. Mwenyekiti, Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa akiwemo na yeye alieuliza swali hili ifanye nini tena ili iweze kumshawishi na kumbadilisha fikra Mhe. Mwakilishi huyu ili aone kwamba serikali yetu hii inawaunga mkono wapiganaji wetu hawa. *(Makofi)*

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri sana ya mdogo wangu Naibu Waziri wa Afya, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwanza napenda tu nitoe taarifa kwamba mimi nilikuwa nazungumzia Hospitali ya 14KJ ya Kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyopo 14KJ *Alhamisi Camp*, wala sikuwa nimeuliza swali hili la msingi kwa Hospitali ya Vitongoji, *Cottage* ni Hospitali ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania iliyopo Vitongoji katika Jimbo la Wawi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hiyo, jibu nusu na robo kajibu Hospitali ya Vitongoji, *Cottage Hospital* hajajibu kuhusu Hospitali ya Jeshi. Sasa pamoja na majibu robo aliyonipa Mhe. Naibu Waziri ya hii Hospitali ya 14KJ, naomba niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa kuna tatizo la muda mrefu katika Hospitali ya Jeshi ya 14KJ na sio *Vitongoji Cottage Hospital*, kuna tatizo la muda mrefu la kwamba wao wanapima Virusi vya UKIMWI, lakini hadi leo hii hawajaruhusiwa kutoa zile dawa za *ARV* kwa wale waathirika wa mambo haya ya UKIMWI.

Mhe. Mwenyekiti, siku za nyuma nilijibiwa kwamba hakuna mtaalamu pale, *Doctor in medicine*. Nataka niulizie tu kwamba kwa sababu wana utaratibu Wizara ya Afya kuwasaidia wauguzi pale Hospitali na kuna wauguzi ambao ni raia. Je, hawawezi kufanya busara kupitia wizara yake ikiwa hawa wapiganaji wetu hawajapata *Doctor in medicine* na kuweza kuruhusiwa kutoa hizo *ARV* au hawawezi kufanya busara zao tukawapelekea daktari mmoja bingwa japo *part time* pale hospitalini pao na wakaweza kutoa hizo *ARV* na wao. *That is (a).*

(b) Hili suala la skuli nadhani nililipeleka kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa sababu nimezungumzia skuli na Hospitali, lakini la skuli halikupata jibu. Je, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na yeye isingekuwa vyema akajibu kuhusu hii skuli kwamba na wao serikali, ni lini watawapatia angalau banda moja la skuli hapo kwa sababu Mheshimiwa yupo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana Mhe. Mwakilishi hakunisikiliza, alikaa kwa kuwa alikuwa keshakuwa na masuala yake ndani ya kichwa hasikilizi ninachokisoma hapa, nitakapomaliza nitampa hizi karatasi asome nilichokiandika. Sikuzungumza *Vitongoji Cottage Hospital* ,nimezungumza Hospitali ya Jeshi.

Mhe. Mwenyekiti, swali (b), anazungumzia suala la dawa za UKIMWI katika Hospitali hiyo ya Jeshi. Taratibu za dawa za UKIMWI zinapelekwa katika madaraja na Hospitali zenye viwango na sifa kama zilivyowekwa na Wizara ya Afya. *Vitongoji Hospital* haijafikia sifa hiyo, watu walioko pale wanatakiwa wende *Chake Chake Hospital* na wengine wote wanakwenda Hospitali ya Chake Chake. Kwa hiyo, si suala la busara wala si suala la kupeleka daktari wa *part time*, isipokuwa viwango vya Hospitali ile, hao wafanyakazi wa dawa hawana, watakuwa na uwezo wa kutoa *ARV*?

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kidogo nisikitike sana. Nasikitika kwa majibu ya Naibu Waziri kwa sababu mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii kama Makamu Mwenyekiti wa Kamati ni miaka miwili nyuma.Suala hili la Hospitali ya Jeshi kutoa dawa za UKIMWI lilizungumzwa miaka miwili iliyopita na wizara hii hii, Naibu Waziri huyu huyu wakaijibu Kamati kwamba wanalishughulikia kwa karibu na Majeshi wakasema kwamba wako tayari kutoa mtu aajiriwe wao watamlipa mshahara kwa *rate* ya Jeshi.

Mhe. Mwenyekiti, leo Naibu Waziri akisema kwamba hawana uwezo wa kupima UKIMWI waje wapewe dawa, kwangu mimi hii ni kejeli na kama haya ndio majibu ya Mhe. Naibu Waziri, naomba anijibu swali langu kwamba, je, haya ndio majibu anayowajibu wananchi na amesahau majibu yake hata ya miaka minne nyuma, kweli anafaa kuwa waziri?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, kama hivyo ndivyo, ilikuwa Jeshi waje watueleze kwamba mtu tumeshamuajiri na vigezo tunavyo, hawajaja kwetu.

Utaratibu

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, Majeshi hawakuzungumza kwa njia ya simu, Majeshi walizungumza kupitia Kamati na Wizara ya Afya ilikuwepo, sasa aambiwe wapi.

Mhe. Mwenyekiti: Samahani Mhe. Mjumbe toa kifungu cha Kanuni ambacho unataka kukirejea.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi nimesema nililokuwa nimehoji mwanzo.

Mhe. Mwenyekiti: Sijakufahamu, tuendelee.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mwakilishi Hospitali iko jimboni kwake na lisemwalo lipo. Je, Naibu Waziri atakuwa tayari kufuatana na Mwakilishi kwenda kupata uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nirudie Mwenyekiti. Kwa kuwa Mwakilishi ni kiongozi wa wananchi na Hospitali iko jimboni mwake na lisemwalo lipo. Je, Mhe. Naibu Waziri yuko tayari kufuatana na Mwakilishi kwenda kujua kuwa serikali inasaidia na wizara haisaidii. Naomba majibu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Kwa mujibu wa taratibu zetu maswali ya nyongeza yanakuwa ni matatu. Sawa sawa nimekuruhusu Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima na taadhima ni kwamba kiti chako ndicho kinachoongoza Baraza hili, kutokana na muongozo wako ndio uliomfanya Mhe. Naibu Waziri wa Afya aondoke pale mbele kwa sababu ulisema tuendelee, msingi wa tuendelee maana yake kwa sasa umemaliza sehemu hiyo ma maswali.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante nimekuelewa Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa hiyo swali hili tutaliacha kwa sababu tulikwishakutoa maelekezo kwa Mhe. Naibu Waziri kwamba tuendelee. Katibu.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 - Wizara ya Nchi (OR) Ikulu na Utawala Bora

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwa siku ya leo tuna wageni ambao wamefika hapa kwetu na wageni wetu wa siku ya leo ni wageni ambao wameletwa na Mhe. Nassor Salim Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Rahaleo, ambao ni viongozi wanane wa *Ujamaa Sports Club* ya Jimbo la Rahaleo.

Wageni hao majina yao ni kama ifuatavyo:-

1. Ndugu Ameir Makungu Makame
2. Ndugu Ali Vuai
3. Ndugu Juma Khalfan Said
4. Ndugu Othman Sultan
5. Ndugu Omar Abdalla Said
6. Ndugu Abdulmalik Said
7. Ndugu Yussuf Mwinyi Dadi
8. Ndugu Khamis Omar

Na kwa taarifa tu tumeambiwa kwamba hawa ndio mabingwa wa Wilaya ya Mjini. Ahsante, Mhe. Waziri tuendelee.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuwasilisha michango mbali mbali waliyotoa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu katika kuchangia hotuba ya Wizara ya Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kwanza kukushukuru wewe binafsi kwa kutuongoza vyema, alianza Mhe. Naibu Spika, ukafuatia wewe na pia, naomba nichukue fursa hii kuwashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia na naamini hao wengine walitaka, lakini kwa sababu mbali mbali ukiwemo na utaratibu tuliojiwekea, basi hawakuwahi kuchangia, lakini kuna wengine vile vile walichangia kimaandishi nao tunawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla tulipata michango 22, Waheshimiwa 19 walipata fursa ya kuchangia ukumbini na Waheshimiwa 3 walipata fursa kuchangia kimaandishi, lakini kabla sijaendelea naomba kwa dhati kabisa niwapongeze Waheshimiwa wote hasa wale waliompongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa juhudi kubwa anazozichukua na juhudi hizo yeye ni kiongozi, lakini tunashirikiana pamoja sote Mawaziri na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi kwa ujumla kuleta maendeleo katika nchi yetu. Chini ya uongozi wake, nchi yetu imepiga hatua kubwa kimaendeleo na kuimarisha uchumi na pia, kuimarisha miundombinu ya barabara zilizosalia kujengwa upya hususan katika kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa dhati kabisa pia kumpongeza Kaimu Mwenyekiti Mhe. Shadya Mohammed Suleiman aliyewasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa niaba ya Mwenyekiti wake Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile, naomba nimshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Hesabu za Serikali (*PAC*). Kwa kweli miongozo wanayotupa hasa kupitia Ofisi ya *CAG* na kufanya kazi Kamati yake kwa pamoja na Ofisi yetu ni faraja sana na mafanikio makubwa kwa kweli tumeyapata kutokana na miongozo na maoni yao wanayotupa kama nilivyosema pamoja na Kamati hii ya Kusimamia Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, naahidi kwamba maoni waliyotupa na ushauri wao tutaufanyia kazi na tutawajulisha maendeleo yake kadiri tutakavyokuwa tunakutana kwenye Kamati.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kama nilivyosema kuwashukuru tena Wajumbe wote wa Kamati hizo mbili ambao wameshirikiana vizuri nasi tangu wakati wa matayarisho wa bajeti na mpaka kuwasilisha kwake na hatimaye tuweze kuipitisha hii leo. Naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba tunaithamini sana michango na ushauri wao tumepokea kwa dhati kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia niseme kwa maelezo ya jumla kwamba Wajumbe walizungumzia kuhusu matumizi ya kawaida katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2014/15 na walionesha *concern* kwa nini kuna matumizi madogo. Nataka kusema tu kwamba kwa ujumla bajeti yetu ya fungu 10 imepungua kwa asilimia 17 na hii kutokana na keki yenyewe lazima tukubali mapato yetu bado hayakidhi matumizi yetu. *Alhamdulillah* maendeleo yamekuwa mengi watu wameshajihika, lakini bado nazo juhudi zetu za kukuza mapato lazima tuzifanye bora zaidi ili twende sambamba pamoja na shughuli za matumizi yetu. Kwa hiyo, hili pungufu lilitokezea kwa asilimia 17, naamini hata bajeti nyengine zijazo mtaona nazo kuna mapungufu kwa njia moja au nyengine, sio kama tumeonewa la hasha.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema naomba sasa niwatambue Waheshimiwa wale 19 waliochangia ukumbini na 3 waliochangia kimaandishi.

1. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
2. Mhe. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
4. Mhe. Hija Hassan Hija
5. Mhe. Fatma Mbarouk Said
6. Mhe. Mussa Ali Hassan
7. Mhe. Ali Salum Haji
8. Mhe. Abdi Mosi Kombo
9. Mhe. Panya Ali Abdalla
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma
11. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
12. Mhe. Farida Amour Mohammed
13. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
14. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad
15. Mhe. Marina Joel Thomas
16. Mhe. Mohammed Haji Khalid
17. Mhe. Machano Othman Said
18. Mhe. Salma Mussa Bilal
19. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi

Mhe. Mwenyekiti, wote tunawashukuru sana kwa michango yenu kama nilivyosema ilikuwa mingi, lakini zaidi ilikuwa ya kuboresha kufanya utendaji wetu pale ambapo kuna mapungufu tuweze kujirekebisha na mmetoa rai twende vipi kwa siku za usoni. Kama nilivyosema yote tunayapokea haitokuwa rahisi kwa saa moja hii kujibu kila hoja. Sasa naomba sana kwamba pale ambapo hatutojibu msione kwamba tumeidharau, lakini tutaichukua na *Inshaallah* na wao wasiwe kimya tuzidi kushauriana hata nje ya Baraza.
Waheshimiwa 3 waliochangia kimaandishi ni:-

1. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
2. Mhe. Nassor Salim Ali
3. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mingi ya michango ya Waheshimiwa Wajumbe ilikuwa katika mapendekezo, maoni, ushauri na ufafanuzi na mambo yaliyoguswa sana takriban yapo kama 11. Naomba niyataje tu, halafu tena nitaanza kuchambua Mheshimiwa mmoja baada ya mwengine.

Mhe. Mwenyekiti, suala la rushwa na uhujumu wa uchumi takriban limezungumzwa na Waheshimiwa karibu wote, na hii inaonesha wazi tunavyokerwa na suala hili la rushwa na uhujumu wa uchumi. Hili ni jukumu letu sote Waheshimiwa na tuseme tuwe mstari wa mbele kabisa katika kulikabili. Tusiseme wafanyabiashara la, sote hili linatukabili tulisimamie vizuri, tuwaongoze wananchi wetu, tuwaelimishe, nitatoa maelezo zaidi kwa urefu baadae.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la pili, ni suala la Wazanzibari wanaoishi nchi za nje na ushiriki wao katika kuiletea Zanzibar maendeleo. Hili nalo Waheshimiwa takriban wengi sana wameligusia na tunashukuru kwa mitizamo mipya waliyokuja nayo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu suala la Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye kitengo hichi nalo limeguswa na hasa ushiriki wetu upande wa Zanzibar na ile Taasisi ya Kiswahili tuliyoizungumza. Nitakuja kueleza kwa urefu baadae.

Mhe. Mwenyekiti, lakini la tatu ambalo limezungumzwa kwa kirefu sana ni suala la nyumba za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Nalo hili nafikiri Waheshimiwa wengi wamelitolea maelezo na wametoa ushauri na heshima ambayo viongozi wetu wanapaswa kupewa. Naomba nikiri kwamba ni nia ya serikali yetu kuwaenzi viongozi wetu tuone kwamba wanakaa katika nyumba ambazo zinastahiki kote Unguja, Pemba, Dar-es-salaam na hata wakenda nchi za nje. Si vyema kumwona kwamba Rais wetu au Makamu wake wote wawili au hata sisi Mawaziri kwamba tunapata tabu ya mahala pa kukaa. Haipendezi kuona mtu anakaa mahala pasipostahiki. Kwa hiyo, hili nitalitolea maelezo kwa urefu.

Mhe. Mwenyekiti, halafu suala la nne ni Ofisi ya *CAG* na hasa sifa kemkem ambazo Waheshimiwa wamemtolea. Kwa kweli kwa niaba ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, naomba kupokea sifa zote na wengine walipendekeza kabisa kwamba tumpe nishani maalum ya ujasiri na ukakamavu wake. Ushauri huo tunaupokea na limeingia kwenye *record.*

Mhe. Mwenyekiti, lakini maslahi ya Ofisi yake pia Waheshimiwa wengi wamezungumza, sitaki kuwataja majina nitakuja kutaja baadae. Ninachosema ni kwamba kulikuwa mwanzo kuna matatizo kweli, lakini hivi sasa tumekaa tayari na mkakati unaendelea vizuri kabisa. Nitakuja kusema baadae kwamba sio kama hayajashughulikiwa, matatizo yao yameshashughulikiwa na mengine yamo njiani. Hivi sasa tokea wiki iliyopita mpaka wiki hii Kamati zinaendelea pamoja na Tume ya Utumishi kuona kwamba mambo yao yanaendelea vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti za ukaguzi katika Mamlaka ya Vyombo vya Baharini pamoja na uchunguzi kuhusu viinua mgongo na mishahara hewa, lini taarifa hizo zitawasilishwa katika Baraza. Hili nalo Waheshimiwa walichangia na walionesha *concern* yao, kwa nini bado kuna uzito. Nitalitolea taarifa kazi hii imeshafanywa na ripoti tayari zimeshatayarishwa. Ni suala la utaratibu tu mpaka Waheshimiwa ziwafike hizo ripoti.

Mhe. Mwenyekiti, suala la Utawala Bora, mwenyewe umeniuliza nini utawala bora na Waheshimiwa wengi sana walitaka kujua nini utawala bora. Nitakuja kuelezea kwa urefu hapo baadae, lakini ni suala ambalo Waheshimiwa wengi wametaka kujua.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu, sheria na bajeti ya Ofisi ya *GSO,* Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na wengine wengi kabisa wamezungumzia suala hili. Nalo nitakuja kulieleza kwa ufasaha kabisa. Ni muhimu sana, umuhimu wa kitengo hichi na vipi labda uguse wafanyakazi wengine wa *Private Sectors.* Nitakuja kuelezea kwa kirefu mbele.

Mhe. Mwenyekiti, la nane ni suala la ufuatiliaji, tathmini, takwimu, mipango, ukuaji wa uchumi na ongezeko la mfumko wa bei. Hili nalo Waheshimiwa wengi walitaka kujua na hasa mwenendo wetu na tofauti labda ya Idara zile mbili ulizozitaja nitakuja kutoa ufafanuzi kwa urefu kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, Mawasiliano Ikulu nalo ni suala limezungumzwa na Waheshimiwa wengi na wameshauri hata Mhe. Rais wetu anapokwenda ziara nchi za nje kuwe na mashirikiano kati ya kitengo chetu na waandishi wengine ili wakirudi wafanye *documentary* au vipindi. Ni wazo zuri tumelisikia nitakuja kuelezea vizuri baadae.

Mhe. Mwenyekiti, la kumi, ni ripoti ya haki za binadamu, hili nalo Waheshimiwa wachache walizungumza hasa Mhe. Farida Amour Mohammed alizungumza sana. Nakushukuru kwa *observation* zako na nitakuja kuzungumza kwa kifupi zile ripoti ambazo zimeshatoka. Elimu kwa wafanyakazi Mhe. Farida Amour Mohammed nae alizungumza sana suala hili, nalo nitakuja kulizungumza kwa kifupi tu.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema, haya mambo ni mengi na nitajitahidi kwa kifupi kabisa na nimeona bora tuyaandike ili tuyasome kwa mtiririko mzuri. Ufafanuzi wa vifungu sijamsahau Mhe. Wanu Hafidh Ameir na Mhe. Ali Salum Haji, nitavisoma vifungu vyao na nahisi nisije nikasahau bora nianze mwanzo, kwa sababu nikija nikisahau, hivi mabuti najua yatakuwepo. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba bora nianze hili la vifungu kuweka sawa.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Salum Haji na Mhe. Wanu Hafidh Ameir walitaka ufafanuzi katika vifungu vifuatavyo. Kwenye ukurasa wa 71, kifungu 31 (1200) matumizi ya milioni 20 ya gari. Tunasema kwamba matumizi ya ununuzi wa gari yatafanywa kwa awamu. Hizi ni fedha za malipo kwa awamu ya mwanzo kabisa. Tunajua milioni 20 hainunui gari, lakini tuna utaratibu maalum kwa sababu unajua pesa tunavyopata nazo zina kazi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini tukipata kama hizo na tumeshakubaliana na wale wanunuzi. basi tunapeleka milioni 20 tunasubiri *Inshaallah* tukipata nyengine. Haitozidi mwaka tuna utaratibu mzuri tu na tumeshanunua tumeshafanya utaratibu huo kwa muda mrefu na hii tunaepuka kununua gari *second hand,* serikali inapenda kununua gari mpya na ndio maana tumeona tufanye utaratibu huu na una watu *very effectively* hauna tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 74 kulikuwa na suala la milioni 2, umetuuliza, utafiti gani huo utafanywa kwa milioni 2. Ni kweli huu utafiti Mhe. Wanu Hafidh Ameir umeshafanywa na utafiti wenyewe ni mdogo tu kuhusu utawala bora na hivi sasa upo katika hatua za mwisho kukamilika. Kwa hiyo, tunahisi milioni 2 hizi zitakamilisha ile kazi iliyobaki. Sio kama ndio tunaanza milioni 2, ni kweli hazitoshi, ukifuata zile sheria za utafiti *is a peanut,* lakini hizo hasa madhumuni yake ni kumalizia.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu kingine kipo ukurasa wa 76 ni 220408, gharama za umeme. Ulituuliza huo umeme au mna *solar,* kwa sababu mmeweka maziro tu pale. Ukweli ni kwamba gharama hizi za umeme pamoja na kifungu cha 263178 cha UKIMWI na *HIV Aids* vimekuwa *centralized* katika Idara ya Uendeshaji. Katika Wizara tume-*centralized* pale mambo yote haya tumeona kuyafanya yatiririke kwenye Idara mbali mbali ni tabu kidogo. Kwa hiyo, tumeona tuya-*centralized,* mfano katika Idara ya Uendeshaji na Uchumi. Kwa hiyo, hilo wa umeme pamoja na kifungu 263178 vya UKIMWI jibu lake ndio hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia, Mhe. Ali Salum Haji nakumbuka alituuliza kuhusu fedha zimeongezeka katika ukurasa 86, kifungu 220501 kutoka milioni 24.8 mpaka 44.5. Jibu kwamba fedha hizo zimeongezeka kwa sababu zimetengwa fedha zitakazotumika kwa ununuzi wa vifaa vya kuandikia Ofisi ya Maadili ya Viongozi inayotarajiwa kuanzishwa baada ya kupitishwa Sheria ya Maadili. Hatutaki tena tupate tabu zile za mwanzo ambazo tulizipata tulipofungua mamlaka hii mpya ya rushwa. Nakumbuka wengi mlisema mbona tume-*take off*, lakini hakuna kazi zinazoendelea. Zipo kazi, lakini kuepuka matatizo kama haya ya vifaa, ya Ofisi, basi tumeona bora tutenge pesa hizi maalum kwa kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, halafu Mhe.Ali Salim alituuliza kwenye kifungu 220701 *page 86, six millions* zile. Hizo mbona ni *minor* au ni *major repair* au *major maintenance*. Ukweli ni kwamba fedha za kifungu hichi zimetengwa kwa matengenezo madogo madogo ya majengo ya Utawala ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Lazima tutofautisha na hapo vipo vifungu vyote viwili, kipo kifungu cha *minor civil work* na *major civil work*. Huo sio ujenzi mpya ni *maintenance* na kwa kweli vifungu kama hivyo tusipovitumia au tusipoviomba, ndio utakuta majumba yanatuangukia. Unajua Waswahili wanasema kwamba "Usipoziba ufa utajenga ukuta". Ni ule tu ukarabati mdogo mdogo, wewe unaona mdogo tu, kesho unauacha, keshokutwa unauacha, mwisho ukuta mzima unaanguka na yanatofautiana kwa mujibu wa wenyewe wizara munavyosema, zipi ziwe *minor* na zipi *major*. Hivyo, vifungu vimewekwa na Wizara ya Fedha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ni suala kifungu 281400 shilingi milioni kumi zilizoekwa kwenye ukurasa wa 87 wa buku lile. Fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kukodi Ofisi itakayotumiwa na Ofisi ya Maadili ya Viongozi inatarajiwa kuanzishwa baada ya kupitishwa kwa sheria ya maadili, sio kwamba tunalipia kodi, aah! ni kifungu tu hicho, lakini madhumuni yake ni hayo hasa. Kwa hivyo, matarajio ya Ofisi yetu hii itakapo-*take off Inshaallah* pesa hizi tusipate taabu tena kupata nyumba au pa kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha mwisho ni kifungu kipo ukurasa 88, kifungu cha 220401, *from twenty point seven to eighteen millions.* Unasema upande wa *GSO*, kifungu hichi mbona kimepungua. Kwa kweli kimepungua kama nilivyosema sababu kubwa hasa ni ufinyu wa bajeti, yaani matumizi ya mafuta. Ni ufinyu wa bajeti uliofanya *to allocate* kwengine sio kama kazi zao hazina umuhimu, kazi zao zina umuhimu, suala la usafiri tutasaidiana ndani ya wizara tuone kwamba kazi zao zinafanikiwa. Naona upande wa vifungu bora nivimalize kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niwachukue moja kwa moja kwenye michango mbali mbali ya Waheshimiwa Wajumbe. Naomba kutoa maelezo yangu kwa kuanza na ufafanuzi wa mchango aliotoa Mhe. Shadya Mohammed Suleiman kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambapo alitoa mapendekezo na ushauri na aligusia karibu Idara zote za Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, namuhakikishia Mhe. Shadya Mohammed Suleiman kwamba mapendekezo yaliyotolewa na Kamati yake tutayazingatia kwa makini na kuyafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kama nilivyosema awali namshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe - Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza hili ya *PAC* kwa ufafanuzi mkubwa aliotoa wakati akiwasilisha hotuba ya Kamati yake.

Mhe. Mwenyekiti, michango aliyotoa maelekezo na ushauri aliotoa tunamuahidi tutaufanyia kazi. Maelekezo ya kina na mapendekezo ya Kamati hii nitayatolea, sambamba na maelezo ya Waheshimiwa Wajumbe mbali mbali katika *sections* ambazo Waheshimiwa walichangia.

Mhe. Mwenyekiti, moja ambalo kati ya jambo ambalo limeleta utata wakati ninawasilisha hotuba yangu, ni tofauti ya dhana ya ujenzi na matengenezo. Waheshimiwa wengi, Mhe. Fatma Mbarouk Said mmoja wapo aliliuliza hili. Utata huu ulihusishwa na jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali liliopo Pemba, mbali

na Mhe. Omar Ali Shehe, Wajumbe wengine waliona upo utata juu ya jambo hili, ni Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mohammed Mbwana Hamada na Mhe. Fatma Mbarouk Said kama nilivyosema.

Mhe. Mwenyekiti, kimsingi sote tunazungumzia kitu kimoja na wala hakuna haja ya kujenga hofu katika jambo hili.Ukweli ni kwamba kuna ujenzi, yaani *construction*. Pia, kuna matengenezo, yaani *renovation*. *Construction* kwa Kizungu ni aina ya ujenzi unaofanywa kwa kuanzia tokea msingi wa nyumba hadi kukamilika kwa nyumba au kitu husika au kitu kama hicho. Wakati matengenezo ni aina ujenzi ambao unaendelea na kurekebisha baadhi ya sehemu za nyumba na kuacha maeneo mengine ya nyumba hiyo kama yalivyo. Ninajua tunao ma-*engineers* hawa ma-*experts* hawa akina Mhe. Nassor Ahmed Mazrui watatusaidia zaidi baadae.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba sasa kuhusiana na jengo lile la Ofisi ya Mdhibiti wa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Pemba, kwa vile jengo hilo halikubomolewa lote bali liliendelezwa na kuimarishwa ambapo marekebisho hayo yalikuwa makubwa, ndio maana baadhi ya Wajumbe wa Baraza hili walihisi kuwa kulikuwa na ujenzi kamili. Hata tukiangalia ukurasa wa 96 katika kitabu cha makadirio na matumizi ya mapato na matumizi, kifungu 220702 ambacho ndicho kilichoidhinishiwa bajeti yake mwaka jana, kinaeleza wazi kwamba ni matengenezo makubwa ya majengo. Aidha, pendekezo la Kamati ya *PAC* la kufanya ukaguzi maalum litafanyiwa kazi. Kwa hivyo, huo ndio ufafanuzi hasa.

Mhe. Mwenyekiti, ninawashukuru kwanza Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Salim, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwa michango, ushauri na maelekezo juu ya kuziendeleza nyumba za Ikulu. Hatua kwa hatua Ofisi yangu inakusudia kuendeleza ujenzi mkubwa wa majengo hayo, nyumba moja baada ya nyengine kama tulivyoanza matengenezo makubwa ya nyumba ya Mkoani na hivi sasa tunaendelea na Ikulu ya Laibon.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka ujao wa fedha 2014/2015 tutaanza matengenezo ya Ikulu ya Dodoma na kuendelea na ujenzi katika nyumba ya mapumziko ya Micheweni. Sambamba na hayo, serikali ina azma ya kuzifanyia matengenezo nyumba zote za Ikulu.

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Waheshimiwa Wajumbe hasa Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi kwamba viongozi wetu wakuu huwa wanakaa katika hoteli hasa wanapokuwa katika shughuli zetu za kikazi nje ya Unguja. Hata hivyo, mahoteli wanayokaa ninathubutu kusema kwamba yana hadhi ya kukaa viongozi wakuu. Wakuu kwenye *suit* za maana kabisa na sio kama wanatupwa au wanadharauliwa. Aidha, serikali itayafanyia mapendekezo ya kuona nyumba za serikali ambazo zitatumiwa na viongozi wetu wakuu wanapokuwa nje ya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Salma Mohammed Ali, Mhe. Mahmud Muhammed Mussa, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Machano Othman Said na Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, wote kwa pamoja tunawashukuru kwa pongezi zenu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi kubwa anazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo umeleta tija kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, serikali inatekeleza mapendekezo na ushauri ambao huwa unatolewa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupitia ripoti zake za kila mwaka. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad si kama ripoti tunazidharau hazishughulikiwi, laa! Ndani ya serikali, ndani ya *Cabinet* tunaijadili ripoti ile kwa undani kabisa na tunatoa mapendekezo na Makatibu Wakuu wote wapo na hapo tunatoa maamuzi nani afanywe nini. Kwa hivyo, *Cabinet* yenyewe chini ya mwenyewe Mhe. Rais tunatoa kipa umbele katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hivyo, tukimaliza sisi watu wote au waliohusika wote wanaambiwa wajibu hoja, halafu ripoti ile tena nayo munaletewa upande mwengine huku Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, si kama mapendekezo yake hayafanyiwi kazi na kuna mafanikio kabisa yamepatikana kutokana na ripoti zake. Hilo tunashukuru sana na pia upande wenu wa Kamati ya *PAC*. Pia, mapendekezo yenu nayo tunayathamini na yametusaidia sana kutoongoza upande wa serikali, mfano uliotolewa kuhusu kodi ya ardhi umetekelezwa na kupelekea makusanyo ya kodi hiyo kuongezeka kwa kiasi kikubwa kabisa. Sambamba na hilo, ushauri uliotolewa kujengwa ukuta katika nyumba za Wazee Sebleni umetekelezwa hata kabla ya Kamati ya *PAC* kufuatilia.

Mhe. Mwenyekiti, kufuatilia ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2011/2012 kuhusiana na soko la Mombosa kujengwa vibanda kinyume na utaratibu, yaani kuchafua taswira ya soko pamoja na uchafuzi wa mazingira, taasisi husika ilichukua hatua kwa kuvunja vibanda vyote ili kurejesha haina nzuri ya soko hilo, ndio kama nilivyosema hatua kwa kweli zinachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya kazi maalum ya mishahara na viinua mgongo. Ukaguzi umekamilika na ripoti yake ipo katika hatua za mwisho. Ukaguzi huo ulianza kwa kulipa mishahara wafanyakazi wote wa serikali ambapo kazi hiyo ilichukua zaidi ya miezi mitano. Katika masuala ya ulipaji wa viinua mgongo na pencheni nao umekamilika ambapo zoezi la kulipa pencheni kwa kuwatambua wastaafu wanaoendelea kulipwa pencheni umeanza.

Mhe. Mwenyekiti, hata matangazo ya redio juzi mumesikia wapo katika hatua ya mwisho wanaitwa kwenda na vitambulisho vyao na *documents* nyengine na *record* zote. Hilo ndilo zoezi ambalo sasa hivi ndio linakamilika. Miezi mitano walikuwa wanafanya kazi hiyo. Ukaguzi maalum kwa *ZMA* kama ilivyoshauriwa na Baraza lako tukufu, tayari umeshafanyika na ripoti yake tayari imeshawasilishwa serikalini kwa mujibu wa taratibu za serikali. Ripoti hiyo inatarajiwa kuwasilishwa katika kikao kijacho cha Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu kifungu namba 79 *"Scheme of service"* ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zitaanza kutumika katika mwaka wa fedha 2014/2015. Hakuna tofauti ya lugha kati ya Mwenyekiti wa *PAC* na maneno yangu, isipokuwa ninataka kusema tu kwamba marekebisho kidogo yalichukua muda ya zile hatua za kuanza kufanya marekebisho na mengine serikali imeshayakubali moja kwa moja, lakini na mengine bado vikao vinaendelea kulikamilisha hilo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, hakuna wasi wasi wowote. Ninathubutu kusema kwamba serikali mengi ya mapendekezo yao tumeyakubali, yale ya sehemu ndogo ndogo kama kawaida lazima kuwe na *quiries* za hapa na pale, bado vikao vinaendelea kati ya Tume ya Utumishi pamoja na *CAG* na serikali kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, serikali itatuchukua juhudi za makusudi kwa ajiri wataalamu wakiwemo wahandisi na wafanyakazi wa kada nyengine ili kuziba pengo la wataalamu katika Ofisi hiyo baada tu ya *Scheme of service* kutumika. Kulikuwa na wasi wasi kwamba labda kuna wataalamu hawana nao na hawawezi kuwaajiri. Kwa kweli baada ya kukamilika *Scheme of service* hii ni imani yetu kwamba *package* ile itaweza kuwavutia wataalamu ambapo hatuna nao katika Ofisi ile.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ni lazima tukumbuke tu jamani kwamba ushindani umekuwa mkali siku hizi na watu wote kwenye *Private sectors* inawavuta na sisi tunawavuta. Kwa hivyo, na sisi tunasema tujitahidi kama tulivyojitahidi kwenye sekta nyengine kama ya elimu na afya.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Ali Salim Haji, tunashukuru sana kwa ushauri wenu kuhusu utendaji wa *GSO* pamoja na kuifanyia marekebisho sheria ya *GSO* ili iweze kufanya uchunguzi wa kuwakagua wafanyakazi ambao ni raia wa nje wanaofanya kazi Zanzibar. Ushauri wao tunauchukua na tutaufanyia kazi kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini ninataka kusema tu kwamba pamoja na hayo, naomba niwakumbushe kwamba Ofisi hii ya *GSO* hufanya kazi zake kwa kufuata miongozo iliopo katika sheria ya Utumishi wa Umma, ambapo imepewa mamlaka ya kisheria kufanya upekuzi, yaani *Security veting* kwa watumishi wa umma tu.

Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kumuhakikishia Mhe. Hija Hassan Hija kwamba upekuzi unaofanywa na Ofisi ya *GSO* haufanywi kwa upendeleo. Hili tumelisema mara nyingi tu na kama tunafanya kwa upendeleo tupo tayari mutuletee kesi kama hizo, tutazungumza na tutazipatia ufumbuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kunakuwa kwa kweli na matatizo madogo madogo ya kiutendaji, lakini matatizo ya kibinadamu, sio kwamba kuna upendeleo, huyu anaulizwa chama gani, hayapo kabisa. Hiyo, fomu ninakumbuka mwaka juzi tulionesha kabisa na tuliileta hapa, hamna kabisa fomu kama hiyo. Kwa hivyo, upendeleo kabisa haupo, lakini kimsingi Ofisi hii haifanyi ajira, hiyo ninataka tukumbuke. Kwa mujibu wa sheria inayoongozwa na Ofisi hii kazi yake ni kufanya uchunguzi (*Vetting*) ambapo kazi hii pia imeainishwa katika sheria ya Utumishi wa Umma.Uchunguzi huu hufanywa kwa watumishi ambao tayari wamefanyiwa mahojiano na waliofaulu kwa mujibu wa taratibu za Tume ya Utumishi Serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya uchunguzi kufanywa *GSO* hupeleka maoni yake kwa taasisi husika. Wale walioleta hurejeshewa majibu wao. Taasisi za serikali kutoa ushirikiano kwa *GSO* kama sheria inavyowataka. Kumradhi nimeruka kidogo, baada ya uchunguzi kufanywa *GSO,* hupeleka maoni yake kwa taasisi husika. Aidha, namshukuru Mhe. Ali Salim Haji kwa kuzikumbusha Taasisi za Serikali kutoa ushirikiano kwa *GSO* kama sheria inavyoagiza au inavyowataka.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mchango wa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje (DIASPORA) pamoja na ushirikiano wa Jumuiya za Kikanda zimechangiwa na Waheshimiwa wengi nao kama nilivyosema Mhe. Shadya Mohammed, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Fatma Mbarouk Said, Mhe. Ali Salim Haji, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Farida Amour Mohammed na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwapongeze Waheshimiwa Wajumbe wote hao kwa kutuunga mkono katika kuhakikisha kuwa tunawashajihisha DIASPORA kwa Zanzibar ili waweze kuchangia maendeleo ya nchi yetu. Aidha, utafiti unaokusudiwa kufanywa kwa mwaka ujao wa fedha unalenga kutambua michango ya Wazanzibari wanaoishi nchi za nje katika maendeleo ya uchumi na kijamii ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa serikali inawatambua Wazanzibari wanaoishi nchi za nje kupitia Jumuiya zao za ZAWA na ZAKADIA na Umoja wa Wazanzibari wanaoishi katika nchi za Scandinavia ambazo wameziazisha katika nchi wanazoishi pamoja na pale ambapo wanakuja wao wenyewe binafsi kujitambulisha katika Ofisi yetu. Sambamba na hayo juhudi za makusudi Ofisi yangu inafanya za kuwatambua Diaspora wa Zanzibar kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wakiwemo Benki Watu wa Zanzibar, Mfuko wa Hifadhi wa Jamii, *ZIPA* na Shirika la Bima ambapo safari katika nchi za Oman, Uingereza, Denmark, Sweden, Marekani na Dubai zimefanyika kwa lengo la kuwatambua na kuwashajihisha DIASPORA wa Zanzibar wanaoishi katika nchi hizo kuchangia maendeleo katika nchi yao.

Mhe. Mwenyekiti, ninachukua fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu idara yetu inayoratibu masuala ya Diaspora, hivi sasa wameshapatiwa Ofisi nje ya jengo la Ikulu kama Waheshimiwa Wajumbe mulivyotushauri. Ushauri huo tumeuchukua tukalitengeneza lile jengo na Ofisi, sasa imeshahamia pale, haipo ndani ya Ikulu tena. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, aidha, sera ya Diaspora ambayo itaweka mazingira bora na rafiki yatakayowezesha Diaspora wa Zanzibar kuchangia maendeleo ya nchi yao kwa urahisi, imo katika hatua za mwisho kukamilishwa. Halikadhalika Kamati maalum ya utaratibu wa uchumaji wa fedha (*Remittances*) zinazoingia nchini kutoka kwa Wazanzibari wanaoishi nchi za nje imeundwa ambayo inatarajiwa kutoa mapendekezo ya mfumo bora wa utumaji wa fedha hizo. Tayari kazi hii inafanya na maendeleo yake mazuri kabisa, tutawajuulisha itakapokamilika.

Mhe. Mwenyekiti, serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba wataalamu wanawezeshwa kushiriki katika mikutano ya Jumuiya za Kikanda ikiwemo Jumuiya ya Afrika ya Mashariki na *SADC*. Katika kuhakikisha hilo linatekelezwa

kama lilivyopangwa mwaka ujao wa fedha, wataalamu hao watawezeshwa kushiriki mikutano hiyo kupitia bajeti maalum iliyotengwa katika Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, ipo haja au ipo baadhi ya mikutano Jumuiya ya Afrika ya Mashariki huwa inawawezesha wataalamu wa nchi wanachama kushiriki wakiwemo wataalamu wa Zanzibar. Ninapenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mhe. Samwel Sitta - Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuweka utaratibu maalum ambao hutujuulisha rasmi taarifa zote na mialiko inayohusiana na mikutano ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, mkataba wa makubaliano wa kuanzishwa kwa Kamisheni ya Kiswahili ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ni kweli bado haijasainiwa Mhe. Mgeni Hassan Juma, tunakubali ni kweli, lakini hii imetokana na kusubiri kwa maamuzi ya serikali ambayo tayari serikali imeshatoa sasa maamuzi na Makao Makuu ya Kamisheni hiyo ambayo yatakuwa katika Ofisi iliyokuwa ya *EACROTANAL* hapo mpirani.

Mhe. Mwenyekiti, jengo lile tayari serikali imekubali kuwapa Kamisheni ile na itakuwa kwa hapa kwetu chini ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo kwa muda. Kwa mintarafu hiyo, makubaliano hayo ya kuanzishwa kwa Kamisheni itasainiwa mara moja baada ya kukamilika hatua muhimu ambayo ninasema ilikuwa ni uamuzi wa jengo. Sasa madhali jengo limeshapatikana hiyo hatua tutaitekeleza mapema iwezekanavyo na pesa, kwa kweli kama nilivyosema zimeshatengwa. Kwa hivyo, kwa kweli hakuna tena sababu kwa nini hili suala lisi-*take off.*

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Shadya Mohammed, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Panya Ali Mhe. Mwenyekiti, Abdalla, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Mohammed Haji Khalid, Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa na Mhe. Jaku Hashim Ayoub, tunawashukuru sana na nawapongeza kwa michango na mapendekezo muliyoitoa juu ya dhana nzima ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, nawaahidi Ofisi yangu itayafanyia kazi mapendekezo yote muliyotushauri. Sera ya Utawala Bora ya mwaka 2011 imetoa nini, maana ya utawala bora, maana hiyo ni kuwa vile ambavyo serikali inafanya serikali zake katika maeneo yake na namna inavyoweka mahusiano na wananchi, Jumuiya za kiraia pamoja na taasisi nyengine.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, misingi ya utawala bora ni uwajibikaji, utawala wa sheria na haki za binadamu, kuzuia rushwa, ufanisi na tija, ushirikishwaji wa wananchi na kuzingatia matakwa ya wananchi. Hiyo ndio misingi ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, miongoni mwa kazi kubwa za Idara ya Utawala Bora ni kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuelewa misingi ya utawala bora. Elimu hii hutolewa kwa njia ya redio, televisheni na semina za ziara katika Shehia *(Outs rich programme).* Kazi nyengine ya Idara hii ni kuratibu na kusimamia masuala ya utawala bora katika taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, halikadhalika, Idara ya Utawala Bora ina kazi ya kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuwapatia ushauri unaofaa. Kazi nyengine ni utekelezaji wa sera ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama walivyosema Waheshimiwa Wajumbe hasa Mhe. Wanu Hafidh Ameir kwamba shilingi ishirini milioni, nimesema hiyo kwamba hazitoweza kununua gari. Lengo la kuweka fedha hizo ni kuiwezesha Idara ya Utawala Bora kupata gari itakayonunuliwa kwa njia ya kufanya malipo kwa awamu, ambapo fedha hizo ni kwa ajili ya malipo ya awamu ya kwanza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa Tume ya Mipango. Waheshimiwa Wajumbe, waliochangia nawataja kabisa wote ni pamoja na Mhe. Shadya Mohammed Suleiman, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Panya Ali Abdalla, Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Farida Amour Mohammed, Mhe. Marina Joel Thomas na Mhe. Machano Othman Said, ambao waligusia suala la umaskini kwa wananchi wengi wa Zanzibar.

Mapendekezo ya kufanya bajeti mapema kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, mashirikiano wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ushiriki wa wananchi katika sensa na tafiti zinazoendeshwa na serikali, utekelezaji wa malengo kwa asilimia mia moja. Ongezeko la mishahara sambamba na mfumko wa bei, yote hayo waliyachangia, matokeo ya ufuatiliaji na tathmini inayofanywa katika programu na miradi yote ya maendeleo, mashirikiano baina ya sekta binafsi na sekta za umma.

Pia, waligusia lile suala la tofauti ya shilingi milioni 149.1 zilizotengwa kwa kazi za kawaida na kilichopatikana shilingi milioni 135. 1 sawa na asilimia 130.9. Waliuliza kwa nini ongezeko hili kubwa hivi.

Vile vile, kwa Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watendakazi, mpango wa MKURUBITA pia waliuzungumzia na mfanano wa majukumu ya Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo ya Sekta na kupunguza Umaskini na Idara ya Ukuzaji Uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa nitowe kwa ufupi tu maelezo haya yote ya mambo niliyoyagusa. Mhe. Mwenyekiti, kutokana na utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ya mwaka 2009/2010, wananchi wanaoishi chini ya kiwango cha mahitaji ya msingi, yaani chakula, mavazi na makaazi ni asilimia 44. Mikakati inayoendelea kuchukuliwa na serikali hasa kwa wilaya zilizoonekana maskini kama Micheweni ni pamoja na kuanzisha programu maalum ya kuendeleza wilaya kwa kupeleka huduma za maji, kuweka skuli ya maandalizi, kuimarisha kituo cha afya, kuwaendeleza wakulima wa umwagiliaji, kuweka redio ya jamii ili kuwahamasisha wananchi kufanya mambo ya maendeleo.

Aidha, programu na miradi zinazotekelezwa na MKUZA zimelegwa kusaidia kuimarisha kipato cha wananchi na kupunguza umaskini na kuwa sasa *TASAF* itaanza kufanya uhaulishaji wa fedha kwa kaya maskini zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, pia tume itafanya utafiti wa vijiji vitano katika Mkoa wa Kaskazini Unguja, kuhusu kufanya mapendekezo ya bajeti mapema kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha. Ushauri huu tumeupokea na tutaufanyia kazi Inshaalla. Aidha, wazo la kuwa na mashirikiano wakati wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na wananchi, ni wazo zuri Mhe. Mgeni Hassan na tunalichukua kwa kulizingatia.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kutoa wito kwa wananchi wote kushirikiana na taasisi mbali mbali za serikali, katika kushiriki na kutoa majibu sahihi ili serikali iweze kupata takwimu sahihi ambazo hutumiwa katika mipango ya maendeleo ya wananchi. Hata hivyo, napenda kumtoa wasi wasi mheshimiwa na wananchi kwa jumla, kwamba lengo kuu la sensa ya watu na makaazi kwa kupata idadi sahihi ya wakaazi wa Zanzibar, ilifikiwa kwa kiwango kikubwa, licha ya changamoto kadhaa zilizojitokeza kwa baadhi ya wananchi kuwashawishi wenzao kukataa kuhesabiwa.

Aidha, suala la kutofikia utekelezaji halisi kwa asilimia mia moja ya malengo, inachangiwa na mambo mbali mbali. Kubwa ikiwa ni upatikanaji wa fedha, ambapo huwa zinachelewa au kupatikana pungufu. Pia, kuwepo na utaratibu wa manunuzi huwa ni mgumu na unachukua muda mrefu. Kuna upungufu katika kupanga na kutekeleza na kufuatilia kutokana na upungufu wa wataalamu. Vile vile na hali ya hewa nayo mara nyingi huwa inasababisha kutokufikia malengo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la mfumko wa bei wa Zanzibar. Hili huathiriwa na uagiziaji wa bidhaa hasa chakula nje ya nchi. Kwa kipindi cha miaka ya hivi karibuni kasi ya mfumko wa bei imeendelea kushuka na kudhibitiwa katika tarakimu moja. Hilo tunashukuru sana na lazima tuipongeze serikali yetu kwa hili au nchi yetu. Hadi kufikia mwezi Aprili mwaka huu, mwenendo wa mfumko wa bei ulirikodiwa kama ifuatavyo:-

Januari ilikuwa asilimia 2.8, Februari asilimia 0.1, Machi asilimia 0.6 na Aprili asilimia 1.3. Kuendelea kudhibitiwa kwa mfumko wa bei kwa bidhaa, kumetokana na matunda ya juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kudhibiti mfumko huo wa bei kama ifuatavyo.

1. Serikali imeendelea na utoaji wa ruzuku na pembejeo kwa wakulima, kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao hasa ya chakula ambao umepelekea kupunguza kiwango cha uagizaji bidhaa za chakula nje ya nchi.

2. Serikali imeendelea kutoa nafuu ya kodi kwa bidhaa za chakula zinazoingizwa nchini kwa lengo la kupunguza ukali wa maisha kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, zoezi la ufuatiliaji miradi na programu ya maendeleo, suala hili alilizungumza Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mhe. Marina Joel Thomas na yeye pia alilizungumza. Suala hili hufanyika kila mwaka kuangalia matumizi ya fedha zinazotolewa na ufanisi uliopatikana kutokana na mipango iliyopangwa.

Aidha, mafanikio na changamoto za utekelezaji kuweza huweza kujadiliwa. Katika kipindi cha utekelezaji kwa mwaka huu ziara mbili zilifanyika na miradi 60 kutembelewa, ikiwemo miradi ya barabara, ujenzi wa nyumba, maskuli na vituo vya afya. Tathmini ya miradi iliyofanywa ilipelekea mambo yafuatayo kubainika.

Kwanza, baadhi ya miradi kuondolewa katika mpango na kupelekwa katika kazi za maendeleo. Kama mradi wa Mfuko wa Afya Wilayani, Mawasiliano Ikulu, Uhai Hifadhi ya Mama na Mtoto. Miradi hii baada ya tathmini imeweza kuondolewa kabisa. Hapana, sio kuondolewa kabisa, lakini imepelekwa kwenye *recurrent*.

Pili, baadhi ya miradi kuombewa fedha ili iweze kukamilika katika kipindi cha mwaka huu wa fedha. Mfano, uimarishaji wa *SUZA* awamu ya kwanza, ujenzi wa jengo la Wizara ya Katiba na Sheria, mradi wa ujenzi wa studio na muziki na ujenzi wa ujenzi wa maktaba Pemba.

Tatu, baadhi ya miradi kuahirishwa utekelezaji wake Mfano, ukanda wa kiuchumi *special economic zone,* na mradi wa ujenzi wa maabara ya Compyuta *ZIFA*.

Mwisho, kutoa ushauri wa sekta kuimarisha utekelezaji wa miradi.

Mhe. Mwenyekiti, dhana ya mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, yaani *PPP*. Kwa sote ni ngeni kwetu na maana yake ni makubaliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi, ambapo sekta binafsi inatoa huduma au kutekeleza miradi ambayo iliyokuwa ikitekelezwa na serikali. Hivi sasa serikali imo katika maandalizi ya sera, mapitio ya sheria na miongozo ya PPP ambapo itakapokamilika kwa muongozo huo, utasaidia kutambua miradi muhimu itakayotekelezwa kwa mfumo wa *PPP*.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu asilimia 6.7 iliyotolewa kwa mwaka 2013/14, hii imetokana na kuchelewa kupata washauri elekezi, ambapo fedha hizo zilizopatikana zimetumika kuwapeleka maafisa wa kitengo cha *PPP* Tanzania Bara ili waweze kujenga uzoefu. Kwa hivi sasa, kazi ya matayarisho ya sera muongozo wa sheria inayofanyika hupatiwa fedha na benki ya dunia.

Mhe. Mwenyekiti, ziada ya matumizi ilioneshwa ile asilimia 130.9 kama Waheshimiwa Wajumbe kadhaa walivyotuambia. Maelezo yake ni kwamba, gharama za shughuli za utawala na uendeshaji za Tume ya Mipango, ikiwa ni pamoja na malipo ya mishahara kulipwa kwa kutumia fungu la Idara ya Mipango na Maendeleo ya watendakazi tangu mwezi Agosti mwaka jana, kufuatia mabadiliko yaliyofanywa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kuiondosha tume kutoka Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Aidha, kimsingi majukumu ya idara ya ukuzaji uchumi na mipango ya maendeleo ya kitaifa na mipango ya kitaifa, maendeleo ya kisekta na kupunguza umaskini yanatofautiana, ipo tofauti katika idara hizo mbili. Idara ya Ukuzaji Uchumi miongoni mwa majukumu yake ni kufuatilia na kutathmini mwenendo wa uchumi, kwa lengo la kuhakikisha utulivu wa uchumi mpana na wenye kuhimili ushindani wa kimataifa unaozingatia maskini, ambapo idara ya mipango ya kitaifa, maendeleo ya kisekta na kupunguza umaskini, miongoni mwa majukumu yake ni kupanga, kuratibu, kufuatilia na kutathmini mipango ya kitaifa.

Pia, programu za maendeleo na kupima mapitio ya sekta, pamoja na kufuatilia utekelezaji wa MKUZA. Kwa hivyo, ipo tofauti hapo. Lakini hivi vitu haviendi peke yake peke yake, lazima kuna mwingiliano kidogo, lazima wanategemeana kidogo. Lakini kila mmoja ana majukumu yake na ana kazi zinakwenda vizuri tu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukuwe nafasi ya kipekee kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wa Baraza lako, waliochangia kwa kutoa maoni, mapendekezo na ushauri juu ya kuendeleza juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi. Kama walivyosema waheshimiwa wengi sana takriban wote, walizungumzia

suala la mamlaka hii. Wajumbe hao ni Mhe. Shadya Mohammed, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mhe. Fatma Mbaouk Said, Mhe. Mohammed Mbwana, Mhe. Mussa Ali Hassan, Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Salma Mussa Bilal, Mhe. Jaku Hashim Ayoub, Mhe. Abdi Mosi Kombo, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Machano Othman Said na wengi tu, takriban kama nilivyosema waheshimiwa wote waliozungumza basi walizungumzia suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba hakuna jibu la moja kwa moja linaloweza kuelezea sababu za kutokea kwa rushwa, kwa kuwa kila mmoja anachukua rushwa kwa sababu anayoijua mwenyewe. Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti ya tathmini ya shughuli za kuzuwia rushwa Zanzibar ya mwaka 2012, imeeleza baadhi ya mambo yafuatayo ndio yanayopelekea kutokea kwa rushwa hapa Zanzibar.

Kwanza, muhali. Hii inatokana na maingiliano au mahusiano makubwa ya jamii ya Kizanzibari.

Pili, urasimu katika kupata huduma, kila mmoja anataka *shortcut*.

Tatu, mahitaji kuwa ni makubwa kuliko huduma iliyotolewa. Mfano, suala la ajira kuwa ni chache kuliko wahitaji wa ajira.

Nne, usiri wa kupata taarifa.

Tano, uelewa mdogo wa wananchi juu ya majukumu ya kisheria ya watu wenye dhamana juu ya mambo au huduma mbali mbali katika kupata haki zao.

Sita, tamaa nayo ni chanzo kikubwa cha rushwa. Lakini rushwa ni lazima tujuwe kwamba wahusika wakuu ni mtoaji na mpokeaji, tusiende upande mmoja, wote wawili ni *victim*.

Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla wake rushwa inatokana na udhaifu wa tabia wa tabia ya mtu husika. Mhe. Mwenyekiti, serikali inafanya juhudi za makusudi kuona kwamba maslahi ya watumishi ya mamlaka ya rushwa na uhujumu uchumi yanazingatiwa, ili watumishi hao waweze kufanyakazi zao kwa ufanisi na kwa mujibu wa sheria. *Scheme of Service* yao imeshaandaliwa na tayari imeshawasilishwa Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma.

Aidha, mamlaka hii kwa mwaka ujao itafungua ofisi yake rasmi huko Pemba. Hata hivyo, pamoja na kwamba hakuna Ofisi, lakini shughuli za mamlaka ya kuzuia rushwa zinaendelea kama kawaida huko Pemba. Hivi sasa watendaji wa mamlaka wako Pemba wanafuatilia tuhuma mbali mbali zikiwemo magendo ya karafuu. Pia, elimu kwa umma imetolewa zaidi huko Pemba kuliko Unguja. Hadi sasa jumla ya wananchi wa shehia 22 zimefikiwa kupatiwa elimu, pamoja na watendaji mbali mbali wa serikali wakiwemo Maafisa Tawala na Maafisa Wadhamini.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzia mwezi Oktoba mwaka jana, hadi Mwezi Machi mwaka huu, mamlaka imefanya uchunguzi wa tuhuma 21 na majalada matano kati ya tuhuma hizo yameshawasilishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka. Sio kama kitengo au mamlaka haifanyi kitu, kama labda waheshimiwa wengine walivyodhani. Ukilinganisha muda wa kuanzishwa kwa mamlaka hiyo hadi hivi sasa, imeweza kufanya kazi kubwa tena kwa muda mfupi.

Mhe. Mwenyekiti, elimu inayotolewa katika ngazi ya shehia juu ya mapambano dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi, inalenga kuwajumuisha wananchi wote wanaoishi katika shehia husika, wakiwemo viongozi wa ngazi mbali mbali na wananchi wa kawaida. Aidha, katika vita dhidi ya rushwa na uhujumu uchumi, hakuna watu wadogo wala wakubwa, wote ni muhimu.

Mfano, Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, wananchi wa Jimbo la Kitope na majimbo jirani, wanajukumu muhimu la kuhakikisha mashamba ya miwa, ambayo ni mali ghafi ya msingi katika uendeshaji wa Kiwanda cha Sukari cha Mahonda, ambacho ni sehemu ya juhudi ya ukuzaji wa uchumi wa Zanzibar hayahujumiwi kwa manufaa yao na kwa nchi kwa ujumla.

Kwa hivyo, elimu kuhusu rushwa na uhujumu wa uchumi kwao ni miongoni mwa jitihada muhimu za kudhibiti uhujumu wa uchumi pale Mahonda. Sambamba na hayo suala la vita dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi ni jukumu mtambuka, ambalo linamuhusu kila mmoja wetu. Nachukua fursa hii kuwasilisha ombi maalum kwetu sote

Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza na wananchi kwa jumla, kwamba tushiriki katika vita dhidi ya rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Wanu Hafidh Ameir pamoja na mambo mengine alizungumzia umuhimu wa kutayarisha *documentary film*, wakati wa ziara za Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Mhe. Wanu Hafidh alishauri Idara ya Faragha kushirikiana na Idara ya Mawasiliano Ikulu, ili kuweza kufanya *direct coverage* ya moja kwa moja, wakati Mhe. Rais akiwa nje ya nchi. Ushauri wake tumeupokea, tunauthamini na tutaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze pia Mhe. Mgeni Hassan Juma kwa ushauri na pongezi alizozitoa katika ofisi yangu. Aidha, serikali imepokea na kuupa umuhimu ushauri wake wa kutenga eneo maalum kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi. Ushauri wake tumeupokea na tunaahidi kuufanyia kazi kivitendo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nimuhakikishie Mhe. Mgeni Hassan kuwa ushauri wake juu ya kuzingatia masuala ya kijinsia pia nao umeuchukua, na Inshaalla tutauzingatia katika masuala yetu ya bajeti yanayofuata.

Kwa kumalizia, naomba nimshukuru sana Mhe. Machano Othman Said MBM na Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, kwa kusaidia uchambuzi wa hoja mbali mbali na hasa kwenye takwimu, maendeleo na mengine. Aidha, naomba nimshukuru pia Mhe. Thuwaybah Edington Kisasi Mwakilishi wa Jimbo la Fuoni na Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa shukrani zake kwa Mhe. Rais, kwa suala zima la kushajihisha michango ya miradi ya maendeleo wilayani na mikoani. Miradi hii ni yetu, iwe ni changamoto kwetu kwamba sisi ni lazima tushajihishe michango, halafu watu wengine waweze kufuata. Tunachukua pongezi zako mheshimiwa.

Lakini pia, Mhe. Mwenyekiti, wewe mwenyewe binafsi tunakushukuru sana kwa mchango wako na dhana nzima ya suala la utawala bora. Nafikiri tumejitahidi kulieleza kama ilivyopaswa.

Mhe. Mwenyekiti, nimejitahidi sana ku-*cover* michango takriban yote ambayo tumeona ni mikubwa na ni muhimu ambayo mmetupa au mmetushauri. Sasa naomba sana kama tumesahau au tumeghafilika naomba ichukuliwe kama binadamu. Tumejitahidi kueleza kwenye kitabu na tumejitahidi kufafanua. Kwa hivyo, naomba tuwe pamoja tumalize ungwe yetu hii na *Inshaalla* tushirikiane zaidi na matuletee mashauri yenu zaidi ofisini na kwenye kamati.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante hoja imeungwa mkono. Sasa tuwahoji basi wale wajumbe wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono. Wanaokataa. Waliokubali wameshinda. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu: Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza limejadili na kuikubali hotuba ya bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, sasa naliomba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi, ili kupitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU 11 - OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja- 18,000,000
Jumla ya Fungu- **18,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 007 - OFISI YA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA NA URATIBU WA WAZANZIBARI WANAOISHI NCHI ZA NJE

Kifungu 0601 Kuratibu uchumi na ushirikiano wa Kimataifa- 808,200,000

Jumla ya Fungu- **808,200,00**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

FUNGU 008 - AFISI YA RAIS BARAZA LA MAPINDUZI

Kifungu 0501 Baraza la Mapinduzi- 1,458,200,000

Jumla ya Fungu- **1,458,200,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 10 - AFISI YA RAIS IKULU NA UTAWALA BORA

Kifungu 0101	Idara ya Utawala bora -	227,732,000	
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba -	599,906,000	
Kifungu 0401	Idara ya Mipango Seria na Utafiti-	428,324,000	
Kifungu 0701	Afisi ya Faragha -	2,446,754,000	
Kifungu 1101	Idara ya Utumishi na Uendeshaji-	1,131,388,000	
Kifungu 1601	Kitengo cha Ofisi ya Usalama wa SMZ-	47,120,000	
Kifungu 1801	Kitengo cha Mawasiliano na Habari-	225,862,000	

Jumla ya fungu - **5,107,446,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumibi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 11 - AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZANZIBAR

Kifungu 0201 Utawala Unguja -

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ilikuwa nataka ufafanuzi wa ziada pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri, juu ya suala zima la *Scheme of service* ya Ofisi ya *CAG* kulikuwa na mgongano juu ya taarifa baina ya Mhe. Waziri na mgongano wa taarifa ya Mwenyekiti wa kamati ya *PAC*, Mhe. Waziri alisema na alisisitiza kuwa maslahi ya Ofisi ya *CAG* imeshughulikiwa na sasa hivi ipo tayari, lakini kamati ya Mwenyekiti alionesha kwamba bado maslahi ya *CAG* hayajazingatiwa kama *Scheme of Service*.

Sasa naomba Mhe. Waziri atupe kauli ya mwisho na ya uhakika awape wajumbe wa kamati kwamba je suala zima la *Scheme of Service* ya Ofisi ya *CAG* tayari limemalizika ili kuweka rikodi sawa baina ya ripoti yake na ripoti ya kamati.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Kama nilivyosema mwanzo kweli kulikuwa na utata kidogo, ile *scheme of service* walivyotayarisha wenyewe kupeleka Tume kidogo kukawa na labda niseme waliona vitu vingine vikubwa sana, sasa kukawa na kwiri na wakataka maelezo zaidi na hapo nafikiri ndio wengine wakapata habari kwamba labda hii imekwama, lakini kama nilivyosema tumelikwamua baada ya kulikwamua mazungumzo hivi ninavyosema Mhe. Hija Hassan Hija mazungumzo yanaendelea, na baadhi ya vifungu au baadhi ya sehemu kubwa kabisa imeshakamilika na Serikali wameshaikubali.

Sasa wanakamilisha taratibu ndogo tu zilizobaki kwa hivyo naomba achukue kauli yangu ya ukweli kabisa, alivyosema Mwenyekiti wa *PAC* kweli hapo mwanzo kulikuwa na matatizo nakiri kabisa ni kweli, lakini Serikali tumeingilia kati *Alhamdullillahi* liko katika sura nzuri kabisa.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti mimi napata mashaka mazungumzo yanaendelea au tayari imeshakubaliwa, maana ukisema kuzungumza maana yake hakuna makubaliano sasa je, wanaendelea kujadiliana au imekubaliwa, mimi ninachopenda kusikia kwamba sasa tayari hoja ile ya Ofisi ya *CAG* imekubaliwa. Mazungumzo

hata Baraza la Wawakilishi walizungumza miaka mitano nyuma na tayari limetupiliwa mbali. Sasa je Ofisi ya *CAG* wamezungumza au tayari wamekubaliwa nataka kujua hilo tu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Naomba nirejee tena niseme position kubwa unajua lile dubwana kubwa dio maana yake karatasi mbili au tatu na lazima uchambue, sasa mwanzo nakiri kama nilivyosema ilikwama tukaanzisha mazungumzo na *position* kubwa Mkuu wa Utumishi ni Katibu Mkuu wa Baraza la Mapinduzi akaidhinisha sehemu kubwa kabisa, sasa mna vipengele vidogo vidogo tu ni vya kawaida hivyo vifanyiwe kazi viwekwe sawa. Lakini naweza kuseme sehemu kubwa vimeshakubaliwa na nakiri hilo kwamba imeshakubaliwa hivi ni vya kuweka sawa tu ambavyo hii kazi leo au kesho inaweza kumalizika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ninavyojua mimi ni kwamba muundo uliokubalika kwa maana ya vyeo, kuna wakurugenzi pale wakubaliwe kuwepo kama ambavyo Baraza la Wawakilishi walikubaliwa kuweka vyeo bandia lakini cheo kinakwenda sambamba na maslahi. Mimi naomba Mhe. Waziri aniambie maslahi kwa mujibu wa vyeo yamekubaliwa au ndio yanazungumzwa, kama yanazungumzwa maslahi maana yake hakuna kilichokubaliwa. Sio vyeo hapa tunao wakurugenzi wa baraza, kuna nani lakini vyeo tu ni jina tu mtu kuambiwa shehe kwa sababu anavaa kofia lakini maslahi hayajazingatia lile jambo.

Naomba Mhe. Waziri aniambie maslahi yamezingatia vyeo, kama wanazungumza bado atwambie tu kwamba bado suala gumu bado wawakilishi watetee lakini atwambie wapi maslahi yamekubaliwa au ndio mazungumzo maslahi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti mimi sio mtaalam sana wa utayarishaji wa *scheme of service* lakini unaposema *scheme of service* bila ya shaka muundo cheo na mshahara, cheo na mshahara na unaanza leo hapa, mfano karani masjala mfano tu *grade* tatu baada ya mwaka au baada ya miezi mitatu unapanda juu, sasa cheo kile kinawekwa na mshahara wake.

Sasa hayo niseme Mhe. Hija Hassan Hija hayo yameshafanyika na yameshakubalika, lakini ukitaka nikwambie kwamba imeshatoka, aa! siwezi kusema uongo haijatoka lazima wanaimalizia malizia Tume na nikiri tena kama nilivyosema ilikwama, sasa hilo zoezi linamalizika hivi sasa na imani yangu kwamba ndani ya wiki moja mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Hija baada ya hauo utakuwa kidogo umeridhika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, baada ya kuwasiliana na wenzangu tumepata jibu la kitaalam sasa tumeamua tusubiri utumishi wa umma tuje tuhoji suala kwa hivyo tuendelee.

Kifungu 0201	Utawala Unguja -	1,500,126,000
Kifungu 0301	Ofisi Kuu Pemba -	522,874,000
	Juma ya Fungu-	**2,023,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo Juu Vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko Yoyote)

FUNGU 49 - TUME YA MIPANGO

Kifungu 1000	Idara ya Utawala na Huduma-	810,053,000
Kifungu 1001	Idara ya Ukuzaji Uchumi -	463,703,000
Kifungu 1002	Idara ya Mipango ya Kitaifa Maendeleo na sekta ya kupunguza umasikini-	441,379,000
Kifungu 1003	Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi-	243,765,000
Kifungu 2001	Ofisi ya -	

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, tokea kilipoanzisha kitengo hiki mwanzo kabisa nilikuwa nikikipigia kelele sana kitengo hiki hakina baba hakina mama yatima. Mhe. Mwinyi Haji kapata Wizara hii kuiongoza tukubaliane mimi au yeye mmoja awe baba mmoja awe mama, nafikiri mimi nitakuwa mama kwa kutengeneza kitengo hiki, sasa hivi mume wangu atakuwa Mhe. Mwinyi Haji kifungu hiki cha kusikitisha na cha kutia uchungu Mhe. Haji Omar Kheri tulizozana sana kwenye kifungu hiki, nikamwambia Serikali inafanya mzaha

na kifungu hiki haijawa tayari, cha kusikitisha leo hata mtu kama atamuongoza mtu kama ngombe kwa mikwaju gari haiendi. Tokea kuanzishwa tarehe 15/10/2012 haina gari, kimepata juzi miezi miwili haijafika kutoka kwa *UNDP*. Mheshimiwa nikuombe sana tukiwa walezi mimi na wewe lini utawapa gari hawa, ni hayo tu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa zungumza na kiti.

Mhe. Hija Hassan Hija: Ahsante Mkuu nazungumza na kiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuna hoja mbili hapo unapoteza muda, kitengo hiki kinaingiziwa milioni tano au milioni kumi tunafanyakazi kweli kwa milioni tano, ikiwa kitengo hichi katika mkutano kuwatetea wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wametumia milioni ishirini, milioni tano wanafanya ule mchezo wa karata wa chanisi kizigo.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mhe. Jaku Hashim Ayoub alipochangia alizungumza kwa hamasa sana na azma ya kuona kwamba mambo yanakwenda, naomba nimhakikishie tu Mhe. Jaku Hashim Ayoub kuanza jambo ni kazi kubwa sana lazima ujipange vizuri, ili mipango iende utakako, na usitizame na wenzetu kama walipoanza waliruka tu nao walianza.

Hivi sasa suala la gari, hili limo njiani ndani ya miezi mitatu namhakikishia gari pesa zake zipo tayari gari watapatiwa, mbali ya gari ya *UNDP* gari tayari ipo njiani watapewa na mipango yake mingine mizuri tu Mhe. Jaku na mwenyewe ataona na nitamuomba sana aje tushirikiane zaidi kuiendeleza mimi nitamualika Ofisini Mheshimiwa aone ile mipango inakwenda vizuri. Ahsante Mwenyekiti.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti, hiki kitengo kimetengewa milioni 80 katika miaka iliyopita, milioni 80 hazikukidhi kupata gari leo karibu mwaka wakatafuta vifungu vyengine wakazawadiwa, wakaongeza, wakazaa wakapata milioni ishirini au milioni mia kwa kununua gari *land cruiser* ni muda gani, narudia tena mimi na yeye ndio walezi wa hicho kikundi. Hakiwezi kufika leo unafika mwaka mpaka bajeti inakuja hapa milioni 100 gari mpaka leo haijanunuliwa taratibu zote wameshakamilisha, vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub Mhe. Waziri amejibu kwamba gari tayari inakuja katika kipindi kifupi itakuwa imeshafika, sasa tatizo lako liko wapi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa uzoefu ninavyoambiwa na mawaziri ishatokezea serikali ipo mbioni, matunda yake baada ya muda mfupi utayaona wakati wowote ndio lugha zetu humu ndani siku zote hizi, hebu anipe tarehe lini, mwaka mzima imekaa haina gari na pesa zao zipo milioni 100 utaratibu haujafanywa mpaka tunafika leo hatuwafanyii haki. Watamkamata na kumuongoza vipi hawa watu ndio utawala bora unavyosema hivi, kuwa muongoze kwa mikwaju mpaka mjini mtu yuko Makunduchi huko, anataka kumleta mjini kuja kuripoti ndio kweli tunafanya haki, si mzaha huu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti nathubutu kusema kwamba tumeshalipa, unajua mambo ya gari ya usafirishaji tumeahidiwa na sisi hivyo hivyo tunaitaka ije kila siku tunaambiwa kesho mara keshokutwa, lakini kubwa nasema tumeshaji-*commit* na tumeshalipa kwa hivyo gari *any time* itakuja. Mimi naomba anipe miezi mitatu halafu nimualike aje afungue makaratasi ya gari yeye mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku unaambiwa gari baada ya miezi mitatu itakuwa imefika na wewe ukafungue makaratasi.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kwa maana hiyo mamlaka isifanye kazi mpaka miezi mitatu ije kama mtu karipotiwa Makunduchi huko isifanye kazi, hilo naona halina tatizo naona tuendelee kifungu cha pili huu mchezo wa kuingiziwa milioni tano au sita utamalizika lini ili mamlaka iweze kufanya kazi. Hiyo miezi mitatu mimi nimeshakubaliana nayo Mhe. Waziri kama mimi na yeye tuwe walezi wa hicho kikundi hakuna tatizo. Hii kuingiziwa milioni tano au saba utakwisha lini utaratibu huu.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mimi kama uwezo ungekuwa upo tungependa tuingiziwe zote kwa mpigo lakini ndio hali ya bajeti yetu, tuchume tuingiziwe na hiyo keki yenyewe ni ndogo kwa hivyo kinachochumwa ndio tunagawana kidogo kidogo hivyo hivyo, sasa lazima akubali ile hali yetu Mheshimiwa Jaku Hashim, sisi tungependa tuingiziwe asilimia mia juu ya mia, lakini ngumu lazima tukiri ukweli wenyewe na

mwenyewe Mheshimiwa Jaku anajua huyo. Tungependa sana hivyo anavyoshauri yeye. Kwa hivyo, lazima tusaidiane sote yeye ni mchumi huyo, mfanya biashara mzuri, ana mbinu za kukuza mapato, tusaidiane tukuze mapato tuweze kwenda.

TAAFIRA

Mhe. Marina Joel Thomas: Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa naomba kuhusu Mhe. Jaku Hashim Ayoub alivyozungumza juu ya keki hiyo, lugha aliyosema Mhe. Jaku Hashim sio nzuri kumwambia Mhe. Waziri kwamba awe mama au baba kwa kweli hili ni Baraza, nasema lugha si nzuri aliyoizungumza, hili ni Baraza ambalo linasikilizwa na wananchi wengi. Kwa hivyo suala la lugha kama hizi kwa kweli haipendezi, kwa hivyo ajirekebishe haipendezi kabisa. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Kifungu 2001 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali- 1,380,000,000

Jumla ya Fungu - 3,338,900,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0201 Utawala Unguja - 815,400,000

Jumla ya Fungu- 815,400,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 1802 Tume ya Utumishi Idara Maalum- 530,000,000

Jumla ya Fungu- 530,000,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi Bila ya mabadiliko yoyote)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe katika hili buku letu imeandikwa Tume ya Utumishi Idara Maalum, ndivyo ilivyoandikwa katika hili buku, labda tusaidie zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti,Tume ya Utumishi Idara Maalum haiko kwenye Wizara hii, Idara Maalum haiko, ile Idara Maalum ndio kidogo inatupa utata.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tuondoe neno Idara Maalum, iwe Ofisi ya Rais Ikulu si ndio, unaondoa neno Idara Maalum tunaweka Ofisi ya Rais Ikulu.

Kifungu 1802

Mhe. Mwenyekiti: Jina tu limekosewa kama makosa ya kibinaadamu lakini juu inasomeka Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora. Kwa hivyo, wacha Katibu aendelee kusoma yote ili tuzidi kumfahamu.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tukafuata taratibu na sheria. Kwa sababu inawezekana mawili kitabu hiki kimekosewa na kama kimekosewa kama kuna mtu ambae anaweza akatuthibitishia lakini sisi hatuwezi tukenda vyenginevyo, tutakuwa tunakiuka sheria na taratibu zetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Kifungu 660000 usafiri na mawasiliano, kuimarisha mawasiliano Afisi ya Rais Ikulu. Sasa inawezekana pengine jina la Idara hapa ndio limekosewa katika hiki kifungu. Kwa hivyo, wanaweze kututhibitishia ni Waziri mwenyewe kifungu hiki kinakusudia nini ili tuweze kupitisha. Lakini ukisoma huku juu tutakuwa tunafanya makosa kwa sababu haya mambo yanaingia kwenye *Hansard*.

Utaratibu

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, tatizo la Baraza ukishasema na ukishafanya maamuzi yanakuwa yale ndio maamuzi yaliyokubaliwa. Mimi ushauri wangu tuahirishe japo dakika 5, kwa sababu watu wa Wizara ya Fedha wapo, watu wa Idara ya Bajeti wapo ili waje watuthibitishie. Kwa sababu ukiangalia sio kosa la hapo tu, lakini hili fungu zima limekosewa. Sasa wamekosea maneno au kuna taratibu nyengine. Na hili kwa bahati mbaya kwa sababu na mimi kwa kuwa ni kamati yangu ilipitisha Wizara hii, tatizo kwamba siku hizi utaratibu tunapitisha nje ya vitabu hivi.

Sasa makosa kama haya yanapokuja kujitokeza inakuwa kidogo ni tatizo. Kwa hivyo, mimi nadhani mara ya pili hivi vitabu tupewe mapema ili tunapopitisha mafungu ya wizara tuwe tunapitia moja kwa moja katika vitabu hivi. Sasa Mhe. Waziri naona ameletewa kimemo hapo na watendaji wake kama atakuwa hajakuwa na usahihi, basi nitaomba tuahirishe japo dakika 5 ili tupate maelezo tunachokipitisha hapa kinakuwa ndio *rubber stamp*. Ninakushukuru Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante naomba tumpe nafasi Mhe. Waziri na endapo kwamba atakuwa hakuweza kukamilisha hilo tutarejea katika utaratibu wetu wa kawaida wa Baraza tutatoa muda mdogo ili watendaji waweze kutupa maelekezo, na baadae tutaendelea na shughuli yetu.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Mhe. nikiri ni kweli kwamba hili buku limekosewa hapa lakini Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora lile fungu la 10 ni let,u hiyo ni uhakika sio kama ilivyotajwa kwenye Tume ya Utumishi ya Idara Maalum. Sasa hiki kifungu ukifungua kwenye kitabu chetu kwenye muelekeo wa kitabu cha pili imewekwa wazi kabisa na hii usafiri wa mawasiliano *transport communication* pia ni *wrong*. Lakini kifungu sahihi jina lake ni uimarishaji nyuma za viongozi na nyumba za serikali na *figure* ndio hiyo hiyo *five hundred and thirty*.

Mhe. Mwenyekiti: Tusaidie Idara gani.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora: Ndio tunarekebisha sasa hivi, Ofisi ya Rais Ikulu kwenye miradi hii.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri tunaomba kupata Idara gani? Waheshimiwa naomba turudi katika Baraza ili tuweze kuweka sawa mambo haya.

(Baraza lilirudia)

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, ni vyema tukafanya mambo yenye uhakika naomba sana Baraza lako tukufu kwamba ukurasa huo ukachapwe upya ndio utaratibu, ukachapwe upya tuletewe hasa makisio ambayo yamekusudiwa katika Ofisi ya Utawala Bora, kuliko tukipitisha hapa Mhe. Mwenyekiti, ina maana tunapitisha mambo ambayo sivyo kwa mujibu wa taratibu na sheria.

Mhe. Mahmoud Thabit Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuchangia kwa hivyo sina haki ya kuhoji vifungu, lakini naomba tu nitoe taarifa. Tulipata tatizo kama hili juzi tulipokuwa tunapitisha bajeti ya Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ambapo jina la vifungu hilo lilikuwa *traditional* tumeshazoea kuita majina kama hayo. Lakini kwenye kitabu ni tofauti. Sasa ninafikiri hili ni tatizo lile lile kwa sababu ukiangalia kwenye hotuba ya Mhe. Waziri ukurasa wa 24 na 25 ambayo inasema Ofisi ya Usalama wa Serikali *GSO* kingeangaliwa na kifungu hicho kuna *figure* zinalingana pale. Kwa hivyo jina la huku ni tofauti na jina lililokuwa kwenye hotuba Mhe. Waziri. Na hili tatizo lilitokeaea juzi pia katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Ninashukuru Mwenyekiti, naomba nitoe taarifa hiyo.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa tulipokuwa katika kikao chetu cha kamati tulikubaliana kwamba tuwape nafasi wajumbe wa Wizara ya Fedha ili waweze kutusaidia katika kuona ni namna gani tunalisawazisha suala hili. Kwa

hivyo naomba kuchukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili kwa muda wa dakika 5. Naam Mhe. Waziri una *concern* yoyote unataka kutoa?

Naomba kuliahirisha Baraza hili kwa muda wa dakika 5 ili Mhe. Waziri afanye maelekezo na watu wake baadae turejee tena.

(Saa 5.40 asubuhi Baraza Baraza liliahirishwa kwa muda wa dakika 5)

(Saa 5.45 asubuhi Baraza lilirudia)

Mhe. Mwenyekiti: Kwa kutokana na matatizo ambayo yalikuwa yamejitokeza ya kitaalamu tunaomba kumuomba Mhe. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Ikulu na Utawala Bora) ili aweze kutoa hoja ya kuliahirisha Baraza hili kwa sababu wakati wake haujafika na tuweze kuendelea na shughuli zetu jioni saa 11.00.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum: Mhe. Mwenyekiti naomba kutoa hoja kwamba kwa kuwa kuna marekebisho madogo ambayo yanatakiwa yachapishwe upya kwenye kifungu ambacho kimeleta utata, kimaandishi naomba kuliomba Baraza lako tuahirishe hadi saa 11.00 ili Ofisi ya Rais Ikulu, waweze kufanya hayo masawazisho na jioni tuje tupitishe bajeti hii.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Mwenyekiti, Naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kwa mara nyengine tena naomba kuchukua fursa hii kuliahirisha Baraza hili hadi jioni saa 11.00 barabara.

(Saa 5.50 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni barabara)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

KAMATI YA MATUMIZI

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti-	530,000,000
Jumla ya Fungu -		**530,000,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU 49 - TUME YA MIPANGO

Kifungu 1001	Idara ya Ukuzaji Uchumi-	100,000,000
Kifungu 1002	Idara ya Mipango ya Kitaifa, Maendeleo- ya Sekta na Kupunguza umasikini-	3,228,900,000
Kifungu 1003	Idara ya Mipango na Maendeleo ya Watenda Kazi-	261,925,000
Jumla ya Fungu-		**3,590,825,000**

Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha Makadirio ya Fedha ya Wizara yangu ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora pamoja na marekebisho yake sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri, Waheshimiwa Wajumbe hoja imetolewa, sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hotuba ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, wanyanyue mikono, waliokataa, waliokubali wameshinda.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2014/2015 -
Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

UTANGULIZI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma: Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Baraza ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kabla sijaendelea naomba kueleza kwa ufupi kabisa kwamba ninachowasilisha hapa ni muhtasari tu lakini maelezo kamili yako kwenye kitabu chenyewe cha hotuba na naomba yaiingizwe kwenye *Hansard*.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu mwingi wa rehma, kwa kutujaalia uzima, hekima na afya njema na kutuwezesha kutekeleza majukumu yetu ya kila siku ya kuwatumikia wananchi wenzetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, itakumbukwa kwamba mnamo tarehe 10 Januari nilipata mtihani wa kuugua ghafla na hatimae kupelekwa kwenye matibabu Afrika Kusini. Napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru *Allah* (*S.W*.) kwani yeye ndiye mwenye uwezo wa kutibu. Aidha, namshukuru sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Naibu Waziri wa Afya, Katibu Mkuu Kiongozi na Katibu wa Baraza la Mapinduzi, Katibu Mkuu Wizara ya Afya, wafanyakazi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kazi kubwa waliyoifanya na wafanyakazi wa Wizara yangu wote kwa jitihada zao na ushiri kiano wao wanaonipa.

Vile vile, naishukuru familia yangu kwa moyo wao na msaada walionipa na watu mbalimbali walionitembelea wakiwemo Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi. Shukrani maalum kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wananchi wa Jimbo la Makunduchi na Wilaya ya Kusini na Mkoa wa Kusini na wananchi wa Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, ninapenda pia kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotupatia wakati wa kupitia taarifa ya utelekezaji wa Mpango wa Bajeti ya mwa ka wa fedha 2013/2014. Na mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa mwaka 2014/2015, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha hutoba hii ya Bajeti.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza Zanzibar. Ni ukweli usiopingika kwamba, chini ya uongozi wake, Serikali imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wa Zanzibar wakati wa uchaguzi Mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchanguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yamewezesha kuendelea kukua kwa uchumi wa nchi yetu, kiasi cha kuwavutia washirika wa maendeleo kuendelea kuiunga mkono Serikali yetu na wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini.

Mhe. Naibu Spika, napenda kumpongeza Makamo wa kwanza wa Rais Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad kwa namna anavyomsaidia Rais kutekeleza shughuli mbalimbali za Umma. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema shughuli za

Serikali na utekelezaji wa shughuli hizo. Miongozo na maelekezo anayotupa yamesaidia sana katika utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia kuchukua nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Baraza letu tukufu kwa busara na hekima. Kazi nzuri unayoifanya hapa Barazani na ile uliyoifanya katika Bunge la Katiba kule Dodoma ni kielelezo tosha cha busara, hekima na uzoefu wako katika kuongoza mabaraza ya aina hii.

Aidha, nampongeza Mhe. Naibu Spika, Mhe. Ali Abdalla Ali Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini kwa kuendesha vyema shughuli za Baraza. na kwa kweli ni fahari kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuwa na hazina ya aina yako. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Baraza Mheshimiwa Mgeni Hassan Juma na Mhe. Mahamoud Muhammed Mussa wa Jimbo la Kikwajuni kwa kazi nzuri wanazozifanya.

MUELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Muelekeo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/2015 unalenga kuchangia katika ufikiaji wa malengo makuu ya Taifa ya Dira ya Maendeleo ya 2020, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar MKUZA II wa mwaka 2010-2015; Malengo ya Milenia 2015; ilani ya Uchaguzi ya 20102015;

Sera ya Utumishi wa Umma; Sera ya Serikali Mtandao; Sera ya Ajira Zanzibar na Sera nyengine husika na Mpango Mkakati wa Wizara.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi kwa mwaka 2014/2015 imepanga kuendelea kutekeleza malengo yake makuu yafuatayo:-

i. Kuongeza upatikanaji wa fursa za ajira za heshima kwa wananchi hususan vijana.

ii. Kuimarisha utekelezaji wa sheria za kazi usuluhishi na utatuzi wa migogoro ya kazini.

iii. Kuanzisha na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji rasilimali watu wenye sifa.

iv. Kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

v. Kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na Nyaraka.

vi. Kuhakikisha Wizara na Ofisi zote za umma zinafuata Miundo ya Utumishi.

vii. Kuimarisha Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na

vii. Kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 juu ya usalama na afya kazini ili kuhakikisha hali bora ya usalama na afya katika sehemu za kazi.

MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi 820,000,000. Hadi kufikia Machi 2014 Wizara yangu ilikusanya shilingi 157,975,975 sawa na asilimia 19 ya makadirio. Mapato hayo yanatokana na Vibali vya Kazi kwa Wafanyakazi wa Kigeni, Ukaguzi wa Mikataba ya Kazi na Ukaguzi wa Usalama na Afya katika sehemu za Kazi (Angalia kiambatanisho Nam. 1a)

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi iliidhinishiwa matumizi ya shilingi 7,974,489,912/= kupitia fungu 27, 47 na 48. Kati ya fedha hizo shilingi 7,274,489,912/= zilikuwa kwa matumizi ya shughuli za

kawaida ambapo, shilingi 2,80 7,205,682/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 4,467,284,230/= kwa matumizi mengineyo na shilingi 700,000,000 zilipangwa kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi Machi 2014 jumla ya shilingi 3,676,562,392/= zilitumika kwa utekelezaji wa shughuli za kawaida, ambapo shilingi 1,945,111,245/= ni malipo ya mishahara sawa na asilimia 69 ya makadirio na shilingi 1,731,451,047/= ni matumizi mengineyo sawa na asilimia 39 ya Makadirio. Kwa upande wa kazi za maendeleo shilingi 40,000,000/= zilitumika sawa na asilimia 6 ya makadirio (Angalia kiambatanisho Nam. 1b na 1c).

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2013/2014 NA MUELEKEO WA MALENGO KWA MWAKA 2014/2015 KWA KILA IDARA NA TAASISI.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa malengo na shughuli za ofisi hii unasimamiwa na Idara 10, Kitengo cha Waziri na Taasisi nne kama inavyoonekana katika ukurasa wa 6.

i. Mipango, Sera na Utafiti
ii. Uendeshaji na Utumishi
iii. Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu
iv. Mipango ya Rasilimali Watu
iv. Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,
v. Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa,
vi. Teknologia ya Habari na Mawasiliano,
vii. Ajira,
ix. Usalama na Afya Kazini na
x. Ofisi ya Ofisa Mdhamini - Pemba.

Taasisi ni;

xi. Kamisheni ya Kazi
xii. Kamisheni ya Utumishi wa Umma
xiii. Tume ya Utumishi Serikalini; na
xiv. Chuo cha Utawala wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo ya utangulizi, sasa naomba kuchukua fursa hii kutoa ufafanuzi wa mapitio ya taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rai, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na muelekeo wa malengo ya mwaka
2014/2015 kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 idara hii ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa saba.

i. Kuimarisha Mfumo wa habari na Mawasiliano wa Wizara ikiwemo kuwawezesha wananchi kuwasiliana na kupata majibu ya huduma zinazotolewa na Wizara -*"Interactive Website".*
ii. Kuandaa Mipango ya kibajeti na tathmini ya utekelezaji wake.
iii. Kuibua Programu, Miradi Mipya na Maeneo ya Utafiti.
iv. Kuratibu na kusimamia zoezi la upati kanaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.
v. Kuandaa Sera ya Malipo ya Mishahara, Sera ya Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka.
vi. Kutayarisha Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Usafiri wa Watumishi wa Umma.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa tisa.

i. Tovuti ya Wizara imesarifiwa upya kutokana na mabadiliko ya Muundo wa Wizara, jina la tovuti hiyo ni; www.lps.go.tz. Aidha, Mtandao wa mawasiliano ya komputa katika Jengo la Ofisi Kuu ya Wizara yamekamilika na unganishwaji wa Ofisi na Mkonga wa Taifa upo katika hatua za mwisho kukamilika.

ii. Mpango kazi na ripoti za utekelezaji wa majukumu ya Wizara uliandaliwa pamoja na kufanya Mapitio ya Mpango Mkakati na Mpango wa Matumizi wa Muda wa Kati kwa mwaka wa fedha 2014/2017.

iii. Maeneo mbali mbali ya utafiti yameibuliwa, maeneo hayo yatatumika kwa utayarishaji wa Mpango Mkuu wa Utafiti wa Ofisi.

iv. Ripoti ya Usarifu wa Awali wa Mfuko wa Bima ya Afya *(Design Elements of the Social Health Insurance Scheme)* imeandaliwa. Ripoti hiyo inajumuisha mapendekezo ya Makundi yatakayofaidika, Kiwango cha uchangiaji, Huduma zitakazopatikana, Kuvitambua vituo vya Afya vitakavyotoa huduma, Mfumo wa Malipo kwa watoa huduma na Mfumo wa usimamizi wa Mfuko.

v. Ripoti za tathmini ya hali halisi ya malipo na hifadhi ya kumbukumbu na Nyaraka kwa ajili ya utayarishji wa Sera ya Malipo na Sera ya uhifadhi wa kumbukumbu na Nyaraka zimekamilika.

vi. Rasimu ya Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Usafiri imeandaliwa na itawasilishwa kwa Wahusika Wengine Unguja na Pemba ili kupata maoni yao.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, idara imetumia jumla ya shilingi 83,674,965/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 58,968,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 24,706,965/= kwa matumizi mengineyo. Kwa upande wa utekelezaji wa kazi za maendeleo shilingi 12,522,900/= zimetumika. Malengo ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015.Idara imepanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa tisa.

i. Kujenga uwezo wa Idara kwa kuimarisha shughuli za mipango, ufuatiliaji na tathmini, ukusanyaji wa Takwimu na uimarishaji wa Mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
ii. Kuandaa Mpango Mkakati wa Sera ya Malipo na Sera ya Uhifadhi wa Kumbukumbu na Nyaraka.
iii. Kuandaa Mpango Mkuu wa Utafiti wa Ofisi na kuendelea na uratibu wa uanzishwaji wa Mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 156,753,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 106,753,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 50,000,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 35,000,000/= zimepangwa kutumika kwa utekelezaji wa kazi za Maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara hii ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa kumi.

i. Kuwajengea uwezo wafanyakazi 29 ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao.
ii. Kuimarisha usalama wa majengo na mazingira yanayozunguka Wizara.
iii. Kuimarisha kitengo cha utunzaji kumbukumbu na Kitengo cha Habari na Mawasiliano.
iv. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na manunuzi.
v. Kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ili kuelimisha na kujenga taswira nzuri kwa umma na kusimamia haki na upatikanaji wa maslahi ya wafanyakazi.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 20 13/2014 Idara imetekeleza malengo yake katika ukurasa wa kumi.

i. Huduma mbali mbali za kiutawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo; kuwapatia fursa za mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi Watumishi 16. Aidha, watumishi wengine 16 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu ndani na nje ya nchi (Angalia kiambatanisho Nam. 2a na 2b).
ii. Katika kuimarisha kitengo cha masjala wafanyakazi wanane wamepatiwa mafunzo juu ya utaratibu bora wa utunzaji kumbukumbu.
iii. Idara ilisimamia vikao vya Kamati ya Uongozi, Kamati Tendaji, vikao vya ukaguzi, vikao vya Bodi ya Zabuni, vikao vya kamati ya BLW na vya Washirika wa Maendeleo.
iv. Katika hatua ya kuitangaza Ofisi taarifa mbali mbali kuhusu shughuli za Wizara zimetolewa kwenye vyombo vya habari vya *ZBC TV*, *ZBC* Redio, Gazeti la Zanzibar Leo na *Hits FM*.
v. Ukarabati wa sehemu ndogo ndogo za Ofisi ulifanyika. Aidha, Idara ilisimamia maandalizi ya sherehe za miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imetumia jumla ya shilingi 818,123,887/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 600,063,648/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 218,060,239/= kwa matumizi mengineyo.

OFISI YA WAZIRI

Mhe. Naibu Spika, Ofisi ya Mheshimiwa Waziri katika mwaka 2013/2014 iliendelea na utaratibu wake wa kupokea wageni wakiwemo wananchi wa kawaida, wawakilishi wa mashirika mbali mbali ya ndani na nje ya nchi pamoja na Mabalozi. Wananchi wapatao 907 kutoka sehemu mbali mbali za Zanzibar walifika Ofisini kumuona Waziri kwa shida mbali mbali. Pia, Waziri alipata nafasi ya kukutana na kuzungumza na uongozi wa Jumuiya ya Wafanyakazi Zanzibar na viongozi wa *CHODAWU* - Zanzibar. Aidha, alipata kutembelewa na kuongea na ujumbe kutoka *ILO* na "*Save the children*" na ujumbe kutoka *Ras-Al-Khaimah*. Mabalozi waliomtembelea Mhe. Waziri katika kipindi hichi ni Balozi mdogo wa India, Balozi mdogo wa China na Oman.

Mhe. Naibu Spika, Ofisi iliratibu jumla ya shughuli 21 za kimaendeleo, ambazo Mhe. Waziri alishiriki kama mgeni rasmi, miongoni mwa shughuli hizo ni ufunguzi wa mkutano mkuu wa Jumuiya ya Wafanyakazi Zanzibar. Aidha, Mhe. Waziri amefanya ziara za kikazi na kuhudhuria mkutano katika nchi za Ras Al Khaimah, Sharja na Umarekani. Tunategemea ziara hizo zitaleta tija kwa maendeleo ya Wizara yetu na Zanzibar kwa ujumla.

Malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo kama inavyoonekana katika ukurasa wa kumi na mbili.

i. Kuwajengea uwezo watumishi 35 ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
ii. Kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya kazi yatakayorahisisha utekelezaji wa kazi za Wizara na kwa wakati.
iii. Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Manunuzi wa Wizara.
iv. Kutoa taarifa juu ya utekelezaji wa shughuli za Wizara ili kuelimisha na kujenga Taswira nzuri kwa Umma na kuhakikisha haki na maslahi ya watumishi yanapatikana kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaomba kuidhinishiwa matumizi ya shilingi 981,873,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 519,973,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 461,900,000/= kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa kada mbalimbali yanayotolewa na Nchi Wahisani.
ii. Kuandaa mafunzo mafupi kwa kada zilizo chini ya Utumishi kama vile Madereva, Wahudumu na Maafisa Utumishi.
iii. Kuandaa na kuchapisha Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya mafunzo.
iv. Kuendesha mafunzo mafupi ya Viongozi wa ngazi mbali mbali.
v. Kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma ilipanga kuratibu mafunzo mafupi ya maadili ya kazi kwa watumishi wapya Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 13.

i. Imefanya uratibu wa upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa Watumishi 116 kutoka Wizara mbali mbali nje ya Nchi. Kati ya hao, Watumishi 9 ni wa Shahada ya Pili na 107 ni wa mafunzo ya muda mfupi. Aidha, Watumishi wapya 195 wamepatiwa mafunzo ya Maadili ya Kazi katika Chuo cha Utawala wa Umma na Maafisa Utumishi 50 kutoka Taasisi za Serikali wamepatiwa mafunzo ya Uimarishaji wa Utendaji Kazi (Angalia kiambatanisho Nam. 3(a) na 3(b).
ii. Katika kuimarisha kumbukumbu za Watumishi walioko mafunzoni, Idara imetayarisha Daftari la Kumbukumbu ya Mafunzo na taarifa zimeanza kuingizwa.
iii. Imefanya tathmini juu ya ujazaji wa Mikataba ya Mafunzo. Kilichobainika ni kuwa mikataba mingi haikuidhinishwa na Wakuu wa Taasisi. Hatua zilizochukuliwa ni kuwapatia maelekezo watendaji Wakuu wa Taasisi husika ili kufuata utaratibu uliopo.
iv. Imetayarisha Rasimu ya muongozo wa tathmini ya mahitaji ya mafunzo na tayari imeshapata maoni ya Wahusika wengine kwa upande wa Pemba.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imetumia jumla ya shilingi 58,886,950/= kwa kazi za kawaida. Kati ya hizo shilingi 51,565,950/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 7,321,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 6,000,000/= zilitumika kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Malengo ya mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Idara imepanga kutekeleza malengo iliyojipangia kama inavyoonekana katika ukurasa wa 15.

i. Kusimamia na kuratibu mafunzo ya Watumishi wa Umma kwa kada mbalimbali yanayotolewa na Washirika wa Maendeleo.
ii. Kuratibu upatikanaji wa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 150 na mafunzo ya muda mrefu nje ya nchi kwa watumishi 15.
iii. Kuendeleana utafutaji wa fursa zaidi za masomo kwa Watumishi wa Umma kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ili kuongeza idadi ya wataalamu nchini.
iv. Kuandaa na kuendesha mafunzo mafupi kwa kada zilizo chini ya Utumishi pamoja na kusimamia mafunzo ya awali ya miongozo na maadili ya kazi kwa watumishi wapya watakaoingia katika utumishi wa umma.
v. Kukamilisha Sera ya mafunzo, kuichapisha na kuisambaza kwa ajili ya matumizi.
vi. Kuendesha mafunzo mafupi ya Viongozi wa Ngazi mbali mbali na kukamilisha tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya watumishi na kutoa mafunzo kwa watumiaji hususan Maafisa Mafunzo na Maafisa Utumishi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 124,362,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 89,362,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 35,000,000/= kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MIPANGO YA RASILIMALI WATU

Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 16.

i. Kupata maoni ya wahusika wengine juu ya muongozo wa Mpango wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma.
ii. Kutoa taaluma juu ya namna bora ya kutayarisha Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja kwa Taasisi zote za Umma.
iii. Kuendesha mafunzo kwa Maafisa Utumishi na Maafisa Utumishi Wasaidizi juu ya utayarishaji bora wa Ikama.
iv. Kufanya mapitio ya Ikama ya mwaka 2013/2014 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2014/2015. Idara pia ilipanga kuendesha mafunzo ya urithishaji uongozi kwa maafisa waandamizi wa Wizara 16.
v. Kukusanya taarifa za kiutumishi na kuziingiza katika mfumo wa Elekroniki - *Human Resource Data Base*.
vi. Kuandaa taarifa za kiutumishi kuanzia 1964 hadi 2014 kwa miaka 50 ya Mapinduzi pamoja na kujifunza mbinu bora za kiutumishi Kikanda na Kimataifa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Idara imetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 17.

i. Imekamilisha Rasimu ya muongozo wa Mpango wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma na kupatiwa maoni na Wahusika mbalimbali Unguja na Pemba. Aidha, Rasimu hiyo inatarajiwa kuwasilishwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu kwa kupata maoni zaidi.
ii. Imetoa mafunzo kwa maafisa Utumishi na Wasaidizi maafisa utumishi wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali juu ya utayarishaji bora wa Ikama kwa Unguja na Pemba.
iii. Imefanya Vikao 16 vya kujadili ikama na maombi 5,298 yaliwasilishwa. Kati ya hayo, maombi 2,457 yalikubaliwa, ambapo shilingi 1,598,673,120 zitahitajika katika uajiri wa nafasi hizo (Angalia kiambatanisho Nam. 4(a). Nafasi zilizoombwa kwa idadi kubwa ni kada za Ualimu, Afya, Uchumi, Uhandisi, Kilimo na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2014/2015 jumla ya Watumishi 330 wanatarajiwa kustaafu kazi kwa kufikia umri wa lazima. Katika kuimarisha utendaji kazi jumla ya watumishi 37 walifanyiwa uhamisho katika Wizara za Serikali (Angalia kiambatanisho Nam. 4(b).
iv. Imeandaa Ripoti ya miaka 50 ya Utumishi na Ripoti ya hali halisi ya Utumishi wa Umma kwa matumizi ya Serikali.
v. Imefanya uhakiki wa Majalada binafsi (*OPF*) 2,317 ya Wizara ya Afya ambapo, jumla ya watumishi 20 taarifa zao za mikataba ya kuingilia kazini haikuonekana. Watumishi 47 taarifa zao za tarehe za kuzaliwa hazikuonekana na watumishi 740 taarifa zao za kuthibitishwa kuwemo kazini hazikuonekana. Hatua zilizochukuliwa ni kuitaka Wizara husika kurekebisha kasoro hizo.Kukamilika kwa Wizara hii kumepelekea kukamilika kwa zoezi la uhakiki kwa Wizara zote 16.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imetumia jumla ya shilingi 87,564,100/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 64,961,100/= kwa malipo ya mishahara shilingi 22,603,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 10,000,000/= zilitumika kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Malengo ya mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 18.

i. Kutoa mafunzo kwa Maafisa Utumishi na Maafisa Utumishi Wasaidizi juu ya utayarishaji na utekelezaji wa mpango wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja wa Rasilimali Watu katika Utumishi wa Umma kwa Taasisi za Umma.

ii. Kuratibu utoaji wa taaluma kwa maafisa waandamizi wa Wizara 16 juu ya kuwaandaa kushika nafasi mbali mbali za uongozi katika Taasisi za Umma (*Succession Plan*).
iii. Kufanya mapitio ya Ikama (*Norminal Roll*) ya mwaka 2014/2015 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2015/2016. Idara pia itaendelea kukusanya taarifa za kiutumishi na kuziingiza katika mfumo wa *electronic* "*Human Resource Data Base*"
iv. Kushiriki katika mkutano wa kimataifa wa Utawala wa Umma na Uongozi (*AAPAM*) utakaofanyika nchini Ethiopia.

Mhe. Naibu Spika, Katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 157,669,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 107,669,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 50,000,000/= kwa matumizi mengineyo.

IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI.

Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara ilipanga kutekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 20.

i. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miundo ya utumishi kwa Wizara za Serikali na Taasisi zote za Umma.
ii. Kufanya mapitio ya mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma na kuandaa muongozo wa kufanya tathmini ya uchambuzi wa kazi na madaraja *(Job Evaluation and Grading).*
iii. Kutoa elimu kwa watendaji wa Wizara 16 kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake katika maslahi na usimamizi wa watumishi wa umma.
iv. Kukamilisha zoezi la kupitia majukumu ya Serikali na kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na mahitaji ya taasisi (*Staffing levels*).
v. Kuendelea na kazi ya kutoa taaluma ya utayarishaji wa Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Mteja kwa Wizara 11 na Taasisi zilizobakia na kufanya ufuatiliaji kwa Wizara zilizopatiwa mafunzo ya uandaaji wa mkataba huo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yake kama inavyoonekana katika ukurasa wa 21.

i. Wizara 16 zimepatiwa Miundo ya Utumishi na Wizara 8 imekaguliwa na imeonekana Watumishi wamepangiwa ajukumu yao ya kazi kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi. Wizara zilizokaguliwa ni: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Afya, Fedha, Biashara, Viwanda na Masoko, OR- Ikulu na Utawala Bora, OR- Kazi na Utumishi wa Umma, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Aidha, kazi ya kuingiza taarifa kwenye mfumo wa ulipaji mishahara inaendelea kwa Wizara tano teule.
ii. Imefanya marekebisho ya mishahara kwa watumishi wote Oktoba 2013. Aidha, Watumishi wenye uzoefu waliotumikia kuanzia miaka 15 wenye kiwango cha mshahara cha 150,000 mpaka 225,000 wamefanyiwa marekebisho.
iv. Ripoti ya Mapitio ya Kazi na Majukumu ya Serikali (*Functional Review*) imepitiwa tena na uongozi mpya wa Wizara na inatarajiwa kupelekwa kwenye kikao cha Makatibu Wakuu kwa ajili ya kupata maoni.
vi. Ufuatiliaji wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma umefanyika na tayari Rasimu za awali kwa Wizara ya Afya, Ofisi ya Raisi, Kazi na Utumishi wa Umma na Wizara ya Kilimo na Maliasili zimetayarishwa.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imetumia jumla ya shilingi 84,370,200/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 66,452,700/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 17,917,500/= kwa matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara imepanga kutekeleza malengo iliyojipangia kama inavyoonekana katika ukurasa wa 22.

i. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miundo ya Utumishi kwa Wizara za Serikali na Taasisi zote za Umma ambazo hazijakamilisha zoezi la kuwapanga watumishi wake kwa mujibu wa Miundo ya Utumishi.

ii. Kukamilisha uingizwaji wa taarifa za watumishi kwenye mfumo wa malipo ya mishahara (*Pay Roll System*).

iii. Kufanya mapitio ya mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma na kukamilisha muongozo wa kufanya tathmini ya uchambuzi wa kazi na madaraja (*Job Evaluation and Grading*).

iv. Kutoa elimu kwa watendaji wa Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu Kanuni za Utumishi wa Umma iIi kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu pamoja na kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na mahitaji ya taasisi (*Staffing Levels*).

vii. Kuendelea na kazi ya kutoa taaluma ya utayarishaji wa Mkataba wa utoaji huduma kwa mteja kwa Wizara 12 na Taasisi zilizobakia na kufanya ufuatiliaji kwa Wizara zilizopatiwa mafunzo ya uandaaji wa mkataba.

vi. Kufanya ziara nje ya nchi kwa madhumuni ya kuwajengea uwezo maafisa kuhusu mambo mbali mbali ya kiutumishi.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 162,286,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 112,286,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 50,000,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 35,000,000, kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 35,000,000 zimepangwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutayarisha mfumo wa uhifadhi wa Nyaraka kwa njia ya elektroniki.
ii. Kutayarisha mgawanyo wa majalada (*File Classification*) na Daftari la Uhai wa kumbukumbu (*Retention Schedule*) kulingana na majukumu ya msingi ya wizara, idara, mashirika na taasisi za umma.
iii. Kuimarisha ulinzi na usalama wa Nyaraka na Kumbukumbu.
iv. Kununua Mtambo wa *CCTV* pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo.
v. Kuimarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu pamoja na kutoa mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa kumbukumbu kwa wafanyakazi wa masjala na wasimamizi wa kumbukumbu kwa Wizara 11 zilizobakia.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Imefanya uhuwishaji wa Nyaraka 90 chakavu zilizokuwa katika hatari ya kuharibika (Angalia kiambatanisho Nam. 5(a)**)**. Aidha, watafiti 478 walihudumiwa kati ya hao watanzania ni 422 na 56 ni wageni kutoka nchi za nje (Angalia kiambatanisho Nam. 5(b)).
ii. Imeimarisha mfumo wa hewa katika sehemu za kuhifadhia Nyaraka, ambapo vipoza hewa (*A/C*) viwili vya tani 2 vimenunuliwa na vitatu vimefanyiwa matengenezo.

iii. Huduma za kiutawala na uendeshaji zimetolewa ikiwemo; kuwapatia Watumishi Stahiki zao, kufanya ununuzi wa vifaa mbali mbali vya ofisi na matengenenzo madogo madogo ya Ofisi.
iv. Imefanya matengenezo ya mfumo mzima wa upatikanaji wa maji katika jengo la idara ili kuimarisha upatikanaji wa huduma hio.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Idara imetumia jumla ya shilingi 123,963,989/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 108,794,754/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 15,169,235/=kwa matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

45. Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutayarisha mfumo wa uhifadhi wa Nyaraka kwa njia ya elektroniki.
ii. Kuendelea na kazi ya mgawanyo wa majalada (*File Classification*) na daftari la uhai wa kumbukumbu (*Retention Schedule*) kulingana na majukumu ya msingi ya Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma.
iii. Kuimarisha Mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu, kutoa mafunzo ya Mfumo wa Usimamizi wa Kumbukumbu kwa wafanyakazi wa Masjala na wasimamizi wa kumbukumbu kwa Wizara 11 zilizobakia.
iv. Kufanya ukaguzi wa kumbukumbu na Nyaraka katika Taasisi za Umma.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/2015 idara inatarajia kutumia jumla ya shilingi 375,659,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 198,159,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 177,500,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 125,000,000/= zimepangwa kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara ilipanga kutekeleza malengo yake yafuatayo:-

i. Kuandaa Miongozo na viwango vya kiusalama kwa matumizi ya mifumo na vifaa vya kompyuta – (*Guidelines and Standards of Computer Program and Devices*).
ii. Kuimarisha mfumo wa umeme uliopo, kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa idara, kutoa elimu kwa viongozi wa serikali, viongozi wa siasa, viongozi wengine wa kijamii, Watu wenye mahitaji maalumu, na wananchi juu ya dhana nzima ya Serikali Mtandao.
iii. Kufanya upembuzi yakinifu juu ya utayari wa serikali pamoja na wananchi juu ya matumizi ya huduma za kijamii zitakazotolewa na kupatikana katika mfumo wa kompyuta (*E-services*).
iv. Kushirikiana na wahusika wengine kuhakikisha Taasisi zote za Serikali zinaunganishwa katika kituo cha Serikali Mtandao na kujenga vituo vya huduma za kijamii (*Community centre*) mijini na vijijini.
v. Kushiriki katika semina, makongamano na Mikutano ya Kitaifa na Kimataifa ya Mashirikiano ya uimarishaji wa huduma za Serikali Mtandao.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Jumla ya Watumishi wanne wamepata mafunzo ya kujenga uwezo nchini Tanzania Bara, Japan, Singapore na China na watumishi wote wa Idara walipatiwa mafunzo ya matumizi ya vifaa vya ulinzi na usalama na namna bora ya kupambana na majanga.
ii. Vikao 14 vimeratibiwa 12 vya kamati ya ufundi na viwili vya Kamati ya Usimamizi.

iii. Sera ya *E-Government* imetafsiriwa kwa lugha ya kiswahili na maoni kuhusiana na Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Sera ya Serikali Mtandao kwa upande wa Unguja na Pemba yamekusanywa na tayari yameshafanyiwa kazi.

iv. Katika uimarishaji wa huduma za kimtandao Taasisi saba za Serikali zimeunganishwa kimawasiliano na Mkonga wa Taifa. Aidha, uunganishwaji wa Taasisi zilizobakia utakamilika katika mwaka huu wa bajeti.

v. Mafunzo ya "*Configuration*" ya vifaa (*cyberoam -27 na Juniper switch-27*) ambavyo vinatumika katika uunganishaji wa Mkonga wa Taifa na Taasisi za Serikali yametolewa kwa maafisa 30 wa *ICT* wa taasisi hizo. Aidha, mafunzo maalum (*Advanced Configuration*) yametolewa kwa maafisa 8 wa idara ili kuwawezesha kusimamia uendeshaji na matumizi ya taarifa za kimtandao kwa ajili ya kuepusha matumizi mabaya ya taarifa.

vi. Katika kuwajengea uelewa Maafisa Wadhamini, Wakuu wa Mikoa Pemba na Wakuu wa Taasisi zote Unguja, wamepatiwa mafunzo ya siku moja juu ya kukuza uelewa na kuzitambua huduma za kimtandao ambazo taasisi zao zinaweza kuanzisha na kuwafikia wananchi kwa urahisi.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, idara imetumia shilingi 199,342,096/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 146,644,100/= zilitumika kwa malipo ya mishahara na shilingi 52,697,996/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 11,983,500/= zilitumika. kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutoa miongozo itakayowezesha Taasisi za Serikali kuwasiliana kwa mfumo wa data na sauti. Mfumo huu utarahisisha mawasiliano baina ya Taasisi za Serikali na kupunguza gharama za simu.

ii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake ili kuwajengea uwezo kulingana na ukuaji wa teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

iii. Katika kuzitangaza huduma za Kielektroniki, idara imepanga kutayarisha vipindi vya elimu kwa wananchi na kuvirusha hewani kwa kupitia vyombo vya habari (Televisheni na Redio) na kufanya ziara katika wizara kumi na sita Unguja na Pemba.

iv. Kuanzisha "*domain*" ya Serikali ili iweze kutumika katika tovuti ya Serikali, barua pepe za wafanyakazi wa Serikali na huduma za kielektroniki (*E-services*).

v. Kufanya mapitio ya Sheria ya *"Evidence Act* na *Criminal Proceeding Act"* na kuanzisha Sheria zitakazosimamia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, sheria hizo ni; "*Cyber Crime Act*" na "*Data Protection Act*".

vi. Kuhamisha mfumo wa kumbukumbu za wafanyakazi na mfumo wa malipo ya mishahara ya wafanyakazi (*Pay Roll*) na kuziweka katika kituo kikuu cha Mfumo wa taarifa (*Data Centre*).

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 700,880,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 231,880,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 469,000,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 90,000,000/= zimepangwa kutumika kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA AJIRA

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira.

ii. Kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi.

iii. Kushajihisha jamii kuhusu masuala ya ajira kwa vijana.

iv. kukamilisha utaratibu wa kurasimisha sekta isiyo rasmi ya usafirishaji kwa kushirikiana na taasisi nyengine zinazohusika.

v. Kuimarisha mashirikiano na sekta binafsi na nchi washirika katika ukuzaji wa ajira.
vi. Kuimarisha mtandao wa mashirikiano na washirika mbali mbali juu ya masuala ya ajira na kuimarisha uwezo wa Idara ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, idara imetumia jumla ya Shilingi 8,977,460/= kwa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Imewapatia Vijana 410 fursa ya kufanya kazi kupitia Kampuni ya Danaos. Vijana 859 wamepata nafasi za kazi nje ya nchi katika nchi za Djibout, Oman, Qatar, Saudi Arabia, *U.A.E* na Yemen kupitia Mawakala Binafsi wa Ajira. Vijana 340 wameripotiwa kuajiriwa katika sekta binafsi ya Hoteli. Vijana 76 wanaotafuta kazi wamesajiliwa kwa ajili ya kuwaunganisha na waajiri (Angalia kiambatanisho Nam. 6(a), (b) na (c).
ii. Vipindi vitatu vya redio na viwili vya *TV* vimerushwa hewani kupitia *ZBC TV* na Redio na *Bomba FM*. Vipindi hivyo vilizungumzia juu ya upatikanaji na utaratibu wa ajira za nje ya nchi.
iii. Ziara za ufuatiliaji zimefanyika kwa Wilaya ya Mkoani na Chake Chake, Wilaya hizi zimesaidia kuzalisha ajira 112 kupitia nafasi za biashara katika Soko la Chake Chake.
iv. Ukaguzi umefanyika kwa Taasisi 7 za Wakala Binafsi wa Ajira zilizopo na imeonekana zinafanya kazi zao kwa mujibu wa sheria na kanuni za kazi. Taasisi 2 zilizoomba leseni zimekaguliwa ambazo ni *Blue Agency* na *Hijra Man Power Agency*, kati ya hizo moja imeshapatiwa leseni na nyengine inaendelea kukamilisha utaratibu.

Malengo ya Mwaka 2014/15

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji na uwekaji wa taarifa za soko la ajira.
ii. Kuimarisha shughuli za ukuzaji wa ajira nchini.
iii. Kuimarisha mashirikiano baina ya Serikali na Sekta Binafsi katika masuala ya kukuza ajira nchini na kuimarisha kiutendaji Idara ya Ajira.
iv. Kuzalisha ajira zipatazo 2,000 kwa vijana kwa kushirikiana na sekta binafsi.
v. Kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Ajira kwa Vijana.
vi. Kukamilisha utayarishaji na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mafunzo Kazini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi126,204,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 81,204,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 45,000,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 43,000,000/= zitatumika kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo. Pia Idara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi 15,000,000/=.

IDARA YA USALAMA NA AFYA KAZINI

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini, kukuza uelewa wa waajiri, wafanyakazi na jamii kwa jumla juu ya Sheria Nambari 8 ya Usalama na Afya Kazini ya mwaka 2005.
ii. Kusimamia sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa zinafuata na kutekeleza Sheria, Kanuni na Miongozo ya Usalama na Afya Kazini na kuimarisha mashirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini.
iii. Kuimarisha uwezo wa Idara ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo kitaaluma na vifaa.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Sehemu za kazi 180 zimekaguliwa na miongozo imetolewa kwa waajiri na waajiriwa juu ya umuhimu wa kuweka mazingira bora ya Usalama na Afya Kazini.
ii. Wakaguzi wawili kutoka Unguja na mmoja kutoka Pemba walishiriki katika Mkutano uliofanyika Tanzania Bara kuhusiana na ukaguzi kwenye sekta ya mafuta na gesi ambapo, wakaguzi hao walipata fursa ya kuongeza uelewa juu ya masuala hayo. Mafunzo ya Usalama na Afya Kazini yametolewa Pemba kwa watendaji 40 wa serikali na taasisi 50 za binafsi Unguja na Pemba.
iii. Ukaguzi kwa ajili ya Usajili umefanyika kwa sehemu 140 za kazi. Mfanyakazi mmoja mwanamke amepatiwa mafunzo ya Shahada ya Pili kuhusiana na masuala ya usalama na afya kazini nchini Italy.
iv. Vipindi 13 vya Radio na kimoja cha Televisheni vimetayariswa na kurushwa hewani kupitia *ZBC*, *Hits FM* na *Bomba FM*.
v. Mikutano miwili ya kamati ya Afya na Usalama kazini na Mkutano mmoja wa mashirikiano na taasisi nyengine zinazohusika na Usalama na Afya Kazini imefanyika. Mikutano hiyo imewezesha kujenga mashirikiano na taasisi nyengine ambazo majukumu yake yanalingana na majukumu ya Idara ya Usalama na Afya Kazini. Aidha, ziara 2 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Idara Pemba zimefanyika.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, idara imetumia Shilingi 41,472,000/= kwa kazi za kawaida na kukusanya Shilingi 18,336,000/=.

Malengo ya Mwaka 2014/15

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kusimamia utekelezaji wa Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini kwa kufanya ukaguzi katika maeneo 180 na kusajili taasisi 140.
ii. Kusimamia sehemu za kazi ili kuhakikisha kuwa zinafuata na kutekeleza Sheria, Kanuni na miongozo ya Usalama na Afya Kazini.
iii. Kuimarisha uwezo wa Idara ya Usalama na Afya Kazini ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.
iv. Kuimarisha ushirikiano na uratibu wa masuala ya usalama na afya kazini na kukuza uelewa kwa waajiri, wafanyakazi na jamii juu ya Sheria Nambari 8 ya mwaka 2005 ya Usalama na Afya Kazini.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, idara inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 126,235,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 81,235,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 45,000,000/= kwa matumizi mengineyo. Idara pia inatarajia kukusanya shilingi 25,000,000/=.

OFISI KUU PEMBA

Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ofisi ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu warsha ya kujadili na kupata maoni juu ya muongozo wa Mpango wa Rasilimali Watu, kuratibu warsha ya kutoa taaluma juu ya namna bora ya kutayarisha Mpango wa Rasilimali Watu (miaka mitano na mwaka mmoja mmoja), kuratibu mafunzo ya urithishaji Uongozi kwa Wizara zote 16 na kuratibu mafunzo kwa maafisa Utumishi juu ya utayarishaji bora wa Ikama.
ii. Kuendelea na kazi za uhifadhi wa kumbukumbu kwa njia ya elektroniki.

iii. Kufanya mgawanyo wa Majalada na Daftari la Uhai wa kumbukumbu kulingana na majukumu ya msingi ya wizara, idara na Taasisi za Serikali.

iv. Kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miundo ya Utumishi, kuratibu Mafunzo juu ya matumizi ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake kwa Wizara 5, kuimarisha huduma za kiutawala na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

v. Kuanzisha kitengo cha usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi, kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa Sheria za kazi na kuwajengea uwezo vijana 200 kwa kuwabadilisha mtazamo ili kupenda kazi na kuacha tabia ya kuchagua kazi.

vi. Kuratibu mkutano mmoja wa mashirikiano baina ya waajiri, wakala binafsi, na Taasisi zisizo za kiserikali kuhusu masuala ya ajira, kuratibu mafunzo ya usalama na afya katika sehemu za kazi kwa Taasisi za Umma na Taasisi Binafsi, kuratibu mafunzo kwa watendaji wakuu wa Serikali juu ya usalama na afya kazini.

vii. Kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu 60 za kazi na uchunguzi wa matukio (ajali na maradhi) na kufanya ukaguzi maalumu na kusajili sehemu 40 za kazi.

Utekelezaji wa Malengo ya 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, ofisi imetekeleza malengo kama ifuatavyo:-

i. Mkutano wa siku moja wa kujadili Mpango wa miaka mitano wa Rasilimali Watu, ulifanyika na kuwashirikisha Maafisa Wadhamini, Maafisa Tawala wa Mikoa na Wilaya, watendaji wa mahkama na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka.

ii. Imetoa mafunzo ya kujenga uelewa wa Sheria ya Utumishi wa Umma namb. 2 ya mwaka 2011. Mafunzo hayo yaliwashirikisha wafanyakazi wafuatao; Muangalizi wa Ofisi, Katibu Muhtasi, Kalamazuu,Mtunza Kumbukumbu, Walinzi, Tarishi na Dereva kutoka katika wizara 10.

iii. Imefanya ukaguzi kazi kwa Taasisi 30 binafsi. Pia Ofisi imepokea malalamiko kuhusu mishahara na likizo kutoka kwa wafanyakazi wa taasisi mbali mbali za binafsi zikiwemo *Serengeti Company Ltd*, *Hifadhi Hotel & Conference na H-young Company Ltd* na tayari yamefanyiwa usuluhishi.

iv. Imetoa mafunzo juu ya muongozo wa utayarishaji Mkataba wa utoaji huduma kwa mteja, ambayo yaliwashirikisha Waratibu wa Maidara kutoka wizara 5 ambazo ni:- Wizara ya Afya; Wizara ya Kilimo na Maliasili; Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano; Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma.

v. Ofisi pia iliratibu mafunzo ya siku moja kwa Maafisa Utumishi wa Wizara 16 na Idara zinazojitegemea juu ya utayarishaji bora wa Ikama (*Nominal Roll*). Ufuatiliaji umefanywa kwa Wizara na Taasisi zote za Serikali ili kuona kwamba zoezi la utayarishaji wa Ikama linafanywa ipasavyo. Aidha, ukusanyaji wa taarifa za wafanyakazi wapya umefanyika kwa Wizara 15 na zinaendelea kuingizwa katika "*Data Base*".

vi. Ofisi inaendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi wake kielimu, ambapo, jumla ya wafanyakazi 12 wanaendelea na masomo yao ya muda mrefu katika fani na ngazi mbalimbali.

vii. Matayarisho ya uanzishwaji wa Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Kazi (*DHU*) yanaendelea ambapo vitendea kazi mbali mbali vimenunuliwa.

viii. Imetoa mafunzo ya siku mbili ya kuwaelimisha vijana juu ya kupenda kazi na kuacha tabia ya kuchagua kazi kwa vijana 62 katika Wilaya ya Chake Chake na vijana 50 katika Wilaya ya Wete.

ix. Ukaguzi wa Usalama na afya kazini umefanyika kwa taasisi 45 za kazi. Baadhi ya mambo yaliyobainika ni kupungua kwa matukio ya ajali na maradhi kutokana na matumizi ya vifaa bora vya kinga. Aidha, taasisi 24 za kazi zimekaguliwa na kupatiwa hati za usajili. Ofisi iliratibu mkutano uliozungumzia masuala ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi kwa watendaji wakuu wa serikali.

x. Mafunzo ya siku moja juu ya uwekaji na utunzaji wa Kumbukumbu kwa Maafisa Wadhamini na watunza Kumbukumbu wa wizara zilizomo katika mfumo mpya wa utunzaji kumbukumbu yametolewa.

xi. Tathmini ya kumbukumbu imefanywa katika Wizara ya Kilimo na Maliasili, na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Jumla ya majalada 86 yameonekana yanafaa, hivyo yatahamishiwa Ofisi ya Nyaraka na majalada 3,320 yasiyofaa yanategemewa kuharibiwa.

xii. Jumla ya wageni 38 walitembelea Ofisi ya Nyaraka na kupatiwa huduma ambapo wanne ni kutoka nje ya nchi na 34 ni wanafunzi kutoka Skuli ya Konde.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014 Ofisi Kuu Pemba imetumia jumla ya shilingi 301,606,050/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 205,606,350/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 95,999,700/= kwa matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, ofisi imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuratibu mafunzo kwa Maafisa Utumishi wa Wizara zote 16 juu ya utayarishaji wa mpango wa miaka mitano wa Rasilimali watu na kushiriki katika vikao 16 vya kujadili *Nominal roll*.
ii. Kuratibu mafunzo ya utayarishaji wa Mpango wa Urithishaji Uongozi (*Succession Plan*)
iii. Kutoa mafunzo ya Usalama na Afya katika sehemu za kazi kwa Taasisi 40 binafsi na Taasisi 40 za Umma.
iv. Kufanya ukaguzi wa usalama na afya katika sehemu 60 za kazi na kufanya uchunguzi wa ajali na maradhi katika sehemu za kazi.
v. Kuendelea kufanya ukaguzi maalumu na kusajili sehemu 40 za kazi, kuratibu mkutano wa ushirikiano ya masuala ya Usalama na Afya Kazini.
vi. Kuratibu mafunzo juu ya kuongeza ufanisi (*Perfomance Improvement*) kwa maafisa Utumishi na maafisa wa masjala na mafunzo juu ya Mpango wa utekelezaji wa Sera ya Mafunzo.
vii. Kuendelea kuwalipia watumishi gharama za masomo pamoja na kutoa huduma za kiutawala na uendeshaji kwa ofisi.
viii. Kufanya ukaguzi wa utunzaji na utumiaji (*Baseline Survey*) wa kumbukumbu katika Taasisi tatu za Serikali na kuondosha mlundikano wa kumbukumbu mfu (*Decongestion*).
ix. Kuandaa mkutano kwa wakuu wa taasisi na maafisa wa Masjala kwa taasisi tatu zitakazofanyiwa ukaguzi na kuimarisha mfumo wa upozaji hewa katika Jengo la Nyaraka Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Ofisi kuu Pemba inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 427,035,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 311,535,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 115,500,000/= kwa matumizi mengineyo.

KAMISHENI YA KAZI

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamisheni ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba minane ya Kimataifa inayohusu masuala ya kazi pamoja na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*).
ii. Kukuza uelewa wa Sheria za kazi kwa jamii na kuimarisha usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya kazi.
iii. Kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja katika sehemu za kazi, kuendeleza mashirikiano ya Kikanda, Kitaifa na Kimataifa katika masuala yanayohusu sekta ya kazi.
iv. Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kamisheni imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Ukaguzi umefanywa kwa Taasisi 243 na miongoni mwa yaliyobainika ni pamoja na kuongezeka kwa uelewa juu ya sheria za kazi na kuimarika kwa uhusiano kati ya waajiri na waajiriwa.
ii. Mkutano wa kuandaa taarifa za utekelezaji wa mikataba ya Kimataifa na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*) umefanyika na taarifa hizo zilipitiwa na wahusika mbali mbali hapa Zanzibar.
iii. Watendaji wawili wa Kamisheni wameshiriki katika kuandaa taarifa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*). Taarifa hiyo imeshawasiliswa Makao Makuu ya Shirika la Kazi Duniani (*ILO*).

iv. Mikutano miwili ya Bodi ya Ushauri wa Mambo ya Kazi na mikutano miwili ya Kamati ya Utatu imefanyika.
v. Kamisheni imesajili Shirikisho la Vyama vitatu (*ZAPSU*) na Chama kimoja cha Mabaharia cha ZAMAWU ili kuimarisha majadiliano ya pamoja kazini.
vi. Katika upunguzaji wa ajira mbaya za watoto jumla ya watoto 631 wametolewa katika ajira mbaya na kurejeshwa skuli na kupatiwa vifaa vya masomo.

Mhe. Naibu Spika, Hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, kamisheni imetumia jumla ya shilingi 19,001,000/= na kukusanya mapato ya shilingi 139,242,375/=.

Malengo ya Kamisheni ya Kazi kwa Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kamisheni imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kufanya ukaguzi kwa taasisi 240 za kazi ili kuhakikisha zinatekeleza ipasavyo Sheria na Sera za kazi.
ii. Kuimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikataba 8 ya msingi ya kimataifa inayohusu masuala ya kazi pamoja na mapendekezo ya Shirika la Kazi Duniani.
iii. Kuimarisha Mfumo wa Usuluhishi na Uamuzi wa migogoro ya kazi, kuimarisha uhusiano na majadiliano ya pamoja ya sehemu za kazi.
iv. Kuendeleza mashirikiano ya kazi Kikanda, Kitaifa na Kimataifa yanayohusu Sekta ya Kazi.
v. Kuimarisha utekelezaji wa Mpango wa Kupambana na Ajira Mbaya za Watoto.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kamisheni inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 286,444,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 181,944,000/= ni mishahara na shilingi 104,500,000/= kwa matumizi mengineyo. Aidha, kamisheni inatarajia kukusanya mapato ya shilingi 211,000,000/=.

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, kamisheni ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa na kuratibu mikutano 15 na ziara 15 kwa ajili ya kushughulikia na kutoa maamuzi ya masuala ya miundo ya utumishi, miundo ya taasisi,
ii. Kufanya uchunguzi na ukaguzi wa rasilimali watu kwa Waajiri, mamlaka za ajira na nidhamu kwa lengo la kufuatilia uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa rasilimali watu katika utumishi wa umma.
iii. Kuandaa, kuchapisha na kusambaza miongozo ya masuala ya ajira, nidhamu na uzingatiaji wa sheria, Kanuni, na maadili ya utumishi wa umma.
iv. Kuelimisha na kuongeza uelewa wa Watendaji Wakuu wa taasisi za umma kuhusu sheria, Kanuni, taratibu na maadili ya utumishi wa umma, kupitia semina, warsha na makongamano.
v. Kamisheni ilipanga kutayarisha na kuwasilisha ripoti ya hali halisi ya utumishi wa umma itakayowasilishwa kwa Rais kupitia kwa Waziri anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma.
vi. Kuimarisha mazingira ya kazi na kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi 30 wa Kamisheni katika ngazi tofauti.

Utekelezaji wa Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Kamisheni imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Ilifanya Mikutano 22 iliyojadili na kutoa uamuzi kuhusu masuala mbali mbali katika Utumishi wa Umma na kuidhinisha Miundo ya Utumishi mitatu ambayo ni ya Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Idara ya Mahkama.

ii. Imechapisha na kusambaza nakala 3,000 za Muongozo kuhusu Uchunguzi na Ukaguzi wa Rasilimali watu na Muongozo wa utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma kwa wahusika wakuu wa Utumishi wa Umma. Semina tatu za kujenga uelewa juu ya Miongozo hiyo kwa Maofisa Utumishi 200 kutoka wizara, idara zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zimefanyika kwa upande wa Unguja.

iii. Ilipokea rufaa 7 ambazo zilifanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi ambapo rufaa moja ilikubaliwa na mtumishi kurejeshwa kazini na rufaa 6 zilikataliwa kutokana na Kamisheni kutoridhika na madai yao (Angalia kiambatanisho Nam. 7a). Aidha, Kamisheni ilipokea Malalamiko matano (5) ambayo yalifanyiwa uchambuzi na kutolewa uamuzi (Angalia kiambatanisho Nam. 7b).

iv. Katika kujenga uwezo wa Kamisheni, Makamishna watatu na Maofisa wawili wa Sekretarieti walipatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa Utumishi wa Umma nchini India na Kamishna mmoja na Maofisa wawili wa Sekretarieti walihudhuria Mkutano wa 35 wa mwaka wa Jumuiya ya Kiafrika ya Utumishi wa Umma na Uendeshaji (*AAPAM*) nchini Rwanda. Maofisa wote wa Sekreterieti ya Kamisheni walipatiwa Mafunzo Maalum kuhusu Miundo ya Utumishi na Miundo ya Mishahara yaliyoratibiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, Kamisheni imetumia jumla ya shilingi 368,170,677/= kwa matumizi ya kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 168,815,950/= ni kwa malipo ya mishahara na shilingi 199,354,727/= kwa matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, kamisheni imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kutoa ushauri kwa Mheshimiwa Rais kuhusu masuala mbali mbali ya kiutumishi ikiwemo uteuzi wa Watendaji Wakuu na Mishahara ya Watumishi wa Umma, kuwezesha na kusimamia Tume za Utumishi, Bodi za Wakurugenzi za Mashirika ya Umma na Wakala wa Serikali kufikia utawala unaolenga matokeo bora.

ii. Kufuatilia na kutathmini usimamizi wa Watendaji Wakuu wa taasisi za umma kwa kufanya Uchunguzi na Ukaguzi wa Kawaida na Ukaguzi wa Kushitukizia kuhusu usimamizi wa Rasilimali watu katika Utumishi wa Umma.

iii. Kupokea na kushughulikia Rufaa na Malalamiko dhidi ya maamuzi yaliyotolewa na Mamlaka za Ajira na Mamlaka za Nidhamu katika Utumishi wa Umma kadiri yatavyopokelewa.

iv. Kamisheni pia imepanga kushughulikia na kuidhinisha Mapendekezo ya Miundo ya Utumishi, Miundo ya Taasisi na Miundo ya Mishahara kadiri yatavyopokelewa.

v. Kuandaa na kufanya ziara 15 na mikutano 15 kwa ajili ya kujadili na kutoa maamuzi kuhusu masuala mbali mbali ya kiutumishi.

vi. Kuandaa Muongozo kuhusu Ukaguzi wa Afya na Usalama Kazini katika Utumishi wa Umma na Muongozo kuhusu Mashauri ya Nidhamu na Rufaa katika Utumishi wa Umma.

vii. Kamisheni imepanga kuchapisha, kusambaza na kutoa Elimu na Ufafanuzi juu ya Miongozo hiyo. Vile vile,

viii. Kuendelea kutoa elimu na ufafanuzi wa Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake kwa Watumishi wa Umma kupitia Mikutano ya Kazi, Warsha na Semina.

Mhe. Naibu Spika, Kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Kamisheni inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 853,700,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 267,300,600/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 586,399,400/= kwa matumizi mengineyo.

TUME YA UTUMISHI SERIKALINI

Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Tume ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, ambapo ajira 1,419 zilitegemewa kutangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini,
ii. Kuendelea kusimamia haki za wafanyakazi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza za muda wa utumishi.
iii. Kusikiliza rufaa za wafanyakazi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na mamlaka za nidhamu, kutoa ruhusa za likizo bila ya malipo, uajiri wa mkataba, kuthibitishwa kazi, kubadilishwa kada na kustaafu kisheria.
iv. Tume pia imepanga kuandaa muongozo wa upandishwaji vyeo kwa watumishi Serikalini.
v. Kutoa elimu juu ya suala la ajira Serikalini.
vi. Kuimarisha huduma za kiutawala na za kiuendeshaji na kuwapatia mafunzo wafanyakazi wake watatu katika ngazi ya Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, tume imetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Nafasi za ajira 568 zilipokelewa na zilitangazwa kupitia *ZBC* Redio na TV. Usaili kwa nafasi 568 za ajira ulifanyika Unguja na Pemba na kibali cha ajira kwa nafasi hizo kilitolewa (Angalia kiambatanisho Nam. 8a).

ii. Malalamiko 3 yaliwasilishwa na kufanyiwa kazi na Wafanyakazi 19 wameongezwa muda wa utumishi. Aidha, Tume imeidhinisha ajira ya mkataba kwa wafanyakazi 9. Ruhusa ya likizo bila ya malipo kwa wafanyakazi 33 imetolewa. Makosa ya kinidhamu 4 yamewasilishwa na kujadiliwa, kati ya hayo 2 tayari yameshatolewa maamuzi ambapo mfanyakazi mmoja amerejeshwa kazini na mmoja amefukuzwa kazi (Angalia kiambatanisho Nam. 8b).
iii. Rasimu ya awali ya muongozo wa upandishwaji vyeo imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa kwa wahusika wengine kwa ajili ya kutoa maoni.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, tume imetumia jumla ya shilingi 288,366,100/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 71,630,100/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 216,736,000/= ni matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, Tume imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuandaa na kusimamia shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, ambapo ajira 1,862 zinategemewa kutangazwa na Tume ya Utumishi Serikalini. Sambamba na hilo,
ii. Kuendelea kusimamia haki na nidhamu za Wafanyakazi wa Serikali ikiwa ni pamoja na kutoa nyongeza za muda wa utumishi, kusikiliza rufaa za wafanyakazi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume.
iii. Kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kufukuza kazi kwa watumishi watakaothibitika kwenda kinyume na taratibu za kazi, likizo bila ya malipo na kustaafisha kisheria Watumishi wa Serikali.
iv. Kujenga uelewa juu ya Muongozo wa Upandishwaji Vyeo kwa Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi na Maafisa Utumishi wa Wizara na Taasisi za Serikali. Vile vile, Kutoa elimu juu ya Sheria ya Utumishi wa Umma No. 2 ya mwaka 2011 na Kanuni zake.
v. Kuimarisha huduma za kiutawala na za kiuendeshaji na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wawili na mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi wawili.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Tume inaomba idhini ya matumizi ya shilingi 510,900,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 117,300,000/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 393,600,000/= kwa matumizi mengineyo.

CHUO CHA UTAWALA WA UMMA

Malengo ya Mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, chuo kilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kutoa nafasi zaidi kwa watumishi wa umma kujiunga na chuo kwa mafunzo ya kukuza uwelewa pamoja na mafunzo mafupi ya kujenga uwezo katika kada za utumishi.

ii. Kuandaa mafunzo ya kujenga uwezo kwa watumishi wapya wanaojiunga na Utumishi wa Umma pamoja na watumishi wanaokaribia umri wa kustaafu kwa kushirikiana na Idara ya Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali Watu.

iii. Kuajiri wakufunzi wapya wanane pamoja na wahudumu wawili.

iv. Kutayarisha mapendekezo ya mradi wa ujenzi wa Chuo cha Utawala wa Umma kwa ajili ya kuutangaza na kuutafutia wafadhili, kufanya ziara za kubadilishana uzoefu na kutafuta nafasi zaidi za kuwajengea uwezo wakufunzi wa Chuo.

v. Kuwadhamini wakufunzi wawili kwa ajili ya mafunzo ya shahada ya uzamili nchini, kufanya ununuzi wa majoho 100 kwa ajili ya wahitimu wa Chuo. Kuendelea na zoezi la kuipitia mitaala pamoja na kununua vitendea kazi vikiwemo vitabu rejea, *LCD projector* na Kompyuta.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, chuo kimetekeleza malengo yafuatayo:-

i. Watumishi wa Umma 263 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi ya Msingi, Cheti na Stashahada. Watumishi wapya 195 kutoka taasisi mbali mbali za Serikali Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo juu ya maadili ya kazi. Aidha, watumishi 12 wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar wamepatiwa mafunzo mafupi juu ya maadili ya utumishi na utunzaji siri.

ii. Mitaala 2 ya Stashahada ya Uhazili na Stashahada ya Rasilimali Watu imepitiwa na kufanyiwa marekebisho. Mitaala ya mafunzo ya *"Public Service Management"* na *"Public Relation"* imeandaliwa na mafunzo yameanza kutolewa. Mitihani ya muhula wa Julai – Disemba 2013 imefanyika ambapo, watahiniwa 2,567 walifanya mitihani hiyo.

iii. Ziara nane za kimasomo na kubadilishana uzoefu zilifanyika Tanzania Bara. Ziara moja ilifanyika nchini Uholanzi ambapo wakufunzi 3, Mkurugenzi na Mwanasheria walihudhuria.

iv. Ripoti ya hali halisi ya tathimini ya uwezo wa Chuo imeandaliwa na kuwasilishwa *NACTE* kwa ajili ya kupata "*Accreditation*".

v. Huduma mbali mbali za kiutawala na uendeshaji zimetolewa ikiwemo ununuzi wa Kompyuta 14 na printa 4, na majoho 140. Sherehe ya mahafali ya 6 ilifanyika ambapo jumla ya wahitimu 1,463 walitunukiwa vyeti katika ngazi ya Cheti na Stashahada kati ya hao 520 ni Watumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, hadi kufikia mwezi wa Machi 2014, chuo kimetumia jumla ya shilingi 1,193,042,818/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 401,608,593/= kwa malipo ya mishahara na shilingi 791,434,225/= kwa matumizi mengineyo.

Malengo ya Mwaka 2014/2015

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015, chuo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

i. Kuendelea kutoa fursa zaidi kwa Watumishi wa Umma kujiunga na Chuo kwa mafunzo ya kukuza uwelewa na mafunzo ya kujenga uwezo katika fani mbali mbali kulingana na mahitaji ya taasisi husika.

ii. Kuendelea kutoa mafunzo ya maadili kwa Watumishi wapya 907 watakaoajiriwa katika Taasisi za Serikali, wakala na mashirika ya Umma.

iii. Kutoa mafunzo ya kujenga uwezo kwa Wakurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi wa Taasisi zote katika fani za Matumizi Bora ya Kumbukumbu, Mikataba ya Ajira, umuhimu wa "*Job Description*" na uandishi wa kumbukumbu za vikao.

iv. Chuo kitaendelea na zoezi la kuipitia mitaala ambapo, mitaala mipya ya mafunzo ya *"International Relations and Diplomacy", "Public Relations"* na *"Procurement and Supply"* itahusika, kufanya ziara katika taasisi mbali mbali kwa ajili ya kubadilishana uzoefu, kutafuta fursa za mafunzo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wafanyakazi wa Chuo.

v. Kuandaa Sera ya Mafunzo na Muongozo wa Upimaji Kazi na Kupandishwa Vyeo kwa Watumishi wa Chuo.

vi. Kwa upande wa vitendea kazi Chuo kinakusudia kununua "*transformer*" moja ili kupunguza tatizo la umeme ambalo linajitokeza mara kwa mara katika jengo la Chuo - Tunguu, kununua "*server*" kwa ajili ya utunzaji kumbukumbu, majoho 100 kwa ajili ya wahitimu, mashamiana saba, kompyuta na vifaa vyengine vya uendeshaji na utawala.

vii. Ili kutatua tatizo la uchache wa nafasi, Chuo kinakusudia kuendeleza ujenzi wa jengo lake kwa kupandisha ghorofa moja.

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 Chuo kimepanga kutumia jumla ya shilingi 2,005,100,000/= kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 1,450,000,000/= ni mapato ya chuo na shilingi 555,100,000/= ni ruzuku kutoka Serikalini.

SHUKURANI

Mhe. Naibu Spika, ofisi yangu inapenda kutoa shukrani za dhati kwa Washirika mbali mbali wa Maendeleo kutokana na michango yao ambayo kwa kiasi kikubwa imefanikisha utekelezaji wa majukumu ya ofisi. Aidha, ofisi yangu itaendelea kutoa mashirikiana na Washirika wetu wa Maendeleo ili kufanikisha dhamira na malengo yake. Kwa niaba ya serikali na ofisi yangu napenda kuwashukuru kwa dhati Washirika hao wa Maendeleo ambao ni pamoja na nchi wahisani, zikiwemo China, Korea ya Kusini, Japan, Singapore, Uholanzi, India, Oman, Marekani, Sharja, Ras-Al-Khaimah na Mashirika ya Kimataifa yakiwemo Shirika la Kazi Duniani, *KOICA*, *JICA* na Save the Children.

Mhe. Naibu Spika, wizara yangu pia inapenda kutoa shukrani kwa taasisi mbali mbali kwa mashirikiano waliyotupa na naziomba kuendelea kutuunga mkono katika jitahada zetu za kuwaletea wananchi wenzetu wa Zanzibar maendeleo. Taasisi hizo ni pamoja na Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (*ZANEMA*); Shirikisho la Vyama Huru vya Wafanyakazi (*ZATUC*); Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii (*ZATI*), Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (*ZSSF*) na kadhalika.

Mhe. Naibu Spika, nachukua fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi hususan Wakurugenzi wa Uendeshaji na Utumishi na viongozi mbali mbali na watumishi wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mashirikiano mazuri tuliyonayo katika kutekeleza majukumu yetu. Namshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Nchi (OR), Kazi na Utumishi wa Umma na Naibu Katibu, Kamisheni ya Wakurugenzi na Watendaji wote wa wizara yangu kwa kazi nzuri na msaada mkubwa wanaonipa.

Shukurani maalum kwa aliyekuwa Kaimu Waziri Wizara ya Nchiu (OR), Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwa kazi nzuri aliyoifanya kipindi chote ambacho nilikuwa kwenye mtihani. kama nilivyotangulia kusema katika maelezo yangu ya awali Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma ikishirikiana na Idara na taasisi zote zilizopo chini yake kwa jumla.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2014/2015 ofisi itasimamia kuharakisha upatikanaji wa ajira bora, kusimamia haki na wajibu wa watumishi wote, kuongeza fursa za ajira nchini na kuleta ufanisi katika utendaji wa kazi.

Mhe. Naibu Spika, ofisi hii inasimamia mafungu matatu ya bajeti, fungu 27 (Ofisi kuu), fungu 47 (Kamisheni ya Utumishi wa Umma) na fungu 48 (Tume ya Utumishi Serikalini).

Kwa upande wa mapato ofisi inategemea kukusanya shilingi 251,000,000/= na kwa upande wa matumizi mafungu yote matatu yanategemea kutumia shilingi 7,323,100,000/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida na kazi za maendeleo, ambapo, shilingi 6,995,100,000/= zimepangwa kutumika kwa kazi za kawaida na shilingi 328,000,000/= zimetengwa kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kati ya shilingi 7,323,100,000/= jumla ya shilingi 5,630,500,000/= kwa matumizi ya fungu 27, (ikiwemo ruzuku ya Chuo shilingi 555,100,000 na mapato ya Chuo shilingi 1,450,000,000/=), shilingi 510,900,000/= kwa matumizi ya fungu 48 na shilingi 853,700,000/= kwa matumizi ya fungu 47. Uchambuzi zaidi wa muelekeo wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2014/2015 unapatikana katika viambatanisho Nam. 9a, 9b na 9c.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa ijadiliwe)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Waziri hoja imeungwa mkono, tunakupongeza kwa utaalamu na ufundi wa kuwasilisha bajeti yako. Sasa Waheshimiwa tunaanza na mchangiaji wa mwanzo Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Wizara ya Nchi (OR) Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Mhe. Naibu Spika, naanza hotuba yangu hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye uweza wake mkubwa na utukufu umetukutanisha hapa leo tukifanya kazi hii ya wananchi kwa usalama, afya na uzima.

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina wingi wa shukurani kwa Mola wetu kwa kujibu dua na sala zetu kumuombea afya na uzima Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, Mhe. Haroun Ali Suleiman ambae alikuwa akiugua. Tunamshukuru Allah kwa mapenzi yake makubwa kwake kuwa sasa ni mzima wa afya na ameweza kuungana nasi hapa mapema. Tunaendelea kumuombea afya yake iendelee kuimarika ili tuendelee kuwa pamoja naye katika kazi na majukumuya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, kamati haitaacha kumshukuru Kaimu Waziri wa Wizara hii, Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, kwa mashirikiano makubwa aliyotupa wakati wote akiwa kaimu Waziri wa Wizara hii. Hakuna ambacho kamati ilikihitaji katika utekelezaji wa majukumu yake ambacho ilikikosa, kama pengo basi Mhe. Waziri wa Nchi (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ alijitahidi kuliziba licha ya majukumu mazito ya wizara yake, ambayo nayo pia aliyabeba ipasavyo. Tunampongeza na kumshukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nichukuwe nafasi hii pekee kumpongeza Mhe. Mahmoud Thabit Kombo, Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Kiembesamaki, kwa kuteuliwa kuwa mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, tunampongeza na kwakweli kamati yetu imepata nyongeza nzuri ya mjumbe ambaye ameongeza makali ya kamati na hivi sasa kamati hii imeimarika kwa kuwa na wajumbe makini zaidi. Kamati inamkaribisha na inathamini sana mchango wake mkubwa anaoutoa katika kipindi kifupi sana cha uwapo wake kwenye kamati hii, na katika ziara zetu mbali mbali za Mikoa na Wilaya zetu ambazo sote tumekuwa pamoja naye. *(Makofi)*

Aidha, niwapongeze Wajumbe wote wa kamati hii ambao siku zote wamekuwa na bidii na mashirikano makubwa ya kazi na juhudi yao ndiyo imewezesha hotuba hii kusomwa hapa leo mbele ya Baraza lako. Nichukuwe nafasi hii kwa unyenyekevu mkubwa kuwataja kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Ussi Jecha Simai — Mwenyekiti
2. Mhe. Abdalla Juma Abdalla — Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir — Mjumbe
4. Mhe. Nassor Salim Ali (Al-Jazira) — Mjumbe
5. Mhe. Suleiman Hemed Khamis — Mjumbe

6. Mhe. Bikame Yussuf Hamad Mjumbe
7. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo Mjumbe

Pamoja na Wajumbe hao, kamati hii ya Katiba, Sheria na Utawala shughuli zake zinaratibiwa na makatibu wetu ambao ni:-

1. Ndg. Aziza Waziri Kheir na
2. Ndg. Khamis Hamad Haji

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo sasa nianze kutoa maudhui ya hotuba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ambayo imepitia na kuchunguza vifungu mbali mbali vya Fungu namba 27 la Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma pamoja na taasisi mbali mbali zilizo chini ya wizara hii. Licha ya ufupi wa muda wa kupatikana vitabu vya bajeti na mapungufu kadhaa yaliyojitokeza katika vitabu hivyo, kamati yetu ilijitahidi kwa kiasi ilichoweza kupitia vifungu vya wizara hii.

IDARA YA MIPANGO SERA NA UTAFITI

Mhe. Naibu Spika, katika utekelezaji wa majukumu mbali mbali ya idara ya Mipango, Sera na Utafiti ya Ofisi ya Rais, Kazi na utumishi wa Umma kuna suala muhimu la utayarishwaji wa Ripoti ya Tathmini ya hali halisi ya malipo kwa ajili ya utayarishaji wa Sera ya Malipo ya Mishahara. Kamati imepokea taarifa kuwa taarifa hiyo imeshakamilika, tunaomba sasa ifanyiwe kazi ili sera ya malipo ya mishahara itengenezwe na kuanza kutumika haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spika, bado changamoto ya malipo ya mishahara kwa wafanyakazi wa kada mbali mbali za utumishi wa umma ni kubwa. Kamati hii imesharipoti kwenye Baraza hili kuwa, changamoto za kiutendaji nyengine zinasababishwa na maslahi duni wanayolipwa watendaji wetu hasa wale katika ngazi za utaalamu. Nalo hili Kamati inasisitiza kushughulikiwa mapema iwezekanavyo ili kupunguza malalamiko na muda wa kusubiri wananchi.

Mhe. Naibu Spika, sote ni mashahidi pale tunapowaona watendaji hao hao wanapokuwa katika Taasisi za Serikali utendaji wao unakuwa wa kiwango cha chini, lakini wanapokuwa katika Taasisi Binafsi wakifanya kazi hizo hizo au zaidi ya hizo wanafanya vizuri na matokea mazuri yanaonekana. Pamoja na mambo mengine, tatizo la maslahi duni linachangia. Kamati inasisitiza kuwa tukiwa na sera nzuri ya malipo ya mishahara na kuwajali wataalamu wetu hawatakuwa na sababau ya kukimbia ama kuwa bora zaidi kiutendaji katika Sekta Binafsi.

Mhe. Naibu Spika, bado mipango yetu inachelewa sana katika kuanzisha Mfuko wa Bima ya Afya. Kamati yetu imepata taarifa kuwa ripoti ya *"Design element"* kuhusu kuanzishwa kwa Mfuko wa Bima ya afya imetayarishwa, kamati hii inataka kujuwa lini ripoti hiyo itaingizwa katika matendo na Mfuko huo kuanzishwa rasmi kwa hapa kwetu Zanzibar. Kwa upande wa wafanyakazi wa vyombo vya Muungano vilivyopo hapa Zanzibar, tayari wanafaidika na Mfuko wa Bima ya Afya wa *NHIF* ya Tanzania bara.

TAASISI YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZANZIBAR

Mhe. Naibu Spika, Kamati yako ya Katiba, Sheria na Utawala imesharipoti katika Baraza hili kuhusu changamoto mbali mbali zinazokabili Taasisi ya Nyaraka. Kwanza kamati yangu inaikumbusha serikali kuwa taasisi hii siyo idara kwa mujibu wa sheria. Kumekuwa na mazowea hata kwenye vitabu vya bajeti kuitambuwa taasisi hii kama Idara, wakati ni taasisi kamili kwa mujibu wa sheria, tunaomba sana suala hilo lirekebishwe.

Mhe. Naibu Spika, nilikumbushe Baraza lako kuwa mnamo tarehe 30 Januari, 2008, limepitisha Sheria Namba 3 ya mwaka 2008 iliyoanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, ambayo ndiyo taasisi hii iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, Kamati inaomba mara moja marekebisho yafanyike kwa Wizara ya Fedha na Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kutambuwa jina rasmi la taasisi hii kwa mujibu wa sheria hiyo. Mara nyingi taasisi hii imekuwa ikibezwa mpaka jina lake linakosewa kwa muda mrefu sasa.

Mhe. Naibu Spika, mwaka 2014 kwenye Ripoti ya Kamati, yalitolewa maagizo ambayo utekelezaji wake ulitakiwa ufanyike kabla ya kusomwa bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/2015.

Kamati yangu imeelezwa kuwa baadhi ya maagizo hayo yatapatiwa ufumbuzi katika bajeti ya mwaka huu wa fedha 2014/15 na maelezo yake yatatolewa katika maelezo ya waziri.

Mhe. Naibu Spika, maagizo makubwa yalihusu uwekaji wa *CCTV* kwa ajili ya ulinzi wa jengo la Nyaraka, ununuzi wa vifaa vya kuhifadhi nyaraka na vya wafanyakazi. Kamati yangu haijaona fungu lolote la kutekelezwa agizo la upatikanaji wa *CCTV* licha ya maelezo kuwa suala hilo linatekelezwa kwa ushirikiano na Wizara ya Fedha sijuwi kwa kasma ipi, tunaomba kupata maelezo ya kiasi gani hasa kimetengwa mwaka huu kutekeleza maagizo hayo.

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka huu wa fedha 2014/15, kwenye fungu la fedha za maendeleo, katika Ukurasa wa 394 wa kitabu cha pili, kwenye fungu namba 27, kuna kasma namba 0401 ambayo ina fedha za mchango wa serikali ambazo ni shilingi milioni 115, zilizotengwa kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kamati yangu haikubaliani na fedha hizo kutengwa kwenye Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na inapendekeza kasma hiyo ipelekwe moja kwa moja kwenye Taasisi ya Nyaraka ili fedha hizo zitekeleze maagizo ya kamati ya kuimarisha taasisi hiyo, badala ya kupita idara nyengine na kuongeza urasimu katika utekelezaji na utendaji.

Mhe. Naibu Spika, wakati Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inapitia bajeti ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, ilipewa maelezo kuwa hadi kufikia mwezi wa Machi mwaka 2014, Taasisi ya Nyaraka ilishaingiziwa jumla ya Shilingi Milioni mia moja na ishirini na tatu, laki tisa na sitini na tatu elfu, mia tisa na themanini na tisa (123,963,989) kwa kazi za kawaida.

Mhe, Naibu Spika, maelezo haya tuliyopewa na Wizara ni tofauti na Kamati ilipofanya uchunguzi wa kina na kugundua kuwa mchanganuo wa fedha hizo haukuelezwa vizuri. Kamati imebaini kwamba kasma ya fedha hizo walizopewa Taasisi ya Nyaraka, sio kwa ajili ya kazi za kawaida peke yake bali inajumuisha fedha za malipo ya mishahara na kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, mchanganuo wa kasma hiyo umeonesha kuwa kasma ya fedha kwa ajili ya kazi za kawaida hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2014 ilikuwa Shilingi Milioni kumi na tano, laki moja sitini na tisa elfu, mia mbili na thelathini na tano (15,169,235) ambapo fedha za mishahara zilikuwa Shilingi Milioni mia moja na nane, laki saba na tisini na nne elfu, mia saba na hamsini na nne na nukta nane (108,794,754.8). Mchanganuo huo unaonesha kwa mwaka mzima Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu imepata asilimia 4 tu ya fedha kwa ajili ya kazi za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapendekeza na kuiomba Wizara ya Fedha, kuipatia Taasisi ya Nyaraka fungu lake mbali **(***vote)*, ili iweze kuingiziwa na kuweka fedha zake yenyewe kwa utendaji na utekelezaji wa majukumu yao ulio bora zaidi.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inajaribu kuonesha picha, yaani taswira ya jinsi gani Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu inavyopata shida katika kutekeleza malengo yake kwa mwaka kutokana na kukoseshwa fedha za kutekeleza malengo hayo au kupunjwa fedha hizo na Wizara. Hii ni sababu nyengine iliyofanya Kamati yangu kupendekeza kifungu 0401 kilichopo ukurasa wa 394, kwenye fedha za maendeleo kibadilishwe na kasma hiyo itengwe moja kwa moja kwenye kasma za Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2008 iliyoanzisha Taasisi ya Nyaraka na Kumbukumbu Zanzibar, kwenye kifungu cha 21 kumewekwa masharti yanayoeleza namna Taasisi itakavyopata fedha kutoka vyanzo mbali mbali.

Aidha, katika kifungu kidogo cha (2) kumewekwa sharti la kuanzisha Mfuko Maalum wa Maendeleo ya Historia na Urithi wa Taifa ambao fedha hizo zingelihifadhiwa. Kamati yangu ingependa kujua, tangu Baraza hili litunge sheria hiyo mwaka 2008 utekelezaji wa masharti ya vifungu hivyo umekwama wapi, na lini vitatekelezwa?

Mhe. Naibu Spika, yapo mengi katika Taasisi ya Nyaraka ambayo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala imeshayaeleza kwa kina katika Ripoti yake ya mwaka 2014/15, lakini kubwa ambalo Kamati yangu ingelipenda Baraza lako lipate taarifa ni uwepo wa nyumba ya kuishi watu katika eneo la Taasisi ya Nyaraka ambayo inahatarisha usalama wa eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, Kamati inahoji kama Serikali imeshasalimu amri kwa mtu huyu wakati sheria na taratibu za kumuondoa zipo wazi. Kwa mujibu wa Sheria za Ardhi, hususan Sheria Nam. 12 ya Matumizi wa Ardhi ya mwaka 1992, kwenye kifungu cha 56 imeweka sharti iwapo Serikali itahitaji eneo la ardhi kwa maslahi ya nchi, inatakiwa kuthibitisha Mahkamani maslahi hayo, na iwapo Mahkama itaridhika basi amri ya kuchukuliwa eneo hilo inatolewa na mwenye umiliki kulipwa fidia husika.

Mhe. Naibu Spika, utaratibu huo wa sheria unaelekeza malipo ya fidia kufanyika kwa mujibu wa thamani ya soko la ardhi, pamoja na maendeleo yaliyofanywa juu ya ardhi hiyo kwa mujibu wa sheria. Kamati yangu inaamini kuwa utaratibu huu unajulikana kwa vile sheria hii ipo miaka mingi na kama ungefuatwa kwa njia muafaka basi suala hili lingekuwa limeshamalizika. Ndio maana Kamati inahoji kama Serikali imeshindwa kupata ufumbuzi wa uwepo wa makaazi ya mtu katika eneo la nyaraka. Tunaomba tupewe maelezo ya hatua gani sasa zitachulikuwa na Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Ofisi ya Nyaraka Pemba, Kamati ilitoa agizo la kupatiwa jengo lililokuwa la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, na Kamati inapongeza hatua iliyofikiwa ya jengo hilo kuruhusiwa kutumika kwa shughuli za Nyaraka. Hata hivyo, tunakumbusha kuwa agizo la Kamati lilikuwa ni kwa Ofisi ya Nyaraka Pemba kumilikishwa jengo hilo, ili kuepusha usumbufu wa ofisi hiyo kuhamahama kunakopelekea upotevu wa nyaraka.

IDARA YA MAFUNZO NA MAENDELEO YA RASILIMALI WATU

Mhe. Naibu Spika, Kamati inapongeza Wizara kuweka mpango wa kuendeleza wafanyakazi kielimu na kuinua utendaji wao wa kazi. Hata hivyo, bado kuna tatizo la uwekaji vizuri kumbukumbu za mafunzo ya wafanyakazi katika taasisi za Serikali.

Hatua ya Wizara kuanzisha daftari la kuweka kumbukumbu hizo ni nzuri lakini Kamati inapendekeza taarifa hizo zianze kuwekwa kwenye taasisi zote za Serikali ambapo Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma iwe ndio kituo cha kukusanya na kuweka kumbukumbu hizo vizuri.

Mhe. Naibu Spika, ule wakati wa wafanyakazi wetu kuongeza viwango vya elimu kwa ajili ya kupata fursa ya kuongezwa mishahara na vyeo umepita. Kamati inashauri kuwa mpango wa sasa lazima uelekeze mafunzo ambayo yana tija kwa taasisi, na mfanyakazi mwenyewe kujengeka uwezo wa kiutendaji. Aidha, Kamati inashauri kuwe na utaratibu ambao kabla ya mfanyakazi kupewa ajira ya kudumu apewe mkataba wa kupima uwezo wa utendaji ***(****Performance based contract****)*** kwa miaka miwili ili kujua uwezo wa mfanyakazi kabla ya kupewa ajira ya kudumu.

IDARA YA MIPANGO NA RASILIMALI WATU

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imeshtushwa na taarifa za ukaguzi wa majalada binafsi ya wafanyakazi *(OPF)* kwa Wizara ya Afya uliofanywa na Idara ya Mipango na Rasilimali Watu. Kwa mujibu wa taarifa hizo za ukaguzi majalada 2,317 yamehakikiwa ambapo watumishi 20 haikuonekana mikataba yao, watumishi 47 haikuonekana tarehe zao za kuzaliwa na watumishi 740 hakuna taarifa zao za kuthibitishwa kazini.

Mhe. Naibu Spika, ingawa Kamati ilielezwa kuna hatua zinachukuliwa lakini tafsiri ya mapungufu hayo ni kuwa inawezekana kuna baadhi ya wafanyakazi wameghushi tarehe za kuzaliwa kwa kujipunguza miaka, upo pia uwezekano wa hadaa kwa baadhi ya watumishi kulipwa mishahara hewa. Kamati yangu inaitaka Serikali kuchukua hatua sio tu kwa Wizara ya Afya peke yake bali na Wizara nyengine zote ili kubaini mapungufu haya.

IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA UTUMISHI

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inatambua juhudi za Serikali kuongeza maslahi ya wafanyakazi kila uwezo unaporuhusu, na inaipongeza kwa kufanya hivyo. Hata hivyo, bado juhudi kubwa ifanyike kusawazisha baadhi ya mapungufu kadhaa yaliyojitokeza katika zoezi hilo la nyongeza ya mishahara kwa watumishi wa umma, kwani yapo malalamiko mengi kwenye Taasisi za Serikali.

IDARA YA AJIRA

Mhe. Naibu Spika, wakati wa kupitia kasma ya Idara ya Ajira kwenye fedha za maendeleo, Kamati imependekeza kufanyika kwa marekebisho madogo katika kifungu 0601 ambapo kasma ya shilingi milioni 15 mchango wa Serikali, iliwekwa kwenye kijifungu chengine mbali na ile kasma ya shilingi milioni 28 ya mchango wa wahisani. Kamati imeshauri mabadiliko yafanyike kuweka sawa kasma hizo ambazo jumla yake inabakia hiyo hiyo ya shilingi milioni 43. Ukiangalia kwenye kitabu kikubwa marekebisho hayo yameshafanyika.

IDARA YA AFYA NA USALAMA KAZINI

Mhe. Naibu Spika, Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ilitoa maelekezo kwa Wizara kukamilisha mwongozo wa ukaguzi kwenye taasisi mbali mbali za umma kuhusu hali ya usalama na afya za watumishi kwenye maeneo yao ya kazi, kama inavyoelekeza Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2/2011 na Sheria ya Afya na Usalama Kazini Nam. 8 ya mwaka 2005. Kamati yangu inaitaka Wizara kuhakikisha mwongozo huo unakamilika, na kazi za Idara ya Afya na Usalama Kazini zianze kwa ukamilifu ndani ya mwaka huu wa fedha 2014/15.

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA

Mhe. Naibu Spika, Kamisheni ya Utumishi wa Umma inafanya kazi nzuri ya kuendelea kuelimisha watendaji wa taasisi za Serikali na kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2/2011. Kamati yangu bado inaendelea kukumbusha ahadi ya kuchapishwa kwa Kanuni za sheria hiyo ambazo kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Waziri, zinategemewa kukamilika kabla ya kusomwa Bajeti wa Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

KAMISHENI YA KAZI

Mhe. Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2014/15, Kamati yangu imepewa taarifa kuwa Kamisheni ya Kazi, pamoja na mambo mengine, imepanga kuhakiki taasisi zipatazo 240 za kazi kuhakikisha kama zinatekeleza ipasavyo sheria na sera za kazi nchini.

Mhe. Naibu Spika, utekelezaji wa sheria na sera za kazi nchini bado hauridhishi hasa katika sekta binafsi kwenye uwekezaji wa mahoteli ya kitalii. Bado vijana wengi wanaoajiriwa katika mahoteli wanakumbana na changamoto mbali mbali kama kwamba hakuna sheria wala sera ya kutatua changamoto hizo.

Mhe. Naibu Spika, wapo baadhi ya wawekezaji wengi kwenye mahoteli ya kitalii ambao wanatoa ajira bila ya mikataba kwa vijana wetu, wanawafukuza wanavyopenda bila ya kuwalipa stahiki zao, wanawanyima haki na malipo ya mifuko ya hifadhi ya jamii na kadhalika. Achilia mbali matendo mengine ya udhalilishaji ambayo mengi yanatokea bila hatua muafaka kuchukuliwa kama vile hakuna sheria ya kuyasimamia.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inatoa agizo kwa Kamisheni ya Kazi kufuatilia wakati wa kufanya uhakiki wao; kwa kukagua mikataba ya kazi kwenye sekta ya mahoteli na kuchukua hatua stahiki kwa mujibu wa sheria, pale itakapobainika kuwa sheria na sera za nchi hazifuatwi.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ina hoja moja tu kwenye Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Kamati imeshapewa maelezo mengi na ya kutosha kuhusu maandalizi, mipango, vikao na kadhalika, kuhusu kukamilisha uanzishwaji wa ***E-Government.*** Kamati inahoji ni lini mpango huu utakuwa tayari kwa ukamilifu wake?

OFISI KUU PEMBA

Mhe. Naibu Spika, tatizo kubwa ambalo kila Kamati inapotembelea utekelezaji wa kazi Pemba ni kutoingizwa kwa wakati fedha za utekelezaji wa kazi za kawaida na malengo ya kibajeti au kutopatiwa fedha hizo kwa mujibu wa matumizi yanayohitajika.

Mhe. Naibu Spika, malengo mengi ya kibajeti yanashindwa kutekelezwa kwa wakati au kwa ufanisi kwa ukosefu wa kuingizwa fedha mapema au kwa kupelekwa fedha hizo pungufu. Kamati yangu inapendekeza kuwa Ofisi Kuu Pemba ipatiwe fedha kwa wakati na kwa mujibu wa makadirio ili utekelezaji wa kazi na malengo ya kibajeti usikwame.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu inaunga mkono Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma kwa mwaka wa fedha 2014/15. Na nawaomba Waheshimiwa Wajumbe wachangie na kutoa mawazo yao ya kuimarisha bajeti hii, na sisi Kamati tunaahidi kusimamia utekelezaji huo na kufuatilia kila Idara na Taasisi ya Wizara.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kukushukuru kwa mara nyengine na naunga mkono hoja, nikiomba ufafanuzi wakati wa majumuisho ya Mhe. Waziri. Naomba kuwasilisha.(*Makofi)*

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru wewe leo kwa jioni hii na mimi kuanza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanza mimi kwa upole kabisa na unyenyekevu bajeti hii siiungi mkono na ninazo sababu zangu za hoja nzito sana na zenye huruma sana. Na hasa nimegeuka nimekuwa bosi wangu Mhe. Ali Mzee Ali nacheza na *hansard* tu. Na hiyo ndio kumbukumbu ambayo itakayonifanya mimi niweze kusema kuwa sitounga mkono, na hasa fungu hili la Mipango na Sera nalizuia halitofanya kazi kabisa namwambia Mhe. Waziri. Na nilitegemea hasa angekuwa leo Mhe. Haji Omar Kheri ningefurahi sana, lakini kaja Waziri huyu naomba anistahamilie ndio mambo!

Mhe. Naibu Spika, sasa nianze kazi hii ya Kitabu. Mhe. Naibu Spika, hebu niulize kwanza hii Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ni Idara, Taasisi au kiofisi tu, hebu niwaombe Wanasheria nisaidieni. Sheria tumeipitisha hapa lakini naona sijaifahamu. Kwanza naomba hili Mheshimiwa hujanitafsiriwa vizuri sana, pengine sheria zangu mimi na watu wengine za kisasa zinakuwa tofauti, lakini zile sheria za nyuma ndio zenye mantiki na Uingereza sana sheria zile wanazitumia na ndio maana utakuta wengi wamefaulu kwa kupitia Muingereza. Na sisi ndio tumepitia humo humo kwenda kusoma kwa Waingereza katika sheria hizo. Sasa naomba hapa nipewe tafsiri hii.

Na ofisi hii tuliambiwa imeundwa Tume ya kuwa nyaraka zimeibiwa. Hivi jamani tupo *serious* kweli na Serikali hii. Nyaraka si mchezo, nyaraka ni kumbukumbu kubwa sana. Utakuta kuna watu ambao wenye kujua nyaraka umuhimu wake ni watu binafsi tu, hawa hapa kina Mhe. Ali Mzee Ali na watu wengine wanaweka kumbukumbu.

Ni muhimu sana kuweza kujua nyaraka za historia ya nchi, lakini sisi tunafanya hili jambo kama hatupo *serious* nalo. Ndio maana nikakuuliza nipe tafsiri Idara, au Taasisi au kijiofisi tu. Kwa sababu ukiniambia katika mantiki hapa mimi nitakuja kuzuia hilo fungu. Mhe. Naibu Spika, hili suala mimi sikubaliani nalo, linatuumiza sana akili sisi wengine. Nyaraka za Serikali zinaibiwa, Kamati imeundwa hatujui imefikia wapi. Na Kamati leo itatueleza mpaka leo wamefikia wapi, na waliokwenda kwenye Bunge Maalum watatueleza, lakini tumeunda Kamati hapa tumefikia wapi. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, kwa utaratibu sana kuwa nielekezwe kwa sababu haya mambo ya nyaraka kuweka ndani ni muhimu sana kimataifa, na watu kujua kumbukumbu. Inabidi tuwatafute watu wa nje maskini kina Mzee Ali haiwezekani.

Lakini Mhe. Naibu Spika, ukurasa huu wa 29 kuna kitu kinaitwa Ajira. Mimi siifahamu hii lugha ya ajira. Leo hii tunasema ajira kwa sababu ukisema una Idara ya Ajira mimi sijaona u-*specialize* wao, nakataa kabisa hili neno tulifute, kwa sababu bado Wazanzibari hawana ajira. Lakini leo humu tunaambiwa tunazo ajira.

Mhe. Naibu Spika, nikiendeleza katika pointi muhimu naingia katika Kamisheni ya Kazi. Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako namnukuu Mhe. Waziri katika bajeti iliyopita. "Nakubaliana na ushauri wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk suala la wazalendo kupewa ajira katika maeneo yetu wala hatuna pingamizi".

Hawana pingamizi kwa hilo haki yake tumpe pale anapofanya vizuri na tumpongeze na pale anapokosea tutamuelekeza. "Wizara inakubaliana na wazo lake na Serikali kwa ujumla. Katika utafiti uliofanywa na Mamlaka

ya Uwekezaji wa Vitega Uchumi *(ZIPA)* ripoti imepatikana ya mwaka 2012 inaonesha kwamba Wazanzibari walioajiriwa kwa nafasi za wataalamu ni 4,315, kutoka Tanzania Bara ni 1,676 na kutoka nje ya Tanzania ni 316."

Mhe. Naibu Spika, mimi napingana, halafu nimegundua kitu kimoja Mawaziri wetu hawana ule muundo wa kutembelea katika zile Idara zao. Hilo sina wasiwasi hawaendi, humu ndani leo nikiwauliza hapa watashindwa kunambia naamini hivyo, huo ukweli tuseme. Hilo nakubaliana nalo wala wasinipinge, maana yake akinipinga shauri yake Rais anasikia huko atakuja kumwambia tutakaa pembeni. Na ndio maana ikafika pahala wanatupa *data* nyengine zinakuwa si za kweli, na ndio maana yanapotokea matatizo wanakuja kutwambia yanakuwa si ya uhakika.

Mhe. Naibu Spika, maafisa wetu wa Idara ya Kazi kwa kweli hawatendi kazi vizuri. Juzi nilikuwa katika mtihani mmoja mzito sana. Siku moja mwalimu wangu hapa Mhe. Waziri alinambia nisiwataje Wahindi. Na kwa nini, sina njia ya kusema nimseme Mzungu wakati si Mzungu, nimseme mtu kutoka Tanzania Bara wakati si Mtanzania Bara, au nimseme Mzanzibari wakati si Mzanzibari, siwezi, sina njia, namuomba sana Mwalimu. Nitasema Mhindi *from where* nitataja na ile nchi yenyewe sasa atanifahamu, sikusudii Mhindi ndani ya Zanzibar. Naomba sana hilo anistahamilie. Wananchi wetu wa *United Petroleum* wanadhalilishwa, nimekwenda na mwenyewe Mkurugenzi tumechukua na maafisa wao tumekuta mambo ambayo tumeyakuta.

Mhe. Waziri nataka kwanza uende kuna Wahindi watatu pale, kuna Mhindi mmoja anaitwa Sanjeey, na kuna Mhindi huyo watu walifikiria labda Rais kamleta huyo Sanjeey kumbe Ranjeev, na Ranjeev kaletwa kwa mujibu wa sheria. Watu hawakufahamu hawajui kama Mhe. Rais amemleta Ranjeev kutusaidia katika mambo ya *community* ili tupate maendeleo kama nchi nyengine wanavyopata maendeleo, lakini waliji-*confuse* hapa. Sasa ninachoomba sana Mhe. Naibu Spika, huyu mtu amefikia pahala sasa hivi hata ile sheria sasa hivi ya ukaazi imeshakuwa ya muda mrefu. Alifukuzwa hapa aliondoshwa, sijui mipango gani hata akaletwa, ninataka nije nijibiwe, aliletwa vipi hapa nchini hata kupewa kibali, kaweleta na wenzake wengine wawili, wanafundishwa kazi tena ninataka na *certificate*.

Mhe. Waziri njoo na *certificates* zao hapa, kwa sababu wenzetu wana mchezo wa kudanganya, munaona nyinyi hawa wana *certificate* zinakwenda kwa mujibu wa kazi yenyewe, kumbe wanafundishwa. Kazi wanafundishwa hapa hapa Tanzania. Naomba sana *research* hiyo, ninataka uje nazo *certificates* hapa, *certificates* zao ni lazima zipatikane.

Mhe. Naibu Spika, na hii sio hivyo na wananchi wameshachoka kabisa. Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ninamshukuru sana Mhe. Rais amefuta watu kama hao ma-*experts*, mara moja walifutiwa. Sisi tunaona tabu gani, tunawadhalilisha wananchi wetu, tumefikia viwango vizuri vya kusoma, tuna vyuo hapa wanasomeshwa watu wetu. Halafu unasema Wazanzibari hawafanyi kazi, ndio tabia yenu munayosema, munawadhalilisha bure kumbe kazi wanaweza.

Mhe. Naibu Spika, lakini kutokana na wakati tunawanyima haki zao. Hiyo haki ni lazima tuseme ukweli ulivyo. Hii *Hansard* ya ngapi leo imesema hapa hakuna kilichofanyika. Mtu anakwambia kaletwa mtu kushika fedha. Mzanzibari gani asiyejua kuweka hesabu, vyuo vile vina maana kuwekwa kule Chwaka, futeni basi viondoshwe.

Mhe. Naibu Spika, inauma watu wanakuja kuchukua uchumi hapa shamba la bibi. Tena ninakwambieni Waheshimiwa Wawakilishi niungeni mkono jambo si mchezo, tena wanakusikilizeni wananchi. Kazi yetu kubwa ni kuwatetea wananchi wetu, hawana ajira, ajira anakuja kuchukua mtu wa nje. Anachukua ma-*foreign* halafu anaondoka, halafu na uchumi unakua, unakua wapi? Tusiwadanganye wananchi, ninaomba sana kwa hilo.

Ninaomba ninukuu tena *Hansard* hii nzuri tu, inasema hivi, "Mhe. Mwenyekiti, niwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wetu hususan wale wa Chama cha Mapinduzi kwamba wawajibike, kwa kweli wasije wakafikiria na wakafika pahali wakaona Chama cha Mapinduzi kitawalinda na kutokuwajibika, na Chama cha Mapinduzi kisitumike kama kichaka cha kuficha maovu". Mimi sitoficha maovu, huyu hapa Mnadhimu wangu kasema.

Haiwezekani kila siku tunazungumza yale kwa yale. Hii haiwezekani Mhe. Naibu Spika, na ninaomba sana Mhe.Waziri Mhe. Haji Omar Kheri nimshukuru ameifanya kazi vizuri, hakufika pahali pazuri pa kutoa ripoti kwa

sababu alikuwa ameshakuja mwenyewe. Mwenyewe umeshakuja ninaomba sana umwite Kamisheni wako wa Kazi haraka sana kabla sijazuia fungu. Tunangojea ushahidi gani? Mimi hapo ndio ninaposhangaa.

Watu wanakwambia vitu, mtu anafika miezi minane hajalipwa fedha, tena unataka ushahidi gani. Halafu Mhe. Naibu Spika, kuna vikampuni vibovu vibovu hapa, kama kuna kampuni moja ya *security* inayoitwa *VESPA*, imeajiri vijana 30. Mpaka leo hawajalipwa mishahara yao, kila siku wanadanganywa tu, wanaambiwa pesa zenu kule *melia*, ninataka na hili nipewe jibu.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri ninataka na hili kama kuna *cheque* huko ***melina*** huko, sijui *melia* huko ikazuiliwe walipwe Watanzania pesa zao. Sio wanakuja watu, tusiviruhusu vikampuni vibovu vibovu hivi vinadhalilisha watu wetu. Havina hata ule usimamizi mzuri, hizo ofisi zenyewe ni mbovu. Tunamuomba sana Mhe.Waziri na hawa vijana wa *VESPA* ninaomba sana katika kuja kueleza yako ninataka nije nipate jibu lililokuwa rasmi.

Tena wale watu Mhe. Naibu Spika, maskini ya Mungu hawakufungishwa mikataba. Kosa ni nani, hawa watu wetu wa vitengo vyako hawapiti wakawaelimisha watu, ndio tatizo lenyewe hilo. Hawajui sasa hivi nikiwauliza swali ni makampuni mangapi yapo. *Wallahi* hawajui watakuja kunidanganya. Nataka nifahamu ni kampuni ngapi zimefanyiwa *registration* na kampuni gani wataalamu wamekwenda kuzisimamia. Nalo hilo nataka nipate hapa, kwa sababu tukizubaa sasa hivi tumekuwa tunafanya mambo ya kitoto. Ninataka niletewe hesabu ya uhakika.

Na ma-*foreigners* wangapi ambao wanaofanya kazi hapa nchini na *certificates* zao, sasa itabidi tufanye hivyo. Mhe. Naibu Spika, wanakuja watu tu na vi-*certificates* za wizi wizi; vya *forgery* kabisa, na sisi tunaridhika wenyewe hapa, waambieni hapa kama mshahara mdogo maafisa ninaomba Mhe. Waziri wasipende kusaka tonge na wao. Hivi vishahara vidogo vidogo, waongezeni hawa mishahara wasiwadhalilishe watu. Hivi fursa vidogo vidogo hawa wasihangaike na njaa, kuona nikipewa *buffet* au nikipewa tenda hii, hapana. Waambiwe watapigwa makofi siku ya pili wasifanye hivyo.

Mhe. Naibu Spika, ninamuomba sana Mhe.Waziri waongezeeni mshahara maafisa wenu, au kama sheria ipo *weak* tuleteeni tutakusaidieni. Lakini ninasema Mhe. Naibu Spika, mutusaidie kutokana na hali halisi ilivyo watu wanazidi kuumia.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Kamisheni. Mimi sina wizara nyingi nina wizara hizi zangu tatu tu kwa makusudi nimeziweka kwa sababu ya uchungu wa wananchi wa Zanzibar wanavyopata tabu. Kwa mfano kule kwetu sehemu ya Kipandoni, kuna mtwana mmoja anapandisha maua, kila siku anafukuza watu. Hapa pana kazi ipo wapi. Lakini una kitengo kimoja Mhe. Waziri kizuri, maana ninakusifu mpaka tai uliyovaa, siwezi kuacha. Kitengo kile kizuri sana, kinawasaidia Wazanzibari, niseme alau yule jamaa jina lake simjui Mungu amjaalie yupo hapa hapa duniani lakini jina lake limenitoka kidogo.

Jamaa huyo ni mtu mzuri sana, *wallahi* huyo ninampa sifa yake. *Wallahi laadhim* ninampa sifa yake, mimi simpi mtu sifa kipuuzipuuzi wala hanijui wala haniombi, wala sina haja ya pesa zake. Lakini yupo *active* haki ya Mungu ninakwambia, hataki upuuzi upuuzi, anasimamia kesi nimeziona mimi si chini ya kesi tano, kawasaidia Watanzania. Hivyo ndivyo inavyotakiwa lakini Idara yako maafisa wako sio, sikufichi ninakwambia, maafisa wako sio, *wallahi laadhim* sio, na hao watakupotosha Mhe. Waziri sikufichi, wala mimi simuogopi mtu ninamwambia mtu ukweli kutokana na ukweli ulivyo.

Nimekwenda mwenyewe *physical* kabisa *Zanzibar Petroleum* na ninaambiwa pale maafisa wanakwenda siku zote na *still* kesi zipo hazihukumiwi. Mama mmoja anasema pale *wallahi* keshachoka matusi Mhe. Naibu Spika, anatukanwa mtu ndani ya nchi yake na huyo mtu, sasa yule mwanamke kamfundisha kazi mwenyewe, huyo mwenyewe Muhindi kafundishwa kazi na huyo mama, halafu leo anakwenda kumtukana. Mama anasema anataka kulia machozi, kweli yule mwanamke taaluma yake aliyokuwa nayo. Tunangoja ushahidi gani.

Waziri fukuza! Usiweke kitu, fukuza Waziri, hakuna mchezo sasa hivi, kuwa kama Rais Kikwete bwana, hebu fukuza uone mwaka 2015 kama hatukukupa Urais, wala usiwe na wasiwasi, tekeleza sera ilivyo. Unaokoa hapa vijana wako wengi wa Chama cha Mapinduzi, usione tabu Mheshimiwa, fukuza mtu bwana. Jenga *strategic* nzuri, vijana wetu wapate kazi nzuri, uchumi ukue na waenee ule uchumi wao. Sera hiyo tumetunga wenyewe. Ninakuomba sana Mheshimiwa ufanye hivyo. Lakini nije katika Utumishi wa Umma. Mhe. Naibu Spika, kulikuwa na maelezo mazuri sana ya Mnadhimu. Hii kuhusu Utumishi wetu wa Baraza la Wawakilishi, sijui mpaka leo wamefikia wapi.

Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu anasema Mhe. Waziri alipokuwa akijibu, "Kwa muundo umeidhinishwa lakini ikijua kwamba muundo ulioidhinishwa huo tulikusudia sisi isipokuwa kilichoidhinishwa ni muundo wa utumishi katika kada kwenye Baraza la Wawakilishi". Lakini ule muundo ambao ofisi haujaidhinishwa mpaka leo, hii ndio tunayoizungumza hapa.

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa tukieleza nimwambie atupe sababu ya kwamba muundo huo hadi leo ni kwa nini haujaidhinishwa. Mhe. Naibu Spika, ningeomba sana hili ni Baraza tukufu, ni Baraza kubwa sana Mheshimiwa. Sijui tunakuwa na uzito gani wa muundo wetu wa Baraza kutokuletewa hapa na kutokupitishwa. Hebu tusemeni kuna uzito gani jamani. Twambieni kama kuna watu wengine mizigo tutawatoa, siku hizi tunataka kuwatoa watu wengine mzigo hakuna kuacha, tutawatoa tu. Hawa watu mizigo hawatufai kwenye serikali Mhe. Naibu Spika, kwa sababu mizigo inakuwa ni mizito haibebeki, inaididimiza serikali kila siku tu, baada ya kuleta hoja nzuri na kuisaidia serikali, wananchi wakaipenda serikali tunailalamisha. Jamani tunakwenda wapi?

Mhe. Naibu Spika, na hili ninataka nipate jibu, tuone jinsi gani huu muundo huu umekuja kweli au haujaja, na kwa nini sababu gani mpaka leo hii haujaja ili tuweze kupigia buti vizuri. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, nina buti kali sana leo ina njumu, na wewe ndio hali kama hivyo, unaumwa Mwenyezi Mungu akujaalie uendelee na afya nzuri. Lakini buti kwa hili mwalimu wangu Waziri ninaomba sana unistahamilie, hapa nipige kidogo buti kwa sababu kuna mambo ambayo tunarudia yale yale kama nilivyosema, haturudii kwa mujibu wa kuvunja Kanuni. Tunarejea kutokana na utekelezaji wake haufanyiki.

Mhe. Naibu Spika, nilikuwa ninasema kuwa kuna Mawaziri nitakuja kuwataja mizigo au kuna Makatibu wengine nitakwambia ni mizigo, na kuna Wakurugenzi wengine mizigo kwa serikali, hao nitakuja kuwataja lakini wizara hii bado. Nitaona hii atakapokuja kunijibu na atakapokuja kujibu vizuri, nitasema aah! Waziri kumbe si mzigo mwepesi, anafaa tumpandishe. Sitoona tabu, Katibu vile vile nitasema huyu anafaa tumpandishe, Mkurugenzi nitasema vile vile anafaa tumpandishe.

Mhe. Naibu Spika, lakini si hivyo, tutamwambia Rais huo mzigo uliokuwa nao haufai, kutokana na yale mambo tunayoyasema jamani hatujaja hapa kula pesa tu, tunakuja hapa kusema mambo ambayo tunayaona, na Katiba inatulinda sisi kufuatilia mambo haya ya kimaendeleo. Muundo gani wa bajeti au kupitisha bajeti, ndio kazi yetu, wananchi wametuleta kwa sababu hiyo.

Kwa hivyo, ninasema, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri wangu mpendwa asije akaingia katika nakama ya mzigo. Rais atamchoka tu kabisa. Tunawaombeni mawaziri wangu kwa unyonge kabisa ninakwambieni mliokuwa hamujapitishiwa bajeti zenu, hebu turidhisheni, nendeni kwenye *department* zenu hizi kuna matatizo, zifanyieni *refreshment* mapema kabla hamujaingia kwenye shimo, mimi sikuachieni. Kwa sababu tumekula ahadi pale, nimekamatishwa Msahafu, nimekula ahadi pale, nitalinda na nitatetea wananchi eeh! Mungu nisaidie, tena nisaidie nini, anipe mshipa, haiwezekani. Ninaomba Mhe. Naibu Spika, hilo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema sitounga mkono na ninakuona unataka kunipigia kengele, usinipigie kengele. Kwa hivyo mimi ninasema nitaendelea na ile ile sitoiunga mkono, na Waheshimiwa wenzangu ninakuombeni kabisa sana tuwasaidie maslahi ya Wazanzibari hawapati kazi katika makampuni wanadhalilishwa, wanachukua watu wengine ajira bila ya kuwa na ile fani yenyewe, *certificates* bandia zipo tele.

Mhe. Naibu Spika, ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Makame Mshimba Mbarouk. Sasa nafasi ninampa Mhe. Hamza Hassan Juma na baadae Mhe. Ismail Jussa Ladhu. (*Makofi*)

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Naibu Spika, kwanza ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii nikaweza na mimi kutoa mchango wangu mdogo kabisa katika Wizara hii ya Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, mimi simuigi Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, yeye Mhe. Mshimba ana yake na mimi nina yangu. Mimi kwanza hii bajeti kwanza siikubali, na hichi kitabu sikikubali. Kwanza huyu Waziri siye, huyu aliyechapwa kwenye hichi kitabu siye. Yupo wapi, sio mwenye kitabu akae mbele. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, mimi nadhani mlango wa mbele kawaida hukaa mwenye nyumba, akakaribisha wageni. Sasa mwenye wizara kakaa mlango wa nyuma. Sasa kwanza ninaomba wizara utaratibu huu si mzuri. Naomba sana vitabu vyetu vinapoletwa basi yule Waziri mwenye ile dhamana ya wizara basi ndio tumuone hapa mbele. (*Makofi*)

Lakini sio kwamba siungi mkono kwa sababu Waziri kakaa nyuma, siungi mkono kwa ahadi ambazo tunazotolewa kila siku hapa Barazani ili tupitishe bajeti, halafu hazitekelezwi. Mhe. Naibu Spika, ninaanza kutoa shilingi mia moja ya mshahara wa Mhe.Waziri. Na nikitoa shilingi mia moja ya mshahara wa Mhe. Waziri basi ninaamini, kule ofisini kukiwa hakuna Waziri basi labda kazi zitakwenda. Maana yake inaonesha labda Mawaziri ndio wanazuia hizi shughuli za kazi. (*Makofi*)

Na wizara inaweza ikaenda bila ya Waziri. Katibu Mkuu tu anaweza akaendesha shughuli. Mhe. Naibu Spika, ninaanza hivi kwa sababu gani, tumezungumzia kwa muda mrefu na *hansard* zipo hapa, kuhusu ukaidi wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ninaanzia huko. (*Makofi*)

Kamisheni ya Utumishi wa Umma tulipofanya marekebisho ya Katiba tuliipa nguvu, lakini nguvu zile tulizozipa zina mipaka yake. Sasa leo imefika pahala Kamisheni ya Utumishi wa Umma inakuwa baada kwamba Utumishi wa Umma isimamie haki za wafanyakazi kama alivyokuwa Mhe. Waziri alivyokuwa anamalizia *summary* ya hotuba yake, yeye mwenyewe aangalie kule mwisho alizungumzia kwamba wizara itahakikisha kwamba inasimammia haki na maslahi ya watumishi wa umma.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Katiba, Baraza la Wawakilishi linatakiwa liwe na sheria yake ya Utawala. Na tumefanya jitihada kubwa na tunategemea katika kikao hichi mwishoni tutawasilisha mezani ile tunaita kwamba kusomwa mara ya kwanza, mswada wetu wa Baraza.

Lakini pamoja na kwamba ile sheria yetu ya Utumishi na Utawala wa Baraza haijakuwa tayari, lakini Baraza la Wawakilishi lina Tume yake ya Utumishi. Na hii Tume ipo vile vile kwa mujibu wa sheria za nchi.Kuna Tume ya Idara Maalum, Tume ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Mahakama. Hizi Tume zipo vile vile kwa ajili ya madhumuni ya vyombo husika.

Leo Mhe. Naibu Spika, juzi nilikuwa ninamsikiliza Mhe. Rais Hoteli ya Bwawani pale, alipokuwa anaadhimisha maadhimisho ya Sherehe za *May Day*. Alieleza vizuri sana kwamba pamoja na mwaka huu hatutoongeza mshahara lakini tunajaribu kuangalia maslahi ya watumishi kupitia *scheme of service*.Leo ninasikitika sana chombo kama hichi mpaka leo kinanyanyaswa, chombo kama hichi. Tuna *separation of powers*.

Mhe. Naibu Spika, Baraza hili kama leo tunapitisha muundo wetu wa Utumishi na muundo ule tunategemea uwe kivutio cha kuweza kupata wataalamu ambao wataweza kuja kuwasaidia Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kuweza kuisimamia vizuri serikali. Leo Kamisheni ya Utumishi ya Umma inazuia maslahi ya watumishi wa Baraza la Wawakilishi.

Sasa je, utegemee tusiwe na wataalamu hapa kwenye Baraza, tusiwe na mabingwa wa kuweza kutuelekeza kazi zetu. Mimi ninadhani hili si jambo la busara. Sasa mimi ninadhani suala hili tumelizungumza sana tukafika pahala mpaka ikaundwa Kamati ya Maridhiano, tukaenda mpaka mbele huko ikajadiliwa, ikaambiwa suala limeshafikia muafaka.

Lakini sasa leo unaukubali muundo, lakini maslahi huyakubali. Sasa unakubali kitu gani. Kwa hivyo, mimi ninadhani hili suala ni moja katika suala ambalo nitaondoa shilingi mia katika fungu la mshahara wa Mhe. Waziri. Na sio hili tu, kwa sababu sitaki nionekane mbinafsi kwamba ninawatetea watumishi wa Baraza la Wawakilishi kwa kuwa na mimi ninafanya kazi katika Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, katika Utawala Bora inatakiwa *separation of powers* ionekane wazi wazi. Mahakama, Serikali na Baraza la Wawakilishi. Lakini vile vile kuna taasisi ambayo ipo kwa mujibu wa sheria, na taasisi ile ina uzito inakaribiana na Baraza la Wawakilishi ambapo hata ripoti yao anatakiwa airipoti Waziri, ripoti yao anaiwasilisha mwenyewe *CAG* kwa Mhe. Rais, na ripoti ile kama Mhe. Rais ndani ya wiki moja haijafanyiwa kazi, basi anatakiwa aiwasilishe kwa Spika, ili iwasilishwe moja kwa moja Barazani.

Mhe. Naibu Spika, tunasikitika zaidi *CAG* Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, ni chombo ambacho kinatakiwa kiimurike serikali. Leo wananyanyaswa wanazungukwa, sio busara kumtengenezea maslahi yake *CAG* wakati wanaofanyakazi mnashindwa kuwasimamia maslahi yao. Muundo wa Utumishi wa Ofisi ya *CAG*, ingawa Mhe. Waziri alitoa maelezo, lakini mimi naamini maelezo yale alikuwa anatoa Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, ili labda tulainike ile bajeti yake tuipitishe, lakini tukasema sawa kwa sababu yeye hana mamlaka ya kuweza kutoa *Authority* ya masuala ya *Scheme of service* ya Ofisi ya *CAG*, ndio maana tukasema tunamsubiri mwenyewe Waziri muhusika. Haiwezekanai katika nchi ambazo zinafuata Utawala Bora, Zanzibar tumo. Leo kwa nini vyombo ambavyo vinasimamia kuimurika serikali kwa nini mnavinyanyasa.

Mhe. Waziri mwalimu wangu na umenisomesha, lakini kwa leo naomba tuombane radhi, na hili Mheshimiwa nitabakia peke yangu nitashindwa kwa kura, lakini katika haki za hasa hawa watumishi ambao wanatakiwa waisimamie serikali unawakalia. Mimi nadhani Mheshimiwa hii sio haki, na mimi hapa simuangalii labda Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma, najua hawa wako chini ya usimamizi wako, sasa kama umeshindwa kuwasimamia basi tutawasimamia sisi hapa Barazani.

Haiwezekani leo Mkurugenzi katika Ofisi ya Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, anasimamia *vote* zaidi ya nne katika wizara mbali mbali, leo maslahi yake anashindwa na Mkurugenzi kama yule wa Fedha ambaye yuko serikalini, ambaye anasimamia *vote* moja tu, tumeona wapi mambo haya! Mhe. Naibu Spika, Utawala Bora tusiuzungumze kwenye maneno.

Leo Mhe. Issa Haji Ussi Gavu alisoma vifungu vya Katiba hapa katika maswali na majibu. Nilimwambia hivyo vifungu vya Katiba mnavyovisoma msivisome kwa kufurahisha watu; kwamba Katiba inasema hivi, tunataka Katiba iheshimiwe.

Mhe. Naibu Spika, sitoiunga mkono bajeti hii, na hapa Mhe. Waziri naomba kakae na Kamisheni yako, ili tujue miundo ya utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Ofisi ya *CAG* inamalizikia vipi, sio inafikia wapi, inamalizikia vipi. Leo hapa hatutaki tuambiwe tuko mbioni, tumo katika maandalizi. Kama mbio zimeshakuwa ni za muda mrefu na *Hansard* zipo. Mhe. Waziri aliyekuwa anaisimamia Wizara hii aliahidi hapa, kwamba aah! Sasa hivi suala hili katika mwaka huu yaani huu tunaoupitisha bajeti yake linamaliziwa. Iko wapi, hapa katuletea picha, yeye mwenyewe utendaji wake hatukuuona.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli sisi hatutaki sura za watu kwenye vitabu, tunataka matendo yao mazuri kwenye vitabu. Mhe. Naibu Spika, katika taasisi nyengine ambayo bado inaendelea kunyanyaswa ni Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vijana wetu hawa wanatusaidia, wanalinda nchi yetu, na ni vijana wakakamavu. Nilijaribu kufuatilia katika kipindi hiki, nikaambiwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma wameshaukubali muundo

wa utumishi wa Idara Maalum, lakini wameukubali muundo lakini maslahi yao hawajayakubali, sasa ndio mmekubali kitu gani. Yaani hapa ni usanii, Mheshimiwa sasa hivi usanii hatuutaki, hapa tunataka matendo hakuna suala jengine tulilojia hapa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hata Idara Maalum kazi wanazozifanya *scheme* wameshapeleka. mimi nadhani hii Kamisheni ya Utumishi wa Umma ndio imetuonesha kwamba ile mamlaka ambayo tumewapa, sasa hivi wameanza kusahau kwamba kuna taasisi zina mamlaka sawa sawa na wao, ndio maana wanawanyanyasa. Sasa mimi nadhani wakati umefika tuwanyang'anye sasa hii nguvu ambayo tuliwapa.

Mhe. Naibu Spika, hapa tulipitisha Sheria ya Utumishi, tukampitishia maslahi yake Katibu Mkuu Kiongozi, kila mmoja baada ya kupitisha tukauliza sisi ndio tuliopitisha yale. Tulipitisha kwa mur-wa, kwa sababu tunaheshimu mamlaka za watu na taasisi zao.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hii Kamisheni ya Utumishi wa Umma, hebu waende duniani wakajifunze Mabunge mengine yanavyoheshimiwa na hizi Kamisheni za Utumishi. Waangalie hizi Idara Maalum au nchi za wenzetu nyengine wanaita vikosi vinaangaliwa vipi. Ndio maana wenzetu huko kila siku wanapinduana pinduana kwa kushindwa kuangalia maslahi yao. Msiwaone hawa vijana wetu wanakwenda na kurudi, na wao wanaumia!

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea kuzungumzia lile lile suala la Ofisi ya *CAG*, kuna Wakurugenzi ndani ya Ofisi ya Utumishi wa Umma, ambapo watumishi wale wamekuja kuwaunda baadaye, ule muundo wao wamekuja kuunda baadaye wakati Ofisi ya *CAG* tayari walikwishakupeleka muundo wao, watu wao wa ndani ya idara yao au wa kamisheni yao tayari wamewatengenezea *scheme* na wanawalipa marupurupu mazuri na mishahara mizuri, lakini wale wenzao wa *CAG* wamewasahau, tunakwenda wapi. Hapa hatutaki ubinafsi, tunataka kazi tu.

Mhe. Naibu Spika, jengine pamoja na kwamba mwenzangu amelizungumza, lakini na mimi nitalizungumza. Tunaendelea kuzungumzia, na hata niliposoma ripoti yangu ya Bajeti Kuu ya serikali ya hotuba ya Wenyeviti nilizungumzia suala la ajira ambazo hazina mikataba.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wafanyakazi wetu au wananchi wetu wengi wamekuwa manamba sio wafanyakazi wala sio watumishi, ni manamba tu. Mtu anafanya kazi mwaka mmoja ukishamaliza msimu, msimu unaokuja anakwenda kuomba kazi. Kila siku watu hawa kazi yao kuomba kazi, tutakwenda hivi mpaka lini?

Leo Mhe. Naibu Spika, kila mtu anapoishi umri unapungua na huko anakokwenda kwa ajira hizi za *part time;* ajira hizi hazina kiinua mgongo. Baada ya miaka 25 mbele tutakuja kuwa na vizee ombaomba wengi, kwa sababu anaajiriwa leo, kesho ajira yenyewe haina uhakika, anakaa mwaka mzima hajaajiriwa au anapiga zaidi ya miezi sita hajaajiriwa, anahangaika anapata ajira nyengine. Mimi nadhani sasa hivi hii idara ya kazi waweze kufuatilia, na sasa *season* inaanza na hasa katika mahoteli.

Nchi yetu Mhe. Naibu Spika, viongozi wetu wamejitahidi wameleta utalii, utalii huu ulikuwa zaidi uwafaidishe wananchi, lakini utalii huu Mheshimiwa unawafaidisha wageni wanakuja wanawekeza, fedha wanakwenda kuweka nje, matokezeo yake wale wafanyakazi wetu angalau basi wangefaidika wao, matokezeo yake wanafanya kazi za *part time*, wanafukuzwa ovyo, hakuna utaratibu na ukiangalia hata zile jumuiya zao wa wafanyakazi katika hayo mahoteli na wao vile vile wamegeuzwa kama wawekezaji, kwa sababu badala ya kuwatetea wafanyakazi wao wanakuwa upande wa wale wawekezaji.

Mimi nadhani Idara hii ya kazi na wao vile vile nitakuja kuleta tabu sana katika kupitisha hili fungu lao, mpaka watueleze je, wanasimamia vipi haki na maslahi ya wafanyakazi wetu na vijana wetu.

Vile vile, Mhe. Naibu Spika, juzi katika sherehe za Muungano, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano alitoa agizo kwa upande wa Tanzania Bara. Sasa mimi nadhani kuiga kitu kizuri sio vibaya. Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano alieleza kwamba anaagiza kuwa wale wafanyakazi wote kutoka nje ambao wanafanya kazi ambazo

wananchi wa Tanzania ajira zile wanaziweza na wanazo sifa, basi wasipewe vibali vya kufanya kazi. Sasa na msimu unakaribia Mhe. Waziri tunakuagiza, hatukuombi, tunakuagiza uhakikishe huyu Mkurugenzi sijui ndio Kamishna wa hii Idara ya Kazi, au kwa jina lolote, ahakikishe kwamba safari hii vibali anavyovitoa basi ahakikishe kwa kazi ambazo wananchi wetu wa Zanzibar hawana uwezo nazo.

Mhe. Waziri nakupenda sana kwa sababu ni msikivu na mfuatiliaji, lakini tutalifuatilia wenyewe hili suala, kama huo mshahara nitakuja kuuachia uende pale ofisini, basi nitahakikisha kwamba vibali tutajaribu kufuatilia na tunaomba wafanyakazi wote mnaofanya kazi katika sekta ya uwekezaji, tupeni taarifa wakati wowote baada ya ajira hizi kuanza hasa katika mahoteli, mkiona mfanyakazi yeyote mgeni amepewa ajira ambayo mna uwezo nayo basi tuambieni msisubiri bajeti, tuambieni Waziri ofisi yake tunaijua na yeye mwenyewe tunamjua. Kama bahati mbaya fungu lake halikupita la mshahara atakuwepo nyumbani tutamfuata huko huko, maana yake atakuwa anapeleka tu vi-*memo*, tutakwenda huko huko kwake. Kwa hivyo, suala hili Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa namuomba Mhe. Waziri aidha akiwepo ofisini au akiwepo nyumbani ahakikishe anafuatilia vizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini Mwenyekiti wa Kamati nakupongeza sana baada ya kusoma ripoti yako. Ameeleza kwamba mwaka 2008 tulipitisha sisi Sheria Namba 3 ya hii taasisi ya nyaraka, na hii iliwekwa hivi kwa makusudi, kutokana na uzito na umuhimu wa taasisi hii, mpaka leo bado tunai-*treat* kama idara, na ndio maana kuna mambo mengi ambayo walitakiwa wayafanye wanashindwa kuyafanya kwa sababu taasisi hii tunaiendesha kama idara ya serikali. Na tunajua idara zetu za serikali kusubiri mambo ya *OC* na vitu vyengine, wakati idara hii ilikuwa inatakiwa iwe na nyenzo ambazo zitakazoweza kuweka zile kumbukumbu zao.

Mhe. Naibu Spika, nilijaribu kuangalia kitabu chako haraka haraka, kwa sababu utaratibu tuliokuwa nao sasa hivi mnasoma *summary*, tunakuwa hatupati muda mrefu wa kuvisoma hivi vitabu. Lakini waliahidi humu kwamba katika bajeti ya mwaka huu watahakikisha kwamba wanaweka *CCTV Camera;* ili kuhakikisha kwamba zile nyaraka zetu zinakuwa salama na jambo lolote litakalojitokeza basi ili kumbukumbu zile ziwepo.

Mhe. Naibu Spika, sijui suala hili atakuja kulijibu nani, maana yake katika Baraza lililopita tuliunda hapa Kamati Teule, na Kamati Teule ile ilitakiwa iende Idara ya Nyaraka kwa ajili ya kwenda kuchunguza wizi wa nyaraka za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilivyoibiwa, sasa mpaka leo ni zaidi ya miezi mitatu. Sasa sijui utaratibu wetu, kama utakuja kusimama utasema kwamba ile ripoti inakuja au imeganda njiani.

Kwa hivyo, suala hili mimi nafikiri Mhe. Waziri baadaye atawasiliana na Ofisi ya Naibu Spika, ili kutueleza wamefikia hatua gani. Bado dakika tano nimeshasikia.

Mhe. Naibu Spika: Aaah! Bunge la Katiba lilizuia kidogo, lakini mtapewa taarifa.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Alaa, unanijibu kabisa. Nakushukuru kwa kunijibu kabisa, kwamba Bunge la Katiba lilitucheleweshe, lakini bado muda tunao. Kamati hata kipindi hiki ambacho tuko ndani ya shughuli za Baraza, kamati inayo haki na unayo nafasi wewe ni mtu mkubwa, unayo haki ya kutoa agizo kwamba kuanzia Jumatatu Kamati iende ikaanze kazi. Hatutaki kulazalaza mambo, muda uliobakia tunataka mambo yote yawe safi. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, vile vile, suala la Bima ya Afya. Mimi kwa kweli kila siku kuambiwa tumeandaa utaratibu, mambo yako mbioni, utaratibu wa bima ya afya Mhe. Naibu Spika, watu wetu wanyonge, wafanyakazi wetu wa Zanzibar kama tunavyoona maslahi yao kwa kweli yako duni.

Mimi nadhani na suala hili namuomba sana Mhe. Waziri hebu lisimamie, na ninaamini ukiamua kulisimamia, basi naamini ndani ya mwaka huu bajeti ya mwaka ujao tayari wafanyakazi wetu watapata bima ya afya. Tukiweza wafanyakazi wetu kujiunga na bima ya afya basi tutaisaidia hata hospitali ya Mnazi Mmoja.

Mhe. Naibu Spika, tumeanza kuona matunda ya bima ya afya, sasa hivi Hospitali zinakusanya fedha nyingi sana kwa kutibu watumishi wa umma. Al Rahma mwaka uliopita peke yake walikusanya bilioni 1,200,000,000, hiyo ripoti tumeipata tulipokuwa tumekaa na wadau. Ingawa hospitali yetu ya Mnazi Mmoja walipata fedha kidogo, lakini tulijaribu kuwapa maelekezo, naamini na wao watayafuata na serikali yetu kupitia hii wizara yako Mhe. Waziri ikiweza kupitisha hii Sera ya Bima ya Afya kwa wafanyakazi wake, basi naamini hata hospitali ya Mnazi Mmoja itaweza kuimarika katika utoaji wa huduma.

Mhe. Naibu Spika, suala la maslahi ya watumishi mbali mbali. Nimeona hapa mmesema kwamba mmejaribu kuandaa sera ya kuangalia maslahi ya watumishi wa umma, lakini bado kuna viongozi ambao wako katika taasisi nyeti sana. Tena mimi nashangaa Kamisheni ya Utumishi wa Umma zile taasisi nyeti hasa zinazoichunguza serikali wao ndio wanaowabana, mpaka leo ninavyozungumza hapa ni aibu kwamba tumeanzisha idara au kitengo hiki cha kupambana na rushwa, lakini mpaka leo yale maslahi ya Mkurugenzi mwenyewe mpala leo hayajaidhinishwa.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mtu yeye ndiye anawachunguza watu, yeye mwenyewe maslahi yake yako duni, si atakwenda kuchunguzwa yeye huyo? Huyo akifika ofisini anaangaliwa hebu wewe unavuta ngapi huko.

Mhe. Naibu Spika, nitamsubiri Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria atakapokuja katika kitabu chake, labda atatwambia vipi Ripoti ile ya Tume za haki za binadamu, kwa sababu naamini mawaziri hawa wa Katiba na Utawala Bora, huwa wanatakiwa na hizi jumuiya za kimataifa watoe ripoti za utawala bora. Labda waje watwambie katika ripoti za utawala bora je, hizi taasisi zinazoisimamia serikali, serikali imesemwa vipi, je, imesemwa vizuri au imesemwa vibaya. Kwa haya niliyoyasema hapa tu basi naamini ripoti ya utawala bora haitoisema vizuri serikali, kwa sababu serikali inavikalia vile vyombo ambavyo vimewasimamia wao.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, namtaka Mhe. Waziri kuhakikisha kwamba mara tu bajeti yake kama itapita basi tuhakikishe maslahi ya Ofisi ya ZAKUKURU; mamlaka hii ya kuchunguza rushwa, kuhakikisha kwamba maslahi kwanza ya Mkurugenzi, lakini na wale maofisa wake vile vile wanazingatiwa. Ndio maana nikawa najiuliza huku Kamisheni ya Utumishi kuna nini? Mbona hawa wote ambao kazi yao ni kuichunguza serikali wao ndio wanawawekea mguu, ni kuwaadhibu au hawataki kuundwa zile taasisi.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, Mhe. Waziri akija atanipa maelezo, atanipa ile hatua iliyofikia, lakini tunataka utekelezaji wa hatua hizi. Kwa sababu tumeona tulipopitisha bajeti ya serikali, na mimi ndio Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti, ambapo bajeti ya serikali ilikuja mbele yangu na kamati yangu tukaikamua na tukaijadili. Kuna fungu limewekwa kwa ajili ya kufanya marekebisho ya maslahi ya watumishi mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hata hawa ambao niliwasema sasa hivi kwamba maslahi yao mpaka sasa hivi kama hayajazingatiwa basi nadhani liko fungu ambalo tumeliweka katika Mfuko Mkuu wa serikali. Lakini vile vile, kuna fungu maalum tuliliweka kwa ajili ya kufanya *adjustment* ya maslahi ya watumishi kama hawa. Hatuwezi tukawa na wafanyakazi ambao wanafanya kazi kwa manung'uniko.

Mhe. Naibu Spika, suala la *E- Government*. Hebu Mhe. Waziri akija aje atwambie kuhusu hili suala la *E-Government* limeshafikia hatua gani mpaka hivi sasa. Maana yake suala hili limekwenda pale katikati tuliona kasi kubwa, lakini sasa hivi naona hata zile harakati zake hatuzioni. Sasa hebu aje atwambie, kwa sababu mradi huu ulikuwa kama mpira wa kona, huyu anatia kichwa, huyu anatia bega na huyu anatia kifua, mwenyewe hasa hajulikani, kila mmoja anaripoti katika kitabu chake. Sasa hebu labda Mhe. Waziri aje atwambie mpira huu ni wake? Na kama ni wake yeye basi aje atwambie umefikia wapi, unakaribia kuingia goli au bado ndio kwanza uko kwenye kibendera cha kona.

Kwa kuwa Mawaziri wenzake ambao mradi huu, yeye akisema sio wake haumuhusu, wako mbele tunawasubiri wale ambao unawahusu tuje tupate taarifa kamili. Kwa sababu kwa jinsi tulivyoambiwa mradi huu ungeweza kusaidia mpaka kuzalisha mapato, lakini leo mashimo yameshachimbwa, tumewaona Wachina walijitahidi wale

sijui ndio Wajapani, wameshazika mikonga yao na mambo mengine. Sasa je, kilichobakia ni nini? Ngoma imekwama wapi?

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kabisa, mimi nilikuwa nataka niseme Mwenyekiti wa Kamati alizungumzia kama kuwalaumu watumishi wa umma zaidi wanapofanya kazi katika maeneo ya *private*, kwa sababu wako wengine kutokana na taaluma zao wanaweza kufanya kazi huku serikalini, lakini vile vile baadaye wakaenda kufanya kazi uraiani, ilimradi yale masharti ya huku serikalini ameyatimiza inavyopasa.

Lakini wanapokwenda kufanya kazi uraiani wanakuwa wanawajibika vizuri, sasa hebu tujiulize, kwa nini wakawa wanawajibika vizuri. Wanawajibika vizuri kwa sababu wanalipwa vizuri,sasa na huku kwetu Mhe. Naibu Spika, tusiwanyanyase watumishi wetu, tunataka watumishi wetu tuwalipe vizuri ili na wao waweze kufaidika, na hili nalizungumza kwa sababu unapomchereweshea maslahi yake, na hata katika ripoti yetu ya Kamati ya Wenyeviti katika bajeti ya Serikali tulisema, wale ambao waliocherewesha aidha miundo yao au waliochereweshwa kupatiwa maslahi yao, basi wanapoanza kulipwa kuanzia pale aliporekebishwa yale maslahi yao na wao waweze kulipwa *arrears* zao, kwa sababu ile ilikuwa ni haki yao.

Mhe. Abubakar Khamis Bakary, mara nyingi alikuwa anazungumza kwamba unapocherewesha haki ni sawa sawa na kuikosesha haki, ingawa siku hizi kauli ile anakuwa haipendi sana kuisema kwa sababu siku hizi yupo mbele, lakini kipindi kile alipokuwa huku nilipo mimi alikuwa siku zote anasema. Leo nafikiri Mhe. Abubakar atakuja kutueleza kama ile kuchereweshwa sasa hivi imekuwa maana yake kama mkubwa anakuwa hajafika mdogo anakuwa kacherewa, sasa sijui na hii ndio inakuwa vile vile au vipi. Sasa hili nilikuwa naomba sana Mhe. Naibu Spika, katika suala zima la maslahi ya hawa watumishi wetu basi tuweze kulizingatia vizuri ili waweze kufanya kazi vizuri katika maeneo yao.

Mhe. Naibu Spika, lakini samahani kidogo mwaka jana niliwahi kuzungumza suala la maslahi ya madereva, nimeangalia kwenye *Hansard* Mawaziri walipokuwa wakitoa ufafanuzi walisema kwamba maslahi ya madereva yanazingatiwa, na hili nililizungumzia kutokana na mabadiliko ya utendaji wa kazi; zamani vikao vya Baraza la Mapinduzi vimechelewa sana ilikuwa ni saa moja au saa mbili, lakini sasa hivi Mhe. Naibu Spika, vikao vyetu wakati mwengine vinafika mpaka saa tano au saa sita za usiku, sasa hawa madereva kutokana na mishahara yao hawana uwezo wa kununua vespa hawa.

Kwa hivyo, Serikali kupitia Kamisheni ya Utumishi wa Umma watoe muongozo au watoe maagizo kwamba hawa madereva wanaowaendeshea Mawaziri wote waweze kupatiwa vipando, leo Waziri anakaa Mazizini dereva wake anakaa Mwera kikao cha BLM kimemaliza saa saba za usiku au saa nane, je, tutegemee huyu atarudi wapi, na kwa bahati mbaya katika nyumba za Mawaziri hakujawekwa chumba cha dharura cha kulala dereva pale anapocherewa.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nadhani suala hili la madereva hasa wa Mawaziri, na kama nilivyosema mwanzo madereva wa Mawaziri kwanza wapatiwe mafunzo maalum aweze kuwa na uwezo wa kumuendesha Waziri, lakini vile vile na maslahi yao nashukuru mmesema mmeyashughulikia lakini suala la vipando vile vile nilikuwa naomba lishughulikiwe.

Mhe. Naibu Spika, sasa baada ya hayo naomba sana Mhe. Waziri yale niliyosema sikusema kwa masihara, pamoja na kwamba ni mwalimu wangu, lakini hapa ndio tupo kazini, na ile elimu aliyonifundisha ndio hii naifanyia kazi basi tustahamiliane. Bajeti hii Mhe. Naibu Spika, sijaona katika eneo lolote ambalo nitaweza kuiunga mkono, siungi mkono hata kwa asilimia moja, ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kunipa fursa ya kusimama hapa nikiwa hai, mzima wa afya na mimi kutekeleza wajibu wangu, na kwa baraza hili ni mara yangu ya mwanzo kusimama kuchangia katika bajeti za Wizara za Serikali.

Mhe. Naibu spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake, kwa sababu ya muda umepunguza nadhani haya ya shukurani na pongezi niishie hapo.

Mhe. Naibu Spika, niende katika maudhui ya hotuba hii. La kwanza kabisa mimi niombe Serikali, na nikisema Serikali nakusudia Mkuu wa Serikali kwamba ikiwa Serikali inahisi haina haja ya Maalim Haroun katika uongozi basi bora impumzishe; kwa nini nasema hivyo nikiangalia mtiririko wa bajeti ya Wizara hii nimepata mshtuko mkubwa sana kwamba kweli Serikali ambayo ina lengo la kumfanya Waziri wake na Wizara anayoiongoza ifanye kazi zake inaweza kweli ikamtendea haya.

Mhe. Naibu Spika, wakati fulani nilikuwa nikimtania Mhe. Haroun; mwalimu wangu Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Kazi na Utumishi wa Umma, kwamba hiki kitendo cha kila mara kuhamishwa wizara kitapelekea ufanisi wako tuliouzoea maalim wangu kuonekana, lakini sasa napata hofu zaidi kwa mtiririko wa bajeti ya Wizara hii, na nawaomba Wajumbe wenzangu wanielewe waangalie ukurasa wa 59 wa kitabu cha bajeti kinachoelezea mtiririko wa fedha zilizotengwa na zilizoingizwa katika matumizi ya kawaida kwa mwaka huu tunaozungumza.

Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kupima utendaji wa Wizara kwa kuangalia fungu la mishahara maana kama ni hivyo mishahara inalipwa asilimia zote tutakuwa tunalipana kwenda kazini na kurudi lakini hakuna tija wala kazi inayofanyika, kwa hivyo mwananchi haoni matunda ya kulipia kodi serikali iweze kumuhudumia kama huduma zenyewe hazipati. Tutapima umakini wa Serikali na anayeiongoza na sera zinazomuongoza ikiwa tutaona katika matumizi ya kawaida *other charges (oc)*, uingizaji wa fedha ukoje.

Mhe. Naibu Spika, sasa katika Wizara hii, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti imeingiziwa asilimia 31.7, Idara ya Uendeshaji na Utumishi imeingiziwa asilimia 38, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa asilimia 4, Idara ya Mafunzo asilimia 15.9, Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi asilimia 23.7, Idara ya Mipango na Rasilimali Watu asilimia 25, Kamisheni ya Utumishi asilimia 29, Kamisheni ya Kazi asilimia 12.9, Idara ya Ajira inayotegemewa ifanye mipango ya kuleta ajira katika nchi asilimia 7.5, Idara ya Usalama na Afya Kazini inapumua hiyo imepewa asilimia 50, Idara ya Teknolojia ya Habari asilimia 19.6, Afisi Kuu Pemba asilimia 42, Tume ya Utumishi asilimia 43 na Chuo cha Utawala wa Umma ambacho ni taasisi inayojitegemea ndio imepewa angalau asilimia 64.

Sasa Mhe. Naibu Spika, katika hali hii tunategemea kweli Waziri huyo ana maajabu gani hata aweze kutekeleza yale ambayo kayapanga au kapangiwa, na ningeweza kuelewa kwamba tunapoambiwa nchi yetu masikini tuna lugha tunapata kuzisema humu keki yenyewe ndogo, lakini Serikali hii hii kupitia Wizara yake inayosimamia mapato Wizara ya Fedha; inaturipotia kila mwaka kwamba mapato yanaongezeka, sasa mapato yakiongezeka mbona hatuyaoni kwa utendaji katika uingizwaji wa fedha katika Wizara zinazohusika.

Mhe. Naibu Spika, na tutakuja kuona tukifika Wizara zetu nyengine katika kamati tunazosimamia hali hii inajitokeza katika wizara nyingi, lakini Wizara ya Fedha yenyewe ikija mwisho wa mwaka jana nilisema hapa wanaiongojea mwaka huu kila idara asilimia mia moja.

Sasa mimi nimuombe Mhe. Rais, kwa heshima na taadhima kama tunadhani, maana kuna picha iliyojengeka hii kama Wizara ya Fedha inaweza kufanya kazi zote za Serikali basi azivunje Wizara zote aweke Wizara ya fedha ifanye hizo kazi, lakini kwa mfumo huu hatufiki, wananchi wamechoka, wananchi wanalalamika kwa sababu hawajaona tija ya Serikali, kwa sababu huduma hazipatikani, na huduma ziweze kupatikana ikiwa uingiaji wa fedha wa namna hii katika kila Wizara; hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, lakini la pili hata katika ukusanyaji wa mapato nikiangalia ukurasa wa 4 na 5 wa hotuba hii Wizara imeweza kukusanya asilimia 19 tu ya Makadirio ya Mapato, na ukiangalia kiambatanisho 1(a) ambacho kinatoa muhutasari wa mahesabu hayo unakuta Kamisheni ya Kazi imekusanya asilimia 17 tu, ilipangiwa ikusanye milioni 800,000,000/= imekusanya 139,242,375/=, Idara ya Afya na Usalama Kazini ilipangiwa milioni 20 imekusanya milioni 10, imekusanya 18,733,600 sawa na asilimia 94.

Lakini kwa jumla ni asilimia 19 kwa sababu ya Kamisheni ya Kazi, sasa nikiangalia muhutasari wa hotuba hii mapato haya yalikatwa kutokana na vibali vya kazi kwa wafanyakazi wa kigeni, ukaguzi wa mikataba ya kazi, na ukaguzi wa usalama wa afya katika sehemu za kazi. Kwa sababu waliokuwa hawakutimiza malengo ni Kamisheni ya Kazi waliokusanya asilimia 17 tu, maana yake ni kwamba mapato ya vibali vya kazi kwa wafanyakazi wageni na ukaguzi wa mikataba ya kazi ndiko ambako kuna matatizo.

Mhe. Naibu Spika, sasa tunaomba tuelezwe kwamba kwa nini Kamisheni ya Kazi inashindwa kukusanya mapato haya, je, kuna uzembe ama kuna rushwa ya kuwaachia wafanyakazi wa kigeni waweze kufanya kazi lakini mapato yao yanatokana na viwale vyao vya kazi ikawa hayapatikani, na kama imepungua tuambiwe, kwa sababu bajeti hii haikusema, tuelezwe.

Mhe. Naibu Spika, hali hiyo hiyo iko katika uingizaji wa mapato katika fedha za maendeleo lile la *OC* kwa jumla yake Wizara imepata asilimia 39, lakini wanasema haitoi taswira nzuri kwa sababu kuna Idara imepewa asilimia 4, sasa unategemea inaweza kutekeleza kazi zake. Lakini kwenye miradi ya maendeleo kilichoingizwa ni asilimia 6 anatwambia Mhe. Waziri, katika hali halisi tusitegemee mafanikio yoyote katika Serikali ambayo usimamizi wake wa matumizi, vipaumbele vyake ni kama hivi ambavyo nimevieleza, na msimamizi wa hayo Wizara ya Fedha ikija mtakuja kuona hapa ni asilimia 100 kama tulivyoona mwaka jana.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema hayo niende la pili na mimi niungane na aliyesema kwamba siungi mkono bajeti hii na nitaizuilia fungu lake, lakini mimi mbali ya lile ambalo wamezungumza wenzangu nitazuia fungu kwa sababu ya suala la Sera inayoongoza marekebisho ya mishahara kwa ujumla wake.

Mwaka jana ilipokuja Wizara hii nilihoji hapa kwamba tunaambiwa tuidhinishe fedha. Na katika miaka mitatu iliyopita ilikuwa baina ya bilioni 17.5 mpaka bilioni 19 kwamba ni fedha za marekebisho ya mishahara.

Nikahoji mwaka jana hapa nikasema tunataka tuidhinishe sisi Wawakilishi wa wananchi lakini hatujui *formula* gani inakwenda kutumika katika kufanya marekebisho haya ya mishahara, nikamtaka Waziri atwambie, tukaambiwa mishahara ni siri ya wafanyakazi, nikasema sijasema nielezwe kama Ismail Jussa analipwa kiasi gani lakini kuna viwango vimewekwa, tuelezwe marekebisho hayo yatakwenda kufanywa vipi, hatukuelezwa.

Mhe. Naibu Spika, Matokeo yake yalipoanza kurekebishwa kuna malalamiko makubwa kutoka kwa watumishi wa umma, na kinachoonekana ni kwamba tunajipendelea wakubwa. Kuna malalamiko ya wananchi kwamba wakubwa wanajipendelea lakini na watumishi wa kada za juu; Makatibu Wakuu, Wakurugenzi, Mameneja hao ndio wanaonufaika, ndio maana kuna marekebisho mengine watu ukichukua mshahara na marupurupu na maposho mengine pengine alichoongezewa kinaweza kufika shilingi milioni moja, lakini mfanyakazi wa kawaida analalamika anasema wametwambia wengi kwamba wengi wamepewa nyongeza ya moja kwa moja ya shilingi 25,000 kweli ni haki hiyo? Halafu tunasimama tunasema Serikali hii inawajali wananchi, ni serikali ya wakulima na wakwezi na wafanyakazi, hivi ndivyo tunavyowafanyia wafanyakazi wa ngazi za chini Mhe. Naibu Spika, haya wananchi wanayalalamikia.

Mhe. Naibu Spika, nitatoa mfano mmoja kwamba *formula* tusilaumiwe tumedai *formula* hatukupewa humu ndani, kuna wafanyakazi waliokuwa wametumikia kwa uzoefu zaidi ya miaka 16 lakini kigezo wanavyotueleza wao wanavyoambiwa kigezo cha nyongeza kinatizamwa kipato alichokuwa akilipwa kabla, sasa hatujui *formula* ni elimu, *formula* ni miaka aliyotumikia, *formula* ni kitu gani.

Mhe. Naibu Spika, Kwa sababu hawa ninao mfano mmoja wametumikia watu kwa miaka 16; wengine wamelipwa 200,000 na kidogo kwenda juu, wengine wamelipwa 200,000 na kidogo kwenda chini, wote wametumikia miaka 16 na zaidi. Sasa *formula* hatuijui Mhe. Spika, nikija nikisema kwamba fungu hili linatumika vibaya nina kosa gani mimi Mwakilishi? Kwa sababu *formula* niliyoitaka sikupewa kwenye Baraza, na kama chombo hiki hakipewi taarifa mwananchi ataipata wapi taarifa hiyo, huyu mtumishi wa umma ambaye haridhiki na haya anakwenda kuhoji wapi Mhe. Naibu Spika sisi Wawakilishi wao hatupewi taarifa hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, nasema hili, kwa mwaka huu nitalizuilia fungu mpaka nipewe maelezo ya kutosha, nitamzuilia Mhe. Waziri si kwa sababu ya kumuonea Mwalimu Haruon, mimi namuonea huruma kwa haya anayofanyiwa, mimi nasema anayofanyiwa, lakini kwa sababu naihoji Serikali nitataka nije kupewa maelezo, na tuelezwe kwa kina hiyo *formula* inayotumika katika marekebisho ya mshahara najua mwaka huu tumeambiwa hayapo, kuna fungu litatumika katika kurekebisha mishahara kwa mujibu wa taratibu za kawaida, lakini tunapima hapa pia utekelezaji wa miaka iliyopita tunataka maelezo.

Mhe. Naibu Spika, naitaka vile vile Serikali ije itwambie kama inaongeza mapato kama inavyotwambia lini tija hii itamfikia mwananchi katika mkutano wa kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani, Shirikisho la Wafanyakazi Zanzibar lilisema kwamba kwa hali ya maisha ilivyo basi kima cha chini kingefanywa angalau kuwa laki 319,000/= kama nakumbuka vizuri, tunataka kusikia kauli ya serikali juu ya hili, na mimi naamini hata hizo ni kwa kujinyima mno kwa sababu hali ya maisha tunaijua sote mtu anatakiwa alipe nyumba, mtu anatakiwa ajitibu akiumwa, mtu anatakiwa asomeshe watoto wake, leo michango imezidi katika Serikali hii, mtu akiumwa anatakiwa akachangie huduma hospitali, kuna chakula, kuna malazi kuna huduma chungu nzima Mhe. Naibu Spika, naomba Serikali itwambie kauli yake juu ya kauli hii ya Shirikisho la wafanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, jengine na mimi niungane na Mhe. Hamza Hassa Juma kuulizia suala la *E-government*. Mimi naomba serikali ifike pahala itwambie ukweli chombo hichi cha usimamizi wa shughuli za umma, kuhusu mradi huu unaoitwa Serikali mtandao; E-*government*, tushapigwa maneno mengi sana katika chombo hiki.

Mhe. Naibu Spika, na mimi nimekuwa mmoja tangu mwaka wa mwanzo Serikalini nilitaka maelezo juu ya suala hilo sababu nilikuwa na wasi wasi mapema juu ya gharama halisi za mradi huu, tumetumia takriban dola za kimarekani milioni 21 hizi Mhe. Naibu Spika, hazipungui bilioni 32 pengine kwa fedha za Tanzania, lakini ukiuliza hata katika Wizara moja moja kuna fungu kila mwaka la mradi wa Serikali mtandao kumefanyika nini hupati maelezo, Makatibu Wakuu hawana maelezo, Wakurugenzi hawana maelezo, Wizara ya Mawasiliano waliokuwa wasimamizi hawana maelezo, tunapigwa bla bla tu Mhe. Naibu Spika, tumeshachoka na bla bla!

Mhe. Naibu Spika, sasa leo *E-government* haina maelezo tunaletewa *E-services*, naiangalia katika hotuba hii katika ukurasa wa 26 tunaendelea kupewa maneno yale yale kwamba sasa kama vile *E-government* imeshafanya kazi sasa kuna huduma za *electronic* ni *service* za kimtandao zinataka kuingizwa humo, hii *E-government* ku-*take off* imeshindikana fedha hizi zimekopwa kwa ajili ya Wazanzibari wanazilipa kwa kodi zao, huku hospitali hazina madawa, skuli hazina vifaa, maisha yanaendelea kuwa magumu, wanahangaishwa lakini huku fedha zinatafunwa kama hivi, halafu mradi wenyewe huoni kitu. Hakuna *E-government* tumefika pahala Serikali itwambie kama fedha hizi zimetafunwa hakuna kitu tuambiwe tusidanganywe.

Mhe. Naibu Spika, tulidai maelezo hapa Kamati ikaja ikakiri, niliomba Kamati Teule humu ndani nikakataliwa tukaambiwa kamati ya sekta ikachunguze, tumeandika barua wizara zote tangu wizara inaongozwa na Mhe. Haji Omar Kheri wakati ule ni Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, wakatwambia mwende Wizara ya Fedha, tumeandika Wizara ya Fedha hatukupewa, tumeondoka sisi kamati imekuja kamati nyengine mwaka jana imeomba haikupewa maelezo.

Mhe. Naibu Spika, kwa nini tuendelee kuvumilia matumizi mabaya ya fedha za wananchi masikini wa nchi hii ambao huduma hawazipati lakini huku tunaendelea kupigwa maneno kila siku, naomba maelezo katika hilo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, naomba vile vile nielezwe na Serikali katika ukurasa wa 29 na 30 kuna Idara ya Ajira. Katika Idara ya Ajira, tumeambiwa kwamba kuna muhtasari pale wa ajira ambazo zimepatikana mwaka jana, na katika hili kuna watu 410 waliopatiwa kazi kupitia kampuni ya *DANAWOS*, vijana 859 wamepatiwa nafasi za kazi nje ya nchi, vijana 340 wameripotiwa kuajiriwa katika sekta binafsi ya hoteli. Vijana 76 wanaotafuta kazi wamesajiliwa kwa ajili kuwaunganisha na ajira.

Mhe. Naibu Spika, hapa nina suala hivi kama kweli serikali inafanya kazi yake, tunakubali kwamba Idara iripoti kwa mwaka mzima kwamba vijana waliojisajili kwao ni vijana 76 ndio wanaotafuta kazi katika nchi hii? Unaweza kunambia kwamba hajaja kujisajili lakini nitauliza serikali imefanya jitihada gani kushajiisha watu na kujua umuhimu, hivi kweli kama mwananchi kijana anajua kwamba akitaka ajira kuna pahala pa kwenda kusajiliwa ajue halafu asiende?

Mhe. Naibu Spika, lakini tutizame hizi takwimu zilizopatikana kwa mwaka huu mzima tunaahidiwa kwamba tutazalisha ajira 2000 kwa mwaka mzima, lakini maelezo ni hayo. Lakini tunazalisha ajira kwa sera ipi na hii si ndio Wizara hii ina serikali kwa ujumla wake hasa Wizara inayosimamia Tume ya Mipango imekuja na mipango gani ya kiuchumi ya kuitumia nafasi nzuri ya Zanzibar Kijiografia, Kistretejia, kuja na sera barabara za kiuchumi zitakazozalisha ajira?

Mhe. Naibu Spika, leo kwa Zanzibar hapa tungeona si kuna sekta ya biashara, kuna sekta ya viwanda, kuna sekta ya utalii, kuna sekta ya uvuvi, kuna sekta ya utoaji wa huduma, kuna sekta ambayo mpaka leo imekwama kwa sababu tunaona muhali ya mafuta na gesi. Serikali imejipanga vipi kuzalisha ajira katika sekta hizi.

Mhe. Naibu Spika, Leo hiyo sekta moja ya utalii iliyokuwepo nayo Wazanzibari wanashindwa kupata ajira, tumesema kila mwaka tunakata mwaka tunakata mwaka wa nne na tunaukata mwaka wa 5 serikali hii tutaibana tutaendelea vile vile kwamba imeshindwa kuwahakikishia wazanzibari kipaumbele katika ajira katika sekta ya utalii. Kila hoteli unayokwenda, huwaoni wazanzibari, kama unaona labda ni asilimia moja, mbili, tatu, tunafanya nini? Halafu tuwaambie kweli watendaji sisi tuna lengo la kuwapa ajira.

Mhe. Naibu Spika, nchi ambayo haitafuti utatuzi mzito wa tatizo la ajira kwa vijana wake inaandaa jeshi ambalo likiwa haliridhiki linaweza likaja kufanya machafuko katika nchi, tusifike huko. Hizi nchi tulizoziona hazijafika popote leo nchi za arabuni. Lakini ni tafrani za vijana wale wanapoona kwamba serikali haziwahudumii hakuna ajira, hawaoni kwamba serikali zinawajibika kwao, matokeo yake wanaingia mitaani wanafanya vurugu, tusifike huko Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Bado dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, ahsante Mheshimiwa zinanitosha hizo. leo tunaposikia makundi bado tunasoma katika magazeti sijui mbwa mwitu, ubaya ubaya, panya *road*, yanaanza kwa kukosa imani kwa matokeo kama haya. Serikali itwambie ina mpango gani vijana hawa kuwapatia ajira. Jukumu hili la kuja na sera hata katika sekta binafsi, lakini sera zitokane na serikali, na serikali makini tu ndio inaweza ikaja na sera namna kama hii.

Mhe. Naibu Spika, dakika zangu zilizobakia nimalizie haraka haraka katika Idara ya Nyaraka. Idara ya Nyaraka tumeambiwa hapa kuna nyaraka zimeibiwa, urithi wa nchi hii, hazina ya nchi hii. Lakini kwa nini zisiibiwe ikiwa suala la mradi wa kuweka *CCTV camera*, mwaka wa 4 linaripotiwa katika hotuba za bajeti lakini hakuna kilichotekelezwa mpaka leo.

Mhe. Naibu Spika, Leo ukisoma hotuba hii ukurasa wa 23 tunaambiwa kwamba mwaka jana ilikuwa lengo kuweka *CCTV camera* na baada kuhoji sana mwaka jana tunaambiwa mwaka huu zitawekwa. Katika utekelezaji hazionekani kama zimewekwa, katika malengo ya mwaka ujao wa fedha imefutwa kabisa halimo. Sasa tunafanya nini ndani Mhe. Naibu Spika. Lakini kama amepewa asilimia 4 ya bajeti anategemea ataitoa wapi *CCTV camera*?

Kamati nimeisikia wametaja Idara ya Mipango Sera na Utafiti, sijui katika kitabu cha mahesabu, lakini katika malengo Idara ya Mipango Sera na Utafiti hamna humu kwamba kuna lengo la kuiwekea *CCTV camera* Idara ya Nyaraka hamna.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie na hili la Baraza la Wawakilishi na mimi niungane na wenzangu wote wala hatusemi haya kwa sababu labda ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi lakini labda huu ni mfano kwa sababu tuko hapa kwa karibu tunauona.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana tulisimama kwa msimamo mmoja humu ndani, tena Mhe. Salmin Awadh alikuwa ndio mkali sana katika suala la Muundo wa Utumishi wa Baraza la Wawakilishi. Tukataka kauli ya Waziri kwenda kukaa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma ili kulimaliza suala hilo. Ninastaajabu leo wenzangu wanaripoti kwamba bado suala hili halijapatiwa ufumbuzi. Naomba maelezo ya kina ya Wizara na kama nilivyosema, kwa sababu hizo nilizotaja sitaiunga mkono bajeti hii mpaka nipate maelezo ya kina, na kama nilivyosema na nimuombe Kiongozi Mkuu wa Serikali katika Baraza hili, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, aje atwambie kwamba je lengo ni kumfelisha Mhe. Waziri anayesimamia Wizara kwa uingizaji wa fedha namna hii. Ahsante.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia jiioni hii ya leo. Lakini kwanza kabla sijachangia, niseme tu kiungwana na kibinadamu na imani ya dini yangu ya kiislam, nimuombe Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema Mhe. Waziri, ampe nguvu ili tuweze kushirikiana naye kama tulivyomuona hii leo. Kwa kweli tumefarijika na tumejenga imani, na ninaamini Mwenyezi Mungu atamjaalia kila la kheri kumpa nguvu za ziada katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hilo niseme tu mimi nina mambo machache sana ambayo nataka kuchangia katika maeneo haya, na zaidi nataka nichangie katika suala hili la sekta binafsi ambalo wenzangu wengi wamejaribu kulizungumzia. Lakini mimi nitaangalia katika eneo moja tu ambalo linanipa mashaka mpaka leo, na wengi wanasema kwamba kuna kazi ambazo wananchi wa nchi hii wanazimudu hazihitaji taaluma za kutosha, lakini pamoja na kwamba hazihitaji taaluma za kutosha tunazo zile taaluma lakini bado hatujaona fursa kutolewa katika yale maeneo. Eneo ambalo nililokusudia kulizungumza ni eneo la ulinzi na hususan katika mahoteli yetu ya kitalii.

Mhe. Naibu Spika, imekuwa ni mazoea sana katika maeneo yetu haya ya utalii kuona kwamba kuna walinzi wa zile *security guards;* yaani ulinzi wa vile vitengo vya watu binafsi. Sasa viko vingi tu, kuna KK sijui kuna nani ambavyo tumekuwa tuna mazoea ya kuvizoea. Lakini mashaka yangu hayaji kwa pamoja labda tumewapa watu na nini, ni vikundi ambavyo wengine kuna watu kutoka Kenya, kuna watu kutoka Uganda, kuna watu kutoka Tanzania Bara wakati vijana wetu wengi wanakuwa wanateseka na ajira.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nilikuwa nimsaidie Mhe. Waziri katika hili kuna namna gani tunaweza kuwasaidia vijana wetu namna moja au namna nyengine. Wazo ambalo ninataka nimsaidie Mhe. Waziri kwamba hebu tuige mfano wa wenzetu Tanzania Bara. Wenzetu Tanzania kuna vijana huwa wanajiunga katika Jeshi la Kujenga Taifa, sasa wale ambao wanakosa sifa za kwenda kuajiriwa katika vikosi vya ulinzi, iwe Usalama wa Taifa, iwe Jeshi, iwe Polisi wanakuwa wanatumia kwa kuanzisha kitengo maalum cha *Suma Guard*, kwa wale vijana wote ambao sifa zao zinakuwa pungufu wanachukuliwa na wanalinda katika maeneo mbali mbali katika sekta binafsi, iwe mahoteli, iwe katika maeneo ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, Sasa nimuombe Mhe. Waziri hebu ajaribu kufanya mashirikiano ya dhati na tuone namna gani kwa kupitia Idara Maalum tunaweza kuwachukua vijana wetu kupita pale kupata mafunzo baadae kuanzishwa kitengo maalum cha ulinzi ili tuondokane na suala la kulindwa na Wakenya na Waganda wakati vijana wetu wanahangaika katika suala zima la kutafuta ajira. Hilo ni eneo moja.

Mhe. Naibu Spika, Lakini eneo la pili ambalo nilikuwa nataka kuzungumzia katika masuala mazima ya maslahi ya wafanyakazi, wengi wamepiga kelele na ni kweli lazima tukiri, bado kima cha mshahara hakiridhishi kabisa, na watu wengi walikuwa wanategemea na tumekuwa tumejenga mazoea kwamba wenzetu upande wa pili wa Tanzania Bara wakiongeza mshahara basi na wenzetu huku wa Zanzibar wanakuwa wanafikiria kusubiri kuongezewa mshahara. Lakini tumesikia kauli za viongozi wetu kwamba hali sio nzuri na wamejikita zaidi kufanya marekebisho ya mishahara mule ambamo imeonekana bado kuna matatizo madogo madogo hayajakaa sawa, silikatai hilo.

Mhe. Naibu Spika, Lakini niombe tu Wizara kufanya jitihada basi kwa yale maeneo ambayo yanaonekana bado yana matatizo kwa wale wafanyakazi wetu ambao *scheme of service* hazijafanywa vizuri, yaani unamkuta mwenzake anapandishiwa yeye ana muda mrefu yaani tumejikita zaidi katika kungalia katika eneo la watu ambao wana taaluma zaidi. Lakini tumesahau kuangalia maeneo yale ya watu wazoefu na watu wenye ujuzi hawa ndio wanaoteseka zaidi. Kwa hivyo, niombe Mhe. Waziri kufanya jitihada za kutosha ili kuondosha ile migongano midogo midogo na manung'uniko ambayo yaliyopo katika hayo maeneo ya wafanyakazi wetu.

Mhe. Naibu Spika, chengine ambacho ninachotaka nikizungumze hili sitolizungumzia sana lakini ni wakati na mimi angalau nitie barka ili wale watendaji ambao wanahudumia katika ofisi yetu wasije wakasema aa Mhe. Ali yeye kidogo anaonekana hatupendi hakulizungumzia.

Mhe. Naibu Spika, Suala la wafanyakazi wa Baraza katika masuala mazima ya maslahi yao, Mheshimiwa hili silizungumzi sana nakazania pale wenzangu wameshazungumza kwa nguvu, kwanza lazima tuangalie kitengo chetu namna ya kuweza kukifanyia maslahi yao ili kuendana na Mabunge ya wenzetu. Hiki chombo kinajitegemea na kuna fununu ambazo zinasikika labda kutokana na urasimu wetu umefikia pahala kwamba lile fungu lao limeweza kurejeshwa halikuweza kutumika kwa sababu ya urasimu wetu. Hebu tuondoshe huu urasimu ili hii taasisi nayo iweze kupata tena yale maslahi ambayo tunategemea.

Mhe. Naibu Spika, Chengine niliangalia ukurasa wa 13 katika kirumi (ii) kilikuwa kinazungumzia juu ya suala la mafunzo kwa watendaji wetu, nimekuwa na kilio kidogo sana, mimi niiombe Wizara iwe makini katika kuangalia suala la Idara zetu katika mawizara mbali mbali katika kuwasaidia vijana wetu kwenda kupata mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, kumekuwa kuna upendeleo sana, kumekuwa kuna upendeleo katika kuwapa watu kwenda kupata mafunzo katika maeneo mbali mbali. Tunachoangalia zaidi udugu unakuwa unatawala, urafiki unatawala. Sasa tuangalie kuona kwamba kila mwenye haki ya kupata mafunzo basi utaratibu mzuri unatumika katika kutoa mafunzo.

Mhe. Naibu Spika, Mimi nishukuru sana suala hili Mhe. Naibu Spika, lilikuwepo katika maeneo ya Idara Maalum, Idara Maalum ilikuwa anatoka depu leo hakai miezi mitatu anapanda *rank* lakini utakuta mtu ana miaka 13 bado yuko *private*. Lakini nimshukuru Mhe. Waziri ameliona haraka hili na amejaribu kulifanyia kazi; kuona kwamba mtu atakwenda *rank* kutokana na muda aliyoingia na uwezo wake wa kielimu. Sasa na katika maeneo mengine nilikuwa naomba tuliangalie zaidi tulione ili kwamba hii fursa ya kutoa mafunzo kwa wafanyakazi isiwe inaangaliwa katika hali ya upendeleo kabisa.

Mhe. Naibu Spika, Nakuja katika suala la Kamisheni ya Kazi katika suala zima la wazawa kupewa kipaumbele. Ni kweli tumeipiga kelele kuna maeneo ambayo hayastahiki kumkuta mtu mgeni anapewa cheo au anapewa nafasi ya juu katika kuongoza *management* za mahoteli, hususan katika ma-*garden* na masuala mengine ambayo ni masuala ya kawaida tu. Leo katika suala la *garden* unamkuta bosi anatoka Kenya. Katika suala la mapishi unamkuta bosi anatoka Arabuni.

Mhe. Naibu Spika, Ninafikiri ni suala ambalo la kuanza kuangalia wazawa, na hususan nitoe pongezi za dhati kabisa, na ninafikiri katika bajeti itakayokuja ya Wizara ya Elimu kutakuwa kuna sera ambayo imetengenezwa nzuri sana. Na niwashukuru wenzetu wa *SUZA* kwa kuandaa utaratibu uliokuwa mzuri wa kuanzisha Shahada ya Kwanza katika mafunzo kama haya maeneo kama hizi sekta binafsi. Kwa sababu tunajua wakati mwengine tunahisi labda kazi watu wanaziweza lakini wenzetu wanaangalia zaidi cheti.

Mhe. Naibu Spika, Sasa niwashukuru ndugu zetu kwa kuandaa hizi taaluma, lakini pamoja na hayo ninafikiri kuna haja ya kuangalia wenzetu zaidi katika suala zima la kuwapa wazawa kipaumbele, katika suala la ajira la sekta binafsi.

Mhe. Naibu Spika, Jengine na la kumalizia mwaka jana wakati ninachangia bajeti hii na nilikuwa mkali sana juu ya suala la upotevu wa malipo ya wanafunzi katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Nilijaribu kulipigia kelele na nikaambiwa litafanyiwa kazi lakini bado sijapata uhakika wake ni hatua gani ambazo zimeweza kuchukuliwa, hivi niombe tu Mhe. Waziri atapokuja basi anieleze kwamba ile kadhia iliyojitokeza ya ubadhirifu katika Chuo cha Utumishi wa Umma labda Wizara au Serikali ilichukua hatua gani kwa yule muhusika.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya hayo nilisema kwamba leo nitakuwa na machache sana sitozungumza mengi. Mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwahani ninaunga mkono hotuba ya Mhe. Waziri. Ninakushukuru Mheshimiwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii angalau nitie barka kidogo katika hotuba hii ya Mhe. Waziri, nataka nianze kwa kumuombea Mungu amjaalie afya njema zaidi hii aliyonayo. Tunajua kwamba Mhe. Waziri alipata misukosuko mikubwa na *alhamdulillahi* Mwenyezi Mungu kamsaidia, lakini tunaomba amsaidie zaidi ili awe na afya nzuri zaidi.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na ukurasa wa 29 kitabu cha Mhe. Waziri, kuna Idara ya Ajira na malengo ya mwaka 2013/2014 ilikuwa ni kutoa ajira 2000, zilizopatikana kwa mujibu wa taarifa zake ni ajira 1609 na zote hizi ni kupitia taasisi binafsi.

Mhe. Naibu Spika, Sasa mimi kwanza nilikuwa na swali kwa sababu unapokuwa na mipango mizuri basi unapaswa kwanza kujua changamoto uliyonayo na namna ya kuitatua. Sasa nilipaswa kwamba Mhe. Waziri atueleze kwanza mahitaji ya ajira ya vijana wetu Zanzibar ni vijana wangapi ambao wanahitaji ajira, japokuwa kila mwaka wanaongezeka lakini kwa ule mwaka husika, ni watu wangapi ambao wangehitaji kuajiriwa hata akapanga mipango ya kuajiri watu 2000 kwa mwaka, hilo la kwanza.

Mhe. Naibu Spika, Lakini la pili, angepaswa atwambie vile vile katika hili serikali watabeba asilimia ngapi katika watu 2000 na asilimia ngapi itakwenda kwenye sekta binafsi, lakini taarifa hizo zimekosekana. Nilikuwa naomba sana mwaka ujao Mhe. Waziri atupe taarifa za aina hiyo ili tujue asilimia ngapi tunaweza kutatua matatizo ya ajira katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuna taarifa tunazipatapata humo katika maidara humo tunamopita kuwa kuna vijana wameajiriwa, tumeajiri watu wangapi katika hizi taasisi za serikali. Lakini hizi taarifa hazipo hapa au sijui Idara hii inahusika na Idara gani, maana tulipaswa na hawa wote wajumuishwe tuambiwe kama serikali imeajiri watu wangapi na hawa wamekwenda kwenye sekta binafsi. Huu ni wakati wa uwazi, si wakati wa kufichaficha, taarifa hizi ni muhimu sana, nataka kuona maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nimuulize Mhe. Waziri au niiulize serikali, yeye ni kwa niaba ya serikali hapa kwamba miongoni mwa hizi ajira, ajira 859 vijana wameajiriwa nje ya nchi tukatajiwa wameajiriwa Qatar, Djibout, Oman, Yemen na kwengineko. Sasa nilikuwa niulize kidogo hapa kwamba je serikali ina mpango gani wa kufuatilia maendeleo ya hawa vijana wanaopelekwa nje ya nchi na angalau serikali inakuwa na mawasiliano kuwajua walimo na wanavyotendewa huko walikwenda kuajiriwa.

Mhe. Naibu Spika, Maana yake hapa ndani ya nchi tuna sheria kila mwajiri anatakiwa aifuate hiyo sheria kuhakikisha kama maslahi ya yule aliyemuajiri yanatekelezwa. Lakini hao wanaokwenda huko nje, vipi serikali inapata taarifa zao.

Mhe. Naibu Spika, Ninasema hivi kwa sababu tunapata taarifa si nzuri kabisa, vijana wetu wanaotoka hapa kwenda kuajiriwa huko wanapata idhilali kubwa sana. Ukienda katika familia zao mara nyengine unaweza ukapata maneno ya kusikitisha kweli kweli, na yule kijana kule ni mgeni pengine hajui namna ya kurudi kama angekuwa anajua angekuwa tayari kesharudi kwao kwa idhilali wanayoipata kule.

Mhe. Naibu Spika, na tusije tukafika pahali ikaonekana tunarudisha enzi za utumwa, maana yake mtumwa alikuwa anachukuliwa hapa Zanzibar anapelekwa nchi za nje kwenda kufanyishwa kazi isivyo halali. Sasa ikiwa vijana wetu katika wakati kama huu tulionao wanachukuliwa kwenda kufanywa watumwa nchi za nje, mimi sidhani kama ni jambo zuri.

Kwa hivyo, lazima hawa mawakala, kwa sababu nasikia kuna mawakala wanaochukua vijana wakipeleka nje, lazima waekewe masharti humo wanamowapeleka hao vijana wawe wanawafuatilia je wanatendewa vizuri, siyo vijana wa Kizanzibari watoke hapa halafu waende wakadhalilishwe katika nchi za kigeni ni hatari mno. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana Mhe. Waziri atupe taarifa kwamba hawa vijana huko nje wanafuatiliwa.

Mhe. Naibu Spika, Jengine ni kuhusu hizi taasisi ambazo zimo humu ndani sasa, taasisi binafsi hizi ambazo zinatoa ajira. Kwanza tunawashukuru wanatusaidia sana kwa sababu Serikali yenyewe haina ajira za kutosha na haina uwezo, lakini wao wanatusaidia kuchukua vijana, lakini sasa wawatendee vyema kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, kuna taasisi hizi haziwatendei watu vyema; anaajiriwa mtu hajazishwi mkataba miaka mitatu au minne inapita, na kwa sababu hajazishwi mkataba wanamfanya wanavyotaka, wanamkata mshahara wake. Kuna taasisi fulani hapa imeajiri vijana vile wakiwa wanataka kuwaajiri wanawaambia mshahara wako wewe utakuwa huu, lakini anaajiriwa anapewa robo ya ule mshahara akiuliza anaambiwa aah kama unataka kazi vumilia, kama hutaki kazi basi tukuachishe. Na yeye ni masikini ya Mungu atavumilia anakatwa mshahara miaka mitatu hajalipwa mshahara wake, siyo haki kabisa.

Mhe. Naibu Spika, halafu siku nyengine anaweza akaachishwa kazi bila ya kupewa mafao yake, na hivyo akipewa anapewa robo hapewi kamili, kwa sababu gani? Mhe. Waziri hayo masuala yanahitaji kufuatiliwa kweli kweli, vijana wetu wanadhalilishwa hapa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, Jambo jengine ambalo nalo ni muhimu kabisa kuna Idara hii ya Usalama na Afya Kazini, hii idara ni mpya watu wengi hawajajua maendeleo na umuhimu wa hii idara. Lakini ni idara muhimu sana kwa sababu mfanyakazi yeyote anahitaji kuwa salama pale anapofanya kazi, lakini anahitaji kuwa salama, anahitaji kuwa na afya nzuri. Sasa muda mwingi nchi haikuwa ikizingatia haya mambo na utakuta majengo mengi ya Serikali hayakujengwa kiusalama.

Mhe. Naibu Spika, Nitoe mfano kwanza hili Baraza la Wawakilishi hata kama limejengwa juzi milango hii kwa mfano hapa tunatokea mlango ule pale tu, ikitokea zahma tutauana hapo njiani, hii milango ya pembeni ipo lakini haiko *free* ina *lock* hii, hata ukienda ukitafuta ufunguo huko ofisini basi ukija hapa watu wameshaumizana, si vizuri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, pale Hospitali ya Mnazi Mmoja pale palikuwa na ngazi tatu za kupandia juu na kuteremkia, leo pale kuna ngazi zimefungwa ile hospitali inaweza kuchukua watu zaidi ya laki tatu kwa wakati mmoja kule juu, ikitokea zahma kule watu watatokea wapi watakufa kwa kukanyagana. Sasa mimi nafikiri idara hii iwezeshwe vya kutosha ili iweze kukagua majengo mengi ya Serikali ambamo wafanyakazi wamo na kutoa ushauri wao, na ikiwezekana huo ushauri ufanyiwe kazi, siyo tunaambiwa hapa inapewa *other charges* hazifiki hata asilimia 50. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri hilo ni jambo muhimu sana.

Mhe. Naibu Spika, halafu wafanyakazi wetu wengi wao wanafanya kazi katika mazingira ya hatari, kwa mfano hata walimu wa skuli. Walimu wa skuli maisha yao yote ni ya hatari kwa sababu ya kutumia ile chaki, ile chaki lile vumbi lake siku zote mwalimu analitia ndani ya mwili wake lile. Hivi kuna utaratibu gani wa kumsaidia yule mwalimu, kuna wafanyakazi wa Wizara ya Afya wanafanya kazi katika mazingira magumu wanapambana na maradhi mengine ambukizi, kuna utaratibu gani wa kuwasaidia.

Mhe. Naibu Spika, Kuna maposho fulani hata juzi nimepata mfanyakazi mmoja sijui nani kanambia kuna maposho fulani walikuwa wanapewa kama *risk allowances* sasa zimekatwa. Hivyo nilikuwa naomba hii idara ipatiwe uwezo na ifuatilie mambo haya kutoka taasisi moja moja ili wafanyakazi wetu wawe salama na wawe na afya njema.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na Kamati yangu ya Katiba na Sheria, lakini niungane na Wajumbe wengine walioonesha mashirikiano yao makubwa kuhusu hii Idara ya Nyaraka.

Mhe. Naibu Spika, hii Idara tuliitembelea pale kwa kweli haiko katika hali nzuri hata kidogo, hasa ukilinganisha na unyeti wa idara hii na vile inavyokuwa *treated* havilingani kabisa. Tumekwenda pale vile viti vya kukalia na siku nyengine pale unapata wageni muhimu wanafanya *research;* wazungu, tumekwenda kumkuta mzungu amekaa kwenye kiti kile kiti kimefungwa kamba ya mkonge kisianguke, ile miguu yake maana yake. Mimi nikawa najiuliza hii idara inafanywa kama mtoto wa kambu kwa sababu gani? Mkurugenzi mzima hana hata kigari cha kutembelea anaazima gari kutoka idara nyengine, yule mzee wa watu jamani, kwa nini inakuwa hivi inatelekezwa hii idara hii. Jengo lile mule ambamo mnahifadhiwa nyaraka huwezi kukaa hata dakika tano utapata mafua.

Mhe. Naibu Spika, mimi nashangaa kweli kwa sababu wenzetu katika pahali ambapo wanapatunza duniani ni pale, kwani pana urithi wa nchi hakuna nchi isiyokuwa na historia. Leo tunaidharau namna ile nyaraka zinanyambuka hizi zote zinanyambuka hazina matunzo, idara yenyewe mwaka mzima inazuiliwa *other charges* shilingi milioni kumi na tano, *four percent* ya mwaka mzima ndiyo tunafanya nini jamani.

Mhe. Naibu Spika, Sasa mimi nilikuwa nadhani kwanza hii idara ilitungwa sheria Nam. 3 ya mwaka 2008 na kwa mujibu wa sheria inatakiwa iwe na fungu lake; ni taasisi, na taasisi inakuwa na fungu lake, siyo pesa zigaiwe na Katibu Mkuu halafu awape shilingi mia mbili hawana vya kuzitumia. Kwa hivyo, ipatiwe fungu lake halafu ipewe fedha za kutosha za kuhifadhi zile nyaraka, kwani zile nyaraka zinapotea kwa asilimia kubwa sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, kuna nyumba pale kila tukienda ile nyumba lile geti la ile nyumba liko pale kwenye mlango wa ile ofisi yenyewe. Tunahoji kwa nini huyu hahamishwi? Ukihoji hivyo wanakwambia aah kaweka bili kubwa mwenyewe mpaka nyumba yake sijui anauza milioni mia ngapi, utaratibu kwani unakwenda hivyo?

Mhe. Naibu Spika, kama ardhi inatakiwa kwa maslahi ya jamii kuna sheria zake, sheria zifuatwe ile nyumba kama ni kutathminiwa ifanyiwe tathmini kwa mujibu wa soko la wakati huu, lakini kwa vyovyote pale ufike wakati pale aondolewe yule na ile sehemu iwe ni ya ile ofisi yetu au kama hatuwezi hivyo tunamuheshimu sana yule bamkubwa pale, basi tuhamishe ofisi yetu tukatafute pahali pengine tuwajengee watu wa taasisi ya nyaraka. Lakini ile haileti usalama pale na kuna siku itakuja kutokea hatari pale, kwa nini inakuwa hivi?

Mhe. Naibu Spika, baada ya kusema machache sana mimi naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, Ahsante kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma.

Mhe. Naibu Spika, kwanza sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kutupa nafasi kufika hapa tukiwa wazima wa afya tukaweza kuchangia bajeti hii. Vile vile, nimpongeze Mhe. Haroun Ali Suleiman kutokana na afya yake inavyoendelea kuwa nzuri Mungu amsaidie iendelee vizuri.

Kwanza nachangia ukurasa wa 29 kifungu cha 52 kuhusu Ajira.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hivi sasa nchi yetu ina matatizo mengi ya ajira ambayo inaongozwa na ofisi hii kuhusu sekta maalum za watu binafsi pamoja na sehemu zingine ambazo zinashirikiana na serikali ili kuwapatia ajira vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, Hivi sasa serikali imejipangia kuweza kutoa ajira 2000 kwa vijana wetu kwa mwaka huu 2013/2014 ili vijana hawa wapate nafasi muhimu za kuweza kupata ajira. Nikiangalia hivi sasa serikali haina

sehemu nyingi ambazo zinaweza zikasaidia ajira kwa vijana wetu. Lakini kwa hivi sasa nafasi nyingi za ajira binafsi zimo na hizo ndizo ambazo tegemeo kubwa la serikali na ndiyo imeweka kipaumbele ofisi hii ili isaidie vijana.

Mhe. Naibu Spika, Hivi sasa utaona kwamba kuna nafasi muhimu kwamba kuna viwanda vidogo vidogo, hivi sasa viwanda vingi vimefunguliwa vidogo vidogo; kama kuna viwanda vile vya kusindika maziwa kwa Bakhressa iweje ikose vijana wazalendo angalau 500 kufika kwenye kiwanda kile, na utakuta kiwanda kile kimeanza kazi lakini utakuta vijana wetu bado wanahangaika hawajaweza kupata ajira kama hizo ambazo ni muhimu.

Mhe. Naibu Spika, Serikali hivi sasa imetoa nafasi kubwa kwa ajili ya sekta ya utalii, kuna mahoteli mengi sana ambayo yanahitaji vijana wetu waweze kupata ajira hizi, lakini utakuta kwamba vijana wanaoajiriwa katika nafasi zile ni wengi kutoka nje ya nchi. Ukiangalia vijana wengi katika mahoteli hayo wengi wao ni Wakenya na kuendelea juu.

Mhe. Naibu Spika, Kwanza ofisi hii ihakikishe kwamba wazalendo wanapata ajira katika sehemu hizi ambazo zimewekeza Serikali. Kwanza washughulikiwe vijana hawa kwa zile ajira zinazopatikana hasa zile ndogo ndogo ambazo za vijana wetu kuanzia *form two* na kushuka chini. Nafasi ambazo zimo katika hoteli hizo ambapo haina haja ya kupata wageni na nyingi zao utakuta wageni ndizo wanazozishikilia.

Mhe. Naibu Spika, Kama vijana wetu ambao wana uhakika wa kuweza kufanya Shughuli za usafi; mambo ya usafi kwa kweli haihitaji lazima wawe na chuo au wawe *form six*. Lakini utakuta mambo haya ya usafi wa sehemu za mahoteli wote ni kutoka nje ya nchi hii, hivyo inashangaza sana kwamba lengo la serikali halifikiwi.

Mhe. Naibu Spika, mimi namshauri Mhe. Waziri anihakikishie kwamba ni vijana wangapi hivi sasa wazalendo ambao wako katika mahoteli ambayo yamefunguliwa hivi karibuni. Utakuta mahoteli mengi ambayo ingeliwezekana kila hoteli ingechukua hata vijana 30 ambao ni wazalendo basi ingekuwa tatizo la ajira katika nchi yetu lingekuwa ni ndoto. Lakini utakuta katika hoteli utakwenda kuuliza vijana wangapi ni Wazanzibari hutozidi kwenye vijana watano ama kumi, na wote hao utakuta wanawekwa katika sehemu za mitaro ama kusafisha bustani.

Mhe. Naibu Spika, Kwa kweli Mhe. Waziri akija nataka anihakikishie kwa kila hoteli ina vijana wangapi na ambao wote wanafunga *tag* ya kuonesha kwamba wale ni vijana kutoka wapi, na hasa tuhakikishe ni wa Zanzibar, na kama wa Zanzibar tusome *tag* zao zimeandika kwamba kila Mkoa angalau watu wanne ama watano wamepatikana katika mahoteli. Lakini utahakikisha kwamba ukienda katika hoteli huwezi ukapata kijana ambaye unamfahamu huyu ametoka Mkoa wa Kusini, angalau Wilaya ya Kati ama Jimbo la Koani, hilo ni jambo adimu sana katika mahoteli yetu.

Mhe. Naibu Spika, namuhakikishia Mhe. Waziri kama ataweka mbele suala hilo basi atapata sifa katika wizara yake, na kwa hakika hapo tunaweza tukaipitisha bajeti hii na tukasema kwamba bajeti aliyopewa ni ndogo na inawezekana kwamba tusiipitishe ili aongezewe fungu la fedha na aweze kuhakikisha kuwapatia ajira vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nichangie ukurasa wa 32 kifungu cha 57 kuhusu Idara ya Usalama nafasi za kazi. Kwa kweli vijana wetu wanafanya kazi katika sekta nyingi, lakini vijana hawa wanakosa haki zao za msingi pale wanapopata matatizo katika sehemu zao za kazi. Wengi wao wakipata ajali katika sehemu za kazi kama gari limeanguka wakati wa kwenda safarini kama sehemu za mahoteli ama wameanguka katika sehemu za kupanda ghorofa wakati wa utengenezaji basi si wengi ambao wanapata kuhudumiwa katika mahoteli hayo, na matokeo yake mtu huyo inakuwa ajisaidie mwenyewe ama familia yake ndiyo imsaidie.

Mhe. Naibu Spika, mimi namshauri Mhe. Waziri anapopata tatizo la vijana kama hao ahakikishe kuibana hoteli ama wizara yoyote ya binafsi kama vile viwanda ama sekta maalum za usafi wa mji ili vijana wale wahudumiwe na waweze kupata haki zao za msingi. Kwa kweli vijana wengi wanapata ulemavu na utakuta kwamba hivi sasa hawashughulikiwi na sekta binafsi ili wakapata haki zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, vile vile, nichangie ukurasa wa 23 kifungu cha 42 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu. Kwa kweli hivi sasa serikali yetu ina sehemu nyingi sana za kumbukumbu katika Wilaya zetu na Mikoa yetu. Lakini utakuta kumbukumbu hizo yamejengwa magofu hazishughulikiwi wala hazina wafanyakazi. Mimi nashauri kwamba ofisi hii na sehemu hizo za nyaraka hivi sasa ni bora zibinafsishwe kwa watu binafsi pamoja na kumbukumbu ili wapate vijana wetu kuajiriwa katika vijiji vyao ili wahakikishe kumbukumbu hizo zinafanywa vijijini kuliko kujengwa tu magofu yale na hayashughulikiwi chochote.

Mhe. Naibu Spika, Utakuta kuna sehemu nyingi sana kama mimi mwenyewe nina uhakika katika jimbo langu sehemu za Unguja Ukuu kule kumejengwa jumba la kumbukumbu kwa muda mrefu sana, lakini jumba hilo mpaka leo halina wafanyakazi na wala halina kumbukumbu yoyote ambayo imewekwa ndani, basi angalau wangewekwa paa wa vijijini ingelikuwa watalii wanaenda kuona paa.

Mhe. Naibu Spika, Kuna wanyama wazuri kule sehemu za kwetu ambao ni adimu sana kama wale n'gombo, n'gombo ni wanyama adimu sana kuwaona na kwetu wanapatikana sana, kwa nini sehemu ile isibinafsishwe wakapewa wananchi, na hasa utakuta jumba lile limejengwa kwenye shamba la wananchi na limechukuliwa katika sehemu ya mwananchi amechukuliwa eneo lake la ardhi; na ardhi hiyo hakulipwa na limejengwa lile gofu limekaa pale hivi sasa halipungui miaka kumi limekaa tu.

Mhe. Naibu Spika, namshauri Mhe. Waziri alichukue jengo hilo na libinafsishwe kwa wananchi liweze kutoa ajira kwa vijana wetu, hapo ndipo na mimi inawezekana nikahakikisha kwamba bajeti hii nikaipitisha kwa fungu kubwa sana, ama nitaondoa shilingi yangu kama Mhe. Waziri hatoweza kuhakikisha vijana wetu wanapewa magofu yale kuweza kuwapatia ajira.

Mhe. Naibu Spika, Kwa vile Mhe. Waziri sehemu hiyo ameitembelea na anaifahamu, nashauri achukue nafasi hiyo ili kutoa nafasi kwa vijana au kwa vijiji waweze kuhakikisha kwamba maeneo yote yanaweka usafi na kwamba vijana wanatunza majumba hayo ili wahakikishe magofu yote ambayo yako katika Mikoa yetu yanaweza kupata huduma na kuwa safi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kuchangia kwenye kifungu hiki cha magofu nahakikisha pale kwa Bi Hole hivi sasa ni sehemu kubwa sana ambayo ya kupigiwa mfano, na sehemu hiyo kwa muda mrefu ni historia ya tangu miaka na miaka.

Mhe. Naibu Spika, Historia ile sasa kwa kweli haina utunzaji na wananchi wanaitafuta sana ili sehemu ile wapewe vijana waweze kuiendesha na kuhakikisha magofu yale yanakaa katika hali nzuri, pamoja na ile miembe ya Bungi ni sehemu nzuri sana ya mambo ya kale ambayo wapewe wale vijana waweze kuhakikisha kwamba wanatunza sehemu zile ili wananchi waweze kupata ajira angalau waangue hata zile embe ziweze kusafirishwa nchi za nje. Lakini utakuta maeneo yale kwa kweli hivi sasa hayashughulikiwi na wizara hii ambayo inaweka magofu sawa.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ingawa muda wenyewe si mkubwa sana kwa leo nahakikisha kwamba bajeti hii kwa kweli iweze kuhakikishwa kwamba tunaipitisha, na tunahakikisha inapata mchango wetu mkubwa wa kuweza kupata fedha na kuweza kuendesha mambo mengi ya ajira. Pia ihakikishe kuwa Mhe. Waziri hiyo michango ambayo tunaitoa iweze kufika kwa vijana, kwani vijana hivi sasa wana kiu kubwa ya maendeleo hasa kwa kupata ajira katika sehemu za mikoa yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi leo nitaiunga mkono bajeti hii pindi Mhe. Waziri atakapohakikisha kwamba sehemu zote za magofu ambazo hazitunzwi na Serikali yanarudishwa ili kubinafsishwa kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, Kwa leo mchango wangu nitaunga mkono sekta hii pindi Mhe. Waziri atakapounga mkono. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha kikao naomba nizungumze mambo matatu.

Suala la kwanza, niwashukuru kwa kuweza kupitisha bajeti ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora, na pia tumeanza hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma, nashukuru kwamba tumekwenda vizuri na mumenipa mashirikiano mazuri. Lakini niwashauri Waheshimiwa Mawaziri kwamba tumebaini katika vitabu vyetu mna makosa madogo madogo na tunakuja kubaini wakati wa kupitisha vifungu, hivyo yanaleta usumbufu. Kwa hiyo, nashauri wale wote ambao hotuba hawajawasilisha wakae na watendaji pamoja na Wenyeviti wa Kamati ili kuweka marekebisho tukija kwenye vifungu tupitishe bila ya tatizo lolote.

Suala la pili, nimepewa tangazo niseme na Mnadhimu wa CCM kwamba wale Wajumbe wa CCM tukimaliza kikao hiki wabakie kwa dakika tano kuna maelezo muhimu. Baada ya hayo naomba kuakhirisha kikao chetu hadi kesho tarehe 29 siku ya Alkhamis saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:42 usiku Baraza liliakhirishwa mpaka tarehe 29/05/2014 saa 3:00 asubuhi)